ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID - SPIKA

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki

11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera

22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa

39. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
54. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake

80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TISA

WIMBO WA TAIFA WA ZANZIBAR

Kikao cha Kwanza - Tarehe 7 Februari, 2018

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwanza nichukuwe fursa hii kuwakaribisha sana katika mkutano wetu huu wa Tisa wa Baraza letu la Tisa ambao unaanza leo tarehe 7 Februari, 2018. Waheshimiwa Wajumbe napenda kutoa kwenu na kwa wananchi kwa jumla taarifa kuhusu Miswada ya sheria iliyopitishwa katika mkutano uliopita wa Baraza uliofanyika kuanzia tarehe 6 Disemba, 2017 mpaka tarehe 15 Disemba, 2017, katika mkutano wa nane wa Baraza la Tisa la Wawakilishi Baraza hili lilipitisha Miswada minne ya sheria ambayo ni kama hii ifuatayo:-

1) Mswada wa Marekebisho ya sheria mbali mbali na kuweka masharti bora ndani yake na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

2) Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo vidogo na vya Kati Zanzibar pamoja na kuwezesha ushajiishaji na uwendeshaji wa Viwanda Vidogo

vidogo na vya Kati Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

3) Mswada wa Sheria wa Kuanzisha Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar na kuweka vifungu vya Usajili pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

4) Mswada wa Kufuta Sheria ya Uchaguzi namba 11 ya mwaka 1984 na kutunga sheria ya Uchaguzi ya mwaka 2017 na maswala mengine yanayohusiana na hayo.

Waheshimiwa Wajumbe kama inavyotakiwa chini ya Kanuni ya 91(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2016 naomba kutoa taarifa kwamba Miswada hiyo yote niliyoitaja sasa imekuwa sheria kamili baada ya kusainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru sana.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kutukutanisha tena katika Baraza hili tukufu na kuendelea na shughuli zetu kama zilivyopangwa. Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika sasa kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na Vijalizo vyake kuanzia Tarehe 16 Disemba, 2017. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba niwasilishe mezani Mswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya Kusimamia Mwenendo wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji ya Zanzibar namba 2 ya mwaka 1995 na kutunga sheria mpya ya ushindani halali wa biashara na kumlinda mtumiaji wa kuweka

masharti bora zaidi pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Kilimo: Mhe. Spika, naomba kuweka hati mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya kusimamia mwenendo wa biashara na kumlinda mtumiaji namba 2 ya mwaka 1995 na kutunga sheria mpya ya ushindani halali wa biashara na kumlinda mtumiaji na kuweka masharti bora zaidi pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 74

Kufungua Ubalozi Mdogo Zanzibar

Mhe. Simai Mohamed Said - Aliuliza:-

Kwa kuwa nchi ya Qatar na wananchi wake wanatafuta fursa za kibiashara kutoka nchi tofauti.

Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haioni umuhimu wa kufungua ubalozi mdogo hapa *(Consulate General)* kwa ajili ya kushawishi wafanyabiashara tofauti.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 74 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ufunguaji au uanzishaji wa Ofisi za Balozi kubwa, ndogo na heshima unategemea nchi husika *(Sending State)* kuona umuhimu wa kuanzisha Ofisi hizo, kutokana na sababu hizo Serikali hii ya Zanzibar (*Receiving State*) kitaalamu haina mamlaka ya kufungua Ofisi hizo au za aina hiyo.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inachoweza kukifanya ni kuzishawishi na kuzivutia nchi mbali mbali kufungua Ofisi ndogo za kibalozi hapa Zanzibar ili kuweza kufaidika na fursa za uwepo wa Ofisi hizo na kazi hiyo inaendelea kufanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia ofisi zake nashukuru Mhe. Spika.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri ambayo amejibu swala langu lakini ningependa nimuulize swali dogo la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Mhe. Spika, kwa kuwa miaka nenda miaka rudi Zanzibar tumekuwa tuna ofisi ndogo hizi za Kibalozi kama ya China, India, Oman, Misri, Mozambique nafikiria labda na mbili tatu nyengine, lakini hali ya wa Zanzibar katika kujiendeleza kiuchumi au katika kufanya shughuli zao za kila siku wamekuwa sana sasa wanapita katika nchi za katikati za Ughaibuni hasa Dubai lakini Qatar wakuwa mmoja katika mstari wa mbele kuweza kushiriki hata ndege yao sasa inatuwa mpaka Zanzibar.

Je ni ushawishi gani ambao Serikali wanohitaji ili kuhakikisha kwamba sasa wanaweza kufungua ubalozi mdogo hapa Zanzibar lakini (b), Nchi ya Qatar ni nchi moja katika ambayo imepangwa kwamba watakuwa wao ndio waandaaji katika kombe la Dunia mwaka 2022. Jee Serikali ya Zanzibar haioni umuhimu wa kuangalia fursa hizi katika kukuza uchumi pamoja na kuitangaza Zanzibar kuwaalika hawa watu kutoka nchi ya Qatar kuja

Zanzibar ili kuangalia uwezekano huu kufungua ofisi ndogo. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusua yako na kwaniaba ya Mhe. Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mhe. Simai Mohammed Said yote kwa pamoja.

Mhe. Spika, kama ambavyo nimezungumza katika jibu langu la msingi, kinachoifanya Serikali ni kufanya ushawishi na kusikiliza Balozi ambazo zipo ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo kinachotufanya sisi ni kuweka mazingira bora ili wao wenzetu wapate kuvutiwa na kile ambacho tumekuwa tukikifanya, zipo nchi ambazo tunao na tunaona sababu kama Serikali kuwa na ofisi ndogo kwa mfano kama wenzetu aina ya watu wa Italy na wengine ambao tayari ukitizama mahusiano yetu na wao ni makubwa mno hasa katika *Industry* kubwa ya utalii. Sasa hata hili ambalo analisema Mhe. Mwakilishi wa Tunguu swala la wenzetu wa Qatar hata sisi fursa hizi tunaziona na tunatamani lakini mwisho wa siku bado yale mamlaka ya kuanzisha ofisi ile ipo katika nchi husika na ubalozi husika sio jukumu letu sisi kama serikali tutakavyopata ombi lile au agizo lile tunachokifanya ni kuweka mazingira stahiki na bora zaidi ili wao kuweza kuja kufungua hizi ofisi zetu.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika nikushukuru, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, nilikuwa na swali dogo tu nataka kumuuliza, kwa kuwa swali la Ubalozi ni jambo jema katika kukuza uchumi na *diplomasia*. Je Wizara yako kupitia Serikali ina utaratibu gani iliyojipangia kukutana na balozi mbali mbali katika kutoa ushirikiano wa kukuza uchumi na demokrasia katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Makamu wa Pili wa Rais naomba kumjibu Ali Salum Haji mwakilishi wa Jimbo la Kwahani (Mnadhimu) kupitia Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Spika, Wizara yangu kupitia Serikali inafanya jitihada kubwa za kuwa na mashirikiano ya kutosha na mabalozi hasa kwa kupitia Ofisi yetu ya Uratibu iliyopo pale Dar-es-Salaam tumekuwa na utaratibu hata kwa wale ambao wamekuwa na fursa za kupita pale. Ofisi ya Uratibu imekuwa na utarabu wa kwenda kukutana na Mabalozi wa nchi tofauti kuelezea, kutoa fursa na kuelezea mambo mengi ambayo Mabalozi wanaweza wakatoa *invitation* kwa watu wao kuweza kufika Zanzibar. Lakini pamoja na hilo nje tuya kufanya *invitation* ya watu hao kufika Zanzibar wanatengeneza mazingira ya kusema zile fursa ambazo nchi zile ambazo hawazijui Idara ile imekuwa ikizifanya kwa maana hiyo Mhe. Spika, mpaka sasa Wizara yangu imekuwa ikichukuwa jitihada kubwa sana ya kufanya *engagement* ya kutosha kwa ofisi ya kibalozi hasa zile ambazo ziko katika mji wa Dar-es-Salaam nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nakushukuru pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuongezea majibu ya nyongeza kwa Mhe. Ali Salum Haji kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Ofisi yetu kupitia kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais mwenyewe amekuwa akikutana na Mabalozi mbali mbali na akikutana na watu maarufu mbali mbali duniani ambao mara nyingi imekuwa ni kichocheo kikubwa ya kueleza mafanikio makubwa ya Zanzibar na dhamira njema ya Zanzibar katika kuhakikisha kwamba inakaribisha Mabalozi na wawekezaji nchini. Kwa hivyo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais amekuwa

akifanya jitihada hizo na napenda nichukuwe fursa hii nimpongeze sana yeye na Mhe. Rais kwa namna wanavyofanya kukutana na Mabalozi na watu wengine mashuhuri duniani kwa dhamira ya kuelezea Zanzibar na kuvutia uekezaji nchini.

Mhe. Spika, milango yetu iko wazi kwa yeyote yule au mwananchi yeyote yule inaona inahitaji kuanzisha ubalozi kama inatimiza matakwa na masharti kwa mujibu wa taratibu zetu sisi wakati wote tuko tayari kumkaribisha vizuri. Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 69

Matangazo Katika Maeneo Ya Ujenzi

Mhe. Suleiman Sarahani Said - Aliuliza**:-**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahiki pongezi katika juhudi zake za kuleta maendeleo na kuimarisha mambo mbali mbali nchini, hata hivyo, ili kuendana na wakati katika sehemu ambazo ujenzi wa majengo unaendelea huwekwa bao la kuonesha jengo hilo ni la nani na madhumuni yake nini na mwisho huwa kuna maandishi (H.I.V) ya Ukimwi na nembo hiyo huwa kama ndio kibali cha ujenzi na kama ni maradhi yanayotukabili hapa Zanzibar.

(a) Je, maandishi hayo ya (H.I.V) ni lazima yaandikwe ndio upate kibali cha ujenzi.

(b) Je, kuna malipo yanayolipwa kwa ajili ya matangazo hayo.

(c) Je, kama ni janga mbona yapo majanga mengi kama malaria, kipindupindu na huwa hayaandikwi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 69 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda nichukuwe fursa hii fupi kwanza kumpongeza sana Mhe. Mwakilishi kwa namna ambavyo anakuwa akijitahidi sana katika kuuliza maswali katika ofisi hii. Lakini vile vile naomba nichukuwe fursa hii kumpongeza sana kuchukuwa pongezi ambazo amezitoa kwa sababu ameanza na pongezi katika juhudi za Serikali katika kuwaletea maendeleo wananchi wake kwa miradi mbali mbali hapa nchini kwa hiyo kwa niaba ya Serikali nasema kwamba pongezi hizo tumezichukua.

Mhe. Spika, ni kweli katika maeneo ya ujenzi kunakuwa na mabao yanaonesha taarifa za ujenzi pamoja na kuwekwa nembo (alama) inaonesha H.I.V. katika bao hilo ikiwa ni utaratibu tu waliokubaliana wakandarasi, ikiwa ni sehemu ya mchango wao katika vita dhidi ya UKIMWI.

(a) Maandishi hayo hayahusiana na utaratibu wa kupata kibali cha ujenzi.

(b) Hakuna malipo yoyote yanayolipwa kwa ajili ya matangazo hayo.

(c) Hakuna tatizo la kutumika mabao hayo au mbao hizo kuhamasisha jamii katika jengo lolote alimradi muhimu yaendane na mazingira na yasilete tafsiri mbaya katika jamii. Mhe. ahsante.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na nimshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri na pia namimi nichukue pongezi zake kwa Wizara yake kuiuliza maswala mengi pia nami nashukuru. Lakini Mhe. pamoja na majibu yake mazuri nilikuwa nazungumza kwa kuwa Maradhi si kitu kizuri cha kuitangazia nchi na kama ilikuwa kulikuwa na *attention* fulani katika kipindi fulani kwa ajili ya maradhi yale au maradhi mengine yoyote yanayotokea kwa upande wa Zanzibar labda ilifikia hapo hata kwa nchi nyengine nyingi.

Lakini sasa kwa upande wetu suala hili limekuwa kama ndio suala mama la kila siku ambalo nakadiria kama linaitia aibu kama nchi yetu kutokana kwamba ni tangazo kubwa na ambalo halishi na tukitizama *percentage* ni zero *point* zero *one* ni kitu kimoja ambacho kiko chini sana. Lakini wageni wanapokuja na watu wengine wanapoangalia mabango tunaonekana kama kitu hichi kwetu ni kikubwa sana na kinaweza kikaleta hata kama tunaweza tukaandaa mashindano tuseme ya mambo chungu nzima yanaweza kututia dosari kwa sababu sisi wenyewe ndio tulio tangaza.

Namuuliza Mhe. Waziri, je kwa sababu umesema ubao huo unaweza ukatumika kwa jamii ukiachia maradhi hayo kama bado kuna haja ya kuweza kuyaweka hatuna maradhi ambayo ya mripuko kama kipindupindu na sasa hivi kuna maradhi ya ini na mengine yakaweza kuandikwa mengi ambayo yanatuthakili na kama hakuna sababu hiyo kwa nini suala lile lisiondoshwe.

Mhe. Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara

Maalum za SMZ naomba kutoa majibu ya ziada ya Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

Mhe. naomba niseme kwamba matangazo hayo ambayo yametolewa ni kama ambavyo tumejibu hatujapata ambacho tumepata ambacho kinaonyesha kwamba labda kuna madhara fulani kuwepo kuendelea kuwepo mabango hayo. Lakini kwa kuwa jambo hili linashirikisha taasisi mbali mbali ikiwemo Wizara ya Afya wenyewe mimi nahisi kwamba kama kutakuwa kuna lolote ambalo tunahisi kwamba linaweza likaleta madhara basi ni utaratibu tu kwamba labda mutushauri wataalamu, tuweze kuona ni namna gani kwamba tunaweza kuboresha ama tunaweza tukafanya lakini tukumbuke tu kwamba historia ya ugonjwa huu ilivyokuwa imejitokeza kabla ya hapo kulikuwa na tishio kubwa.

Kwa sababu juhudi ambazo za kitabibu zilikuwa kidogo hazijafikia mazingira ambayo kidogo kuna uwezekano kwamba wananchi kupata unafuu, ikaonekana kwamba kila eneo ikabidi kwamba matangazo haya yakaonekana kwamba ni jambo ambalo ni ugonjwa ambalo mtambuka ambalo linapata rika zote ama kwa njia yoyote ile. Sasa ikaonekana ni jambo ambalo historia yake kama tunavyoifahamu Mhe. Spika, kwa maana hiyo sisi kama Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ tutakuwa tuko tayari kupokea taarifa ama ushauri wowote ambao unahusiana na hali hiyo ya kuonyesha kama labda kunaweza kukawa na madhara kama ya nchi, ama ya kiuchumi ama vyovyote vile vile.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Spika, mimi kwanza niipongeze Wizara kuhakikisha kwamba imeweka maandishi ya hali ya hatari katika maeneo ya mkusanyiko kwenye majenzi, hilo ni pongezi za hali ya juu linafaa kupongezwa.

Lakini suala langu liko hapa kwa kuwa Wizara hii inashughulika na masoko na mikusanyiko mbali mbali katika maeneo. Je. Wizara ina mpango gani wa kuweka mabango kama kule sokoni, katika maeneo ya mkusanyiko kwa watu wenye kwenye sikukuu ili kutoa tahadhari kwa janga hili lisiendelee katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba niendelee kutoa majibu ya ziada kwa Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, naomba nirejee kusema kwamba suala la uwekaji wa mabango mara nyingi sisi tunacho angalia zaidi ni mabango ambayo yanayotuhusu moja kwa moja, ni yale ambayo yanahusiana na masuala ya biashara au matangazo ya biashara na mambo mengine. Tunakuwa tuna uratatibu maalum ambao tunaufanya. Lakini namna gani ambayo ya kuweza kuweka mabango yanayohusiana na magonjwa ni jambo la kukaa tukaona namna gani kwa sababu jambo hili kama ambavyo nimetoa maelezo linahusishwa na taasisi nyengine.

Kwa hivyo sisi kama Taasisi nadhani hatuna shida kuhusiana na kupokea taarifa ama maelekezo yoyote ama yanayotolewa na Waheshimiwa ama taasisi nyengine yoyote ambayo inayohusiana na mambo hayo, basi sisi letu ni kufanya hivyo. Kwa kuwa matangazo yale yanakuwa hatutozi hayo basi sisi tuko tayari kuonekana ni namna gani ambavyo tunaweza kusaidiana kwa sababu hili jambo au hili gonjwa ni letu sote na halichagui mtu au rika.

Kwa hivyo Mhe. Spika, naomba nitoe majibu hayo. Ahsante sana.

Nam. 58

Ujenzi wa Madarasa Skuli ya Sizini

Mhe. Said Omar Said - Aliuliza:

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar katika mfululizo wake wa kuendeleza ujenzi wa Madarasa ya kusomea, ilijenga banda lenye jumla ya madarasa matano katika skuli ya Sizini mnamo mwaka 2010 ambalo hadi leo hii halijaezekwa.

Je, Mhe. Waziri unawapa matumaini gani wananchi wa Sizini kutokana na kilio chao cha muda mrefu juu ya banda hili ili watoto wao waweze kulitumia kabla ya kuanguka.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali -Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 58 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara inawapongeza wazazi, wananchi na Wahisani wakiwemo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa juhudi za kushirikiana na Serikali katika ujenzi wa madarasa mapya ili kutatua au kupunguza uhaba wa madarasa uliopo katika skuli au maeneo yao. Serikali imekuwa ikitoa ahadi na itaendelea kutoa ahadi ya kuyakamilisha madarasa yote yanayojengwa kwa nguvu za wananchi yakiwemo ya Skuli ya Sizini.

Ni kweli kuwa ujenzi wa jengo la skuli ya Sizini ulikabidhiwa Wizara mwaka 2010, kwa ajili ya kukamilisha likiwa na vyumba sita, vinne vya kusomea. Mwaka 2011Wizara ilifanikiwa

kuyaezeka madarasa 3, kupiga plasta na kutia sakafu tu. Wizara ilichukua hatua hiyo kutokana na idadi kubwa ya madarasa yaliyokuwa yanahitaji kukamilishwa katika maeneo mbali mbali hasa katika Wilaya ya Micheweni.

Kwa hivyo Wizara inatoa ahadi ya kuyakamilisha madarasa matano (5) yaliyobakia na kuyapaka rangi katika bajeti ya mwaka 2018/2019.

Mhe. Hamida Abdalla Issa: Mhe. Spika, ahsante kwa kuniona pamoja na majibu mazuri ya Mhe. waziri naomba kuuliza Swali moja la nyongeza lenye kitoto (a) na (b).

Mhe. Waziri tunatambua sana jitihada zenu za Wizara yako katika kukamilisha majengo mbali mbali yanayoanzishwa na wananchi naomba kukuuliza suala (a).

a) Kwa mwaka wa Fedha 2017/2018 Wizara yako ilitenga kiasi gani katika kuhakikisha inayamaliza madarasa hayo.
b) Hadi sasa Wizara yako imekamilisha majengo mangapi kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:

Ni kwamba katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imetenga bilioni mbili kukamilisha madarasa 200 yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi, hii inatokana na madarasa 285. Kwa hivyo madarasa 85 yatakamilishwa mwaka mwengine unaofuatia.

Kuhusu majengo mangapi ni kwamba majengo haya yalikuwa mia tano 500 yamebakia 285 katika 285, mia mbili yanakamilishwa mwaka huu na 85 yatabakia. Ahsante sana.

Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf: Ahsante sana Bismillahi rahmani rahim ahsante sana Mhe. Spika, ningeomba nimuulize suali la ziada lenye vifungu a na b kama ifuatavyo:

a) Kwa kuwa kakiri kuna bilioni mbili za kuweza kuwasaidia wale wananchi walioanza kujenga wenye. Je. katika hizo bilioni mbili wananchi wangu wa Chaani Kandwi wamejenga madarasa wenyewe zaidi ya sita, ningependa kujua hizo bilioni mbili ngapi zitatumika kwenye kuweza kumalizia ile Skuli za Kandwi.

b) Kwa kuwa kuna shule nyingi Jimbo la Chaani zinavuja.

Mhe. Spika: Mheshimiwa,

Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf: Naam

Mhe. Spika: Swali lako wewe ni moja tu.

Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf: Si (a) na (b) au hairuhusiwi Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa niaba yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kwamba katika kutoa huduma hii ya kukamilisha majengo Wizara ya Elimu inafanya utafiti wa kina kuona wapi pana mahitaji zaidi kuliko pengine, kwa maana hiyo basi majengo haya yamegawiwa katika Wilaya mbali mbali za Unguja na Pemba

ikiwemo Wilaya ya Kaskazini ambayo Mhe. Nadir anahusika Kaskazini (A).

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuniona na mimi kuweza kunipa nafasi ya kuuliza suala dogo la nyongeza.

Kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa jitihada zao kubwa wanazozichukua ndani ya Wizara yake wakishirikana na Mhe. Waziri niwapongeze sana, lakini ningependa nimuulize suala dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri kwa kweli tunafahamu kwamba ili skuli ihamiwe au darasa limalizike lihamiwe ni lazima lijengwe litiwe saruji na lipigwe plasta halafu baadae litiwe rangi, lakini katika ziara yetu Mhe. Naibu Waziri tumeona kwamba haya madarasa matatu ambayo tayari yameshahamiwa ni madarasa ambayo yametiwa plasta na kutiwa saruji ambayo haina kiwango na sasa hivi hali haiko vizuri.

Je, kama Wizara inachukua jitihada gani ya kusimamia kazi hizi ambazo zinakuwa zinafanywa na Wizara ili huu ubovu au huu udhorotaji usiendelee na huu uchakavu usizidi kuwemo humu maskulini kwa kukidhi haja ya wanafunzi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa niaba yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ili kuona ubora unafikiwa na huu ni ubora wa aina zote ubora wa kitaaluma na ubora wa miundombinu, sasa hivi ni kwamba ujenzi wote ambao tunausimamia katika Wizara ya Elimu unasimamiwa kwa karibu ili kuona ubora wake unapatikana, kazi yoyote ambayo haitafikia kiwango ambayo tumewapa wakandarasi au

mafundi kazi hiyo hatutoipokea mpaka ifikie kiwango kinachohusika na utaratibu huo tunauanza hivi sasa. Ahsante sana.

Nam. 1

Hatma ya Kampuni ya Ujenzi ya Shpya

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

(a) Je, nini hatma ya Kampuni ya ujenzi ya SHPYA ambayo ilipewa kazi ya kujenga barabara zetu lakini ikashindwa kuendelea na kazi na kufanya barabara hizo zisiendelee kutengezwa.

(b) Je, Serikali ilipata hasara kiasi gani kutokana na Mkandarasi huyo kushindwa kufanyakazi kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Aliuliza:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 1 lenye vipengele kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali na Mfadhili na mradi huo Benki ya Maendeleo ya Nchi za Kiarabu kwa Afrika *(BADEA)* kwa kushirikiana na Mshauri Elekezi wa mradi huo *(NEWTECH CONSULTANT)* waliamua kwa pamoja kuuvunja mkataba huo wa ujenzi wa barabara hapo tarehe 11 Februari, 2016.

Baada ya hapo Mkandarasi huyo iliwasilisha madai yake Mahakamani na hatimae kuomba kuwepo na majadiliano nje ya Mahakama *(Out of Court Settlement)*. Aidha, hadi sasa kesi hiyo bado ipo Mahakamani, na Serikali inasubiri maamuzi ya Mahakama. Kwa upande mwengine, ili kuendelea na kazi hiyo

Serikali na Mfadhili wa Mradi huo *(BADEA)* tulikubaliana kama ifuatavyo:-

(1) Kwa upande wa barabara ya Jendele - Cheju - Kaebona Serikali kuimalizia barabara hiyo kupitia ujenzi utakaofanywa na Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara *(UUB)* kwa kutumia lami, vifusi na vifaa nyengine vilivyoachwa na *SHAPRIYA.*

Napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba barabara hiyo tayari imeshafunguliwa rasmi katika sherehe za Mapinduzi na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohammed Shein siku ya tarehe 10.

(2) Kwa upande wa Barabara ya Koani - Jumbi NI kutafuta Mkandarasi mpya wa kuendelea na Ujenzi. Na katika hatua za kumpata Mkandarasi napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba tayari zabuni zimeshatangazwa na tayari watu wamejitokeza kuchukua zabuni hizo.

(b) Kwa kushindwa kufanya kazi kama ilivyokusudiwa Kampuni ya *SHAPRIYA*, Serikali ilipata hasara zifuatazo:-

i. Kushindwa wananchi kuitumia barabara hiyo kwa wakati kwa harakati za kijamii na kiuchumi kama tulivyokusudiwa.

ii. Gharama za ujenzi kumalizia Barabara ya Koani - Jumbi tunategemea kuongezeka baada ya zabuni kufunguliwa, kutokana na kumpata mkandarasi mpya amba hazitakuwa kama gharama za pale.

iii. Gharama katika zabuni za kumpata mkandarasi mpya kama nilivyosema mwanzo zitaengezeka sio kama zile zilizokuwepo hapo mwanzo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kuhusiana na ujenzi wa barabara hiyo ambayo moja imefunguliwa na Mhe. Rais, kwanza nachukua nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa kuiona kadhia ile ya barabara na ikaweza kuijenga na wananchi wetu wakapata kunufaika.

Lakini kwa kuwa tayari Waziri umeshakiri kwamba zipo gharama ambazo zitaongezeka hapo pindipo ujenzi huo utakapokuwa unaendelea. Sasa mimi ningependa kujua je, kuna kanuni ambazo zitaiwezesha Serikali kuidhibiti ile mali yake ili iweze kuwa fidia kwa hizo gharama ambazo zitakuwa za kuongezeka.

a) Je, huyo mkandarasi huyo kwanza ningependa kujua bado ana mali hapa ambazo zinaweza kuzuilika ili Serikali ikapata hiyo fidia.

b) Kwa kuwa mambo yote yaliyoelezwa kwenye jibu la msingi gharama hizo zinakisiwa kufikia kiasi gani kwa ujenzi huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Kama nilivyosema mwanzo *(BADEA)* tayari wamekubali kuchukua hizo gharama baada ya kumalizika ile barabara ya mwanzo na katika bajeti yetu hii ya safari hii ya Wizara yetu ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirisishaji ya 2017/2018 tumetenga

bilioni 7 kutoka kwa mfadhili yaani huyo *BADEA* na milioni 830 kwa ajili ya gharama ya fidia kwa pale ambapo kutaonekana kuna nyumba zimejengwa kwa mujibu wa huo mkataba wetu.

Kwa hivyo mimi nina imani kubwa sana kwa sababu bado tenda haijafunguliwa lakini nina imani kubwa sana pesa zilizowekwa zitatosheleza kujenga ile barabara. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza lenye kitoto (a) na (b). Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake, lakini kama unavyokumbuka utaratibu wa kuingia mikataba lazima kuna eneo la *Big Security Decoration* ambayo inatoa zuio la *some amount* inabaki mpaka pale ujenzi unapomalizika ndio mnakuwa na declare kuimaliza. Sasa katika utaratibu wa mkataba huu pamoja na kwamba hii kesi ipo Mahakamani lakini hili halihusiani na Mahakama, mlizuia kiasi gani ambazo wakati Serikali inaingia mkataba na muwekezaji huyu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza ifuatavyo:

Kama nilivyosema chanzo halisi cha sisi kwenda Mahakamani mojawapo wa chanzo hichi ni kuhusu hii gharama ambayo tunatakiwa tuizuie, kwa hivyo mimi namuomba kwanza atuachie tuendelee na hii kazi mpaka hapo Mahakama itakapotoa maamuzi mengine. Ahsante sana.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi ningependa muulize Mhe. Waziri Suala dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa katika ujenzi wa barabara hizi katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba Serikali imekuwa inatumia

juhudi nyingi sana, kubwa na fedha nyingi ili kuhakikisha kwamba wananchi wanafaidika katika huduma hii. Lakini kumekuwa na matatizo mengi katika barabara hizi mbali ya matatizo na migogoro juu ya mikataba na wakandarasi lakini utumiaji wa barabara hasa katika michanga na mawe ambayo yanazidi kuharibu muda ambao matumizi kwa barabara hizi. Ukiangalia leo barabara ya kutoka Chuini kwenda Mangapwani, Barabara ya Amani kuja mpaka Dunga mashimo yamenza na muda wake ambao umepangiwa bado haujafika.

a) Ni utaratibu upi unaotumia Wizara hii kuhakikisha kwamba hawa watu wanaoharibu wanakamatwa na kupelekwa katika vyombo vya sheria.

b) Katika jimbo letu la Tunguu kumekuwa sasa kuna kasi ya watu kujenga na kujiendeleza kiuchumi na kujenga majumba yao sehemu tofauti, ni utaratibu gani unaotumia Wizara yako katika kutoa elimu kuhakikisha kwamba wananchi wetu wa jimbo la Tunguu katika maeneo kutoka Fuoni kuja mpaka zake Tunguu, Tunguu mpaka Kaebona kupitia Kibele na Bungi hawa watakuja kuathirika wakati barabara hii itakapokuja kuanza kujengwa kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi Maswali yake ya nyongeza yenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, sote tunajua kwamba ile sheria ya barabara Na. 7 ya mwaka 2003 inaelezea taratibu zote ambazo zinatakiwa zichukuliwe pale ambapo waendesha magari watazidisha uzito au watachukua mchanga mwingi tofauti na inavyotakiwa na namna gani ya kutumika. Lakini sasa kazi hii inafanywa na Jeshi la

Polisi. Mimi nitachukua nafasi hii kuwaomba sana Jeshi la Polisi liendelee kufanya kazi zake kwa uadilifu na kuhakikisha wale wote wanaovunja sheria basi wanachukuliwa hatua kwa kuwapeleka Mahakamani.

Swali lake la pili, sisi huwa siku sote tunatoa elimu kwa wananchi kupitia vyombo vya habari tofauti kuhusu hifadhi za barabara na mita ambazo wao hawatakiwi kuingia katika hifadhi ya barabara, lakini nitamuomba sana Mhe. Mwakilishi Makini Mhe. Simai Mohammed Said na wawakilishi wengine wote tuendelee kuwaelimisha wananchi, vile vile nawaomba Wakuu wa Mikoa, Madiwani na Masheha tuendelee kutoa elimu kwa wananchi wetu kwamba hatari ya kujenga katika hifadhi ya barabara ambayo inaweza kuwakuta pale ambapo sisi tunataka kujenga zile barabara.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe Maswali yamemalizika mtaona kwamba maswali yamekuwa machache kwa sababu maswali yaliyoletwa kwenye mkutano huu yapo pungufu sana. Kwa hivyo tunajaribu kuyagawa sawia kwa siku zote ambazo tutakuwepo hapa kwa hivyo ndio maana mnayahisi yamepungua, kwa sababu kuna watu wameniandikia hapa wanahisi kama *order paper* ina upungufu lakini upungufu hasa ni maswali.

Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Mohamed Said Mohamed nafikiri kuhusu utaratibu naomba kukusikiliza, muongozo.

UTARATIBU

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Spika, nikushukuru sana kwa kuniona, nataka kutumia Kanuni ya 42(2) lakini sitaki nichukue muda wako wa Baraza lako Tukufu kujadili jambo hili. Kusudio langu ni kutoa hili jambo ambalo ninalo na baadaye serikali kama yapo majibu iweze kujibu.

Jambo lenyewe hivi karibuni mwisho wa mwezi huu, Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Uratibu wa Bunge, Sera na Mambo mengine yanayohusiana na hayo, ndugu yetu Jenista Joakim Mhagama na Waziri wa Ndani ndugu yetu Mwigulu Lameck Nchemba kwa nyakati tofauti walitoa taarifa juu ya wafanyakazi wanaofanya kazi nchi za nje ya hasa Uarabuni na wakasema kuwa ni mwisho na wakazifungia baadhi ya Makampuni kuwa zisipeleke wafanyakazi kule. Lakini vile vile wakapiga marufuku kuondoka wafanyakazi.

Sasa amapozungumza Waziri wa Mambo ya ndani ya nchi ni ya Watanzania nzima. Lakini tukiangalia Katiba yetu ya Zanzibar mabadiliko ya 10 katika kifungu cha (3) cha Sheria Nam. 9 mwaka 2010 inasema Zanzibar ni nchi ambayo ina eneo na mipaka yake, ni eneo lote la Visiwa vya Zanzibar na Pemba pamoja na visiwa vidogo vidogo vilivyozungukwa kwa bahari yake. Ambapo kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ikiitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, sasa jambo hili limeleta taharuki sana kwa watu wetu ambao wapo kule nchi za Uarabuni ambapo na mimi nilikuwepo nikawa nimewasikia kwamba wameleta taharuki kubwa sana kwa sababu wao ndio wanafanya kazi kule. Lakini ikawa tunaangalia upi umuhimu mkubwa, Zanzibar inajisemea wenyewe kama inayo Waziri wa Kazi Mhe. Maudlin Cyrus Castico au inajisemea kupitia Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ili wafanyakazi waliokuwepo kule wasiende. Nilikuwa nataka nitoe tu taarifa hii ili serikali kama inalojibu ijibu ndiyo au hapana na wafanyakazi wetu wa Zanzibar wanahusika na jambo lile ama laa.

Mhe. Spika, nikushukuru sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mohamed Said Mohamed, mimi ningesheuri kwamba serikali ilichukue hili halafu baadae

wanaweza wakaja wakatoa maelezo. Lakini kwanza tuwape nafasi ili waweze kukaa kubadilishana mawazo halafu baadae watatoa majibu ambayo yatawanufaisha mpaka wananchi wanatusikiliza.

Baada ya hapo Waheshimiwa Wajumbe hoja yetu inayofuata mpaka sasa hivi ina wachangia wawili tu ambao wameomba. Kwa hivyo nafasi bado ipo kwa hivyo watu wanaweza kuendelea kuomba kabla sijamwita Katibu. Naomba nimwite Mwenyekiti aje achukue nafasi halafu baadaye ndiyo tunaiita hiyo hoja. Mhe. Mwenyekiti karibu.

(Hapa Mhe Mwenyekiti alikalia kiti)

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kusimamia Mwenendo wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji ya Zanzibar Nam. 2 ya Mwaka 1995 na Kutunga Sheria Mpya ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, Waheshmiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mola wetu Muumba wa mbingu na ardhi, kwa kutujaalia kukutana tena hapa katika ukumbi huu tukiwa wazima na afya njema.

Naomba kuchukua fursa hii kulishukuru Baraza la Wawakilishi, pia kukushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii adhimu ya kuwasilisha katika Baraza lako tukufu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kusimamia Mwenendo wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji ya Zanzibar Nam. 2 ya Mwaka 1995 na

Kutunga Sheria mpya ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji.

Waheshimiwa wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi mtakumbuka kwamba katika kikao kilichopita cha Baraza hili kilivyopitisha mswaada wa sheria ya kuanzisha mamlaka ya viwanda vidogo vidogo (SMIDA) ambapo mijadala na michango yenu ilipelekea kutungwa kwa Sheria hiyo ambayo Serikali imeshaizindua

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliamua kufanya mabadiliko ya mfumo wa uendeshaji wa njia kuu za uchumi na biashara kwa kufanya mageuzi ya kiuchumi kwa kuweka misingi na Sera ya Soko huria ambayo yalitokana na mageuzi ya mfumo wa Tanzania kutoka kwenye uchumi hodhi na kwenda uchumi unaondeshwa na nguvu za soko.

Mageuzi hayo yalilenga katika kukuza uchumi, biashara na kuongeza fursa za ukuaji wa shughuli za kiuchumi pamoja na kupanua wigo wa shughuli za kiuchumi kwa kuruhusu sekta binafsi kushiriki katika shughuli za biashara na huduma. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali ilitunga Sheria ya Kusimamia Mwenendo wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji Nam 2 ya mwaka 1995 ambayo ilifuta sheria ya Udhibiti wa bei *Price Control Act* ya mwaka 1985. Sheria Namba 2 ya mwaka 1995 iliweka masharti ya kuundwa Taasisi ya Taifa ya Kusimamia Mwenendo wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji *(National Fair Trading and Consumer Protection Bureau)* pamoja na masharti ya kuunda Baraza la Usuluhishi la masuala ya biashara na watumiaji *(Fair Trading and Consumer Protection Tribunal).*

Pamoja na Sheria hiyo kuweka masharti ya kuunda vyombo viwili vikuu *(Bureau na Tribunal)*, kwa zaidi ya miaka 22 sasa, Serikali haikuunda "*Bureau*" kwa wakati huo. Sababu mojawapo ni kuwa

Sheria hiyo ilijikita zaidi katika kusimamia masuala ya kumlinda mtumiaji; hivyo sehemu ndogo ya sheria ilijikita kwenye masuala ya ushindani; masuala hayo ya ushindani yakasimamiwa na Idara ya Biashara. Kwa upande usikilizaji wa mashauri, Serikali iliunda *"Tribunal"* katika mwaka wa 1996 ingawa haikuleta mafanikio ilivyotegemewa na hatimae kushindwa kufanya kazi na hivi sasa haipo tena. Hali hiyo ya kushindwa kufanya kazi kwa Baraza hilo *(Tribunal)* kulitokana na kutokuwepo kwa Chombo kamili cha kusimamia masuala ya kumlinda mtumiaji *(Bureau)* ambacho ni hatua ya mwanzo ya kupokea mashauri na kuyafanyia maamuzi kwa hatua za awali; na baadae ikiwa uamuzi wake unapingwa na muhusika mmoja au wote, ndipo shauri hilo hupelekwa kwenye" *Tribunal*". Baadhi ya kazi za chombo hicho "*Bureau*" zinaendelea kufanywa na Idara ya Biashara na Uendelezaji Masoko.

Mhe. Mwenyekiti, mfumo wa uendeshaji Biashara Duniani, unaongozwa na taratibu za kimataifa zilizo chini ya Shirika la Biashara la Kimataifa *(WTO)* ambalo hutoa miongozo ya kisera na uendeshaji wa biashara, na kwa upande wa masuala ya ushindani yanasimamiwa na Shirika la Maendeleo ya Biashara Duniani *(UNCTAD)* ambalo huweka miongozo ya masuala ya ushindani chini ya utaratibu maalum *(Competition Model Law)* hivyo kwa wakati huu Idara ya Biashara haitoweza kusimamia ushindani na badala yake itasimamia Sera na Sheria ya Biashara.

Mhe. Mwenyekiti, ushindani halali wa biashara ni moja ya nyenzo muhimu ya kibiashara katika uchumi unaongozwa na nguvu za soko. Dhana ya Ushindani Halali wa Biashara inachukua nafasi pana katika kusimamia biashara Duniani kwa lengo la kuweka misingi iliyo sawa ya ushindani katika uchumi wa soko huria *(Fair Level of Playing Field).* Ushindani unajengwa katika misingi ya bei, ubora wa bidhaa na huduma, usawa katika upatikanaji wa zabuni, kuondosha miungano ya makampuni inayohatarisha ushindani, kuhodhi soko na kulitumia vibaya, na

kuingia mikataba ya kibiashara inayopelekea kuharibu ushindani na soko.

Kwa mujibu wa Shirika la Maendeleo ya Biashara Duniani *(UNCTAD),* misingi ya ushindani halali na kumlinda mtumiaji inazitaka nchi wanachama kusimamia masuala ya ushindani kwa uwazi na ushiriki mpana wa sekta binafsi kwa lengo la kusimamia ustawi mzuri wa watumiaji. Kwa upande mwengine, Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia Mkataba *(treaty)* ibara ya 62 imeanzisha Sheria ya Ushindani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuweka masharti ya kuzingatiwa na nchi wanachama juu ya kusimamia Ushindani Halali wa Biashara.

Mhe. Mwenyekiti, Sheria Nam. 2 ya mwaka 1995 ilikuwa ma mapungufu kwenye mnasaba wa masuala ya Ushindani Halali wa Biashara; ikiwemo kukosekana kwa maeneo ya msingi ya ushindani wa kibiashara kama vile taratibu za biashara zinazokatazwa *(Restrictive Trade Practices),* matumizi mabaya ya nguvu soko *(abuse of market power),* miungano ya kimakampuni *(Merger and Acquisition),* udanganyifu katika zabuni *(bid – rigging,)* masuala ya bidhaa bandia *(Conterfeit),* miungano ya wafanyabiashara kuhodhi soko *(Cartels),* na masuala mengine ya aina hiyo.

Aidha, Sheria haikuainisha taratibu za kupokea mashauri na taratibu za ukataji wa rufaa; aidha haikuzingatia matakwa ya kimataifa ya kusimamia Ushindani *(Competition Model Law)* ambayo yanasimamiwa na Shirika la Maendeleo ya Biashara (UNCTAD) pamoja na masharti ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ambayo masuala ya ushindani yamefafanuliwa kwa upana zaidi. Kwa mantiki hiyo, imeonekana ipo haja ya msingi ya kutunga Sheria nyengine ya Kusimamia Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji.

Mhe. Mwenyekiti, Sheria Mpya ya Ushindani wa Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji inayokusudiwa kutungwa itajumuisha uwekaji wa taratibu za uendeshaji wa biashara kwa usawa, pamoja na hatua za kumlinda mtumiaji wa bidhaa na huduma dhidi ya ukiukwaji wa haki za msingi za kibiashara.

Sheria hiyo inayokusudiwa kutungwa na Baraza la Wawakilishi hii leo itaweka masharti yafuatayo:-

i. Kuanzisha Tume ya Kusimamia Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji hapa Zanzibar;
ii. Kuanzisha Baraza la Usuluhishi wa Ushindani Halali wa Biashara *(Fair Competition Tribunal);*
iii. Kuzuia taratibu za kibiashara zinazokatazwa *(Restrictive Business Practices);* ambazo ni udhibiti wa bidhaa bandia *(Counterfeit)* miungano ya kimakampuni *(Mergers and Acquisitions)* miungano ya wafanyabiashara kuhodhi soko (*Cartels*), kuharibu utaratibu wa zabuni *(Bid Rigging);*
iv. Kuzuia udanganyifu katika soko *(Mis leading and Deceptive Conduct);*
v. Kukataza kufanya biashara zisizo halali, *(Unfair Business Practices);* kama kutoa matangazo ya biashara ya udanganyifu *(bait advertising)* kulazimisha manunuzi bila ya ridhaa *(harrasment and coercion);*
vi. Kusimamia Kumlinda Mtumiaji, *(Consumer Protection);*
vii. Kutambua uwepo wa jumuiya za Kiraia za Watumiaji *(consumer's consultative association)* na taratibu zake.
viii. Kuelezea Masuala ya mashauri na ukataji wa rufaa pamoja na adhabu zake. *(Complaints and Appeal mechanisms, offences and penalties.);* na
ix. Mambo mengine ya jumla ikiwemo uwezo wa Mhe. Waziri kutunga kanuni.

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Kusimamia Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji inayopendekezwa itakuwa ni chombo kinachojitegemea kitakachoongozwa na Mkurugenzi Mkuu na kuwa na Bodi ya Wakurugenzi. Chombo hicho kitasimamia masuala ya msingi ya ushindani na kutoa maamuzi yanayoweza kukatiwa rufaa kwenye Baraza la Usuluhishi *(Tribunal).* Tume hiyo inayopendekezwa itakuwa na kazi zifuatazo:-

i. Kusimamia masuala ya Ushindani Halali wa Biashara baina ya wafanyabiashara na makampuni *(Fair Trading);*
ii. Kuzuia mienendo ya biashara isiofaa kama vile matumizi mabaya ya nguvu za soko, kupandisha bei ili kumuondoa mpinzani, na vitendo vya kuwaengua washindani. *(Hoarding, misuse of market power, predatory price, unfair trade practice, bid rigging, exclusionary conducts);*
iii. Kusimamia kumlinda mtumiaji *(consumer protection),* ambayo hayahusiani na usalama wala ubora wa bidhaa *(safety and Quality).* Maeneo mahsusi ya kumlinda mtumiaji yatakayosimamiwa na Sheria hii ni kueka bei elekezi *(Price Structure),* kutambulisha bei za bidhaa na huduma *(Price Display),* dhamana kwa bidhaa *(Product Guarantee),* bidhaa kulingana na sampuli, kutoa maelezo ya bidhaa *(product description)* na haki ya kupewa risiti.
iv. Kudhibiti bidhaa bandia katika soko *(Anti-Counterfeit)* ambazo hazihusiani na masuala ya viwango na ubora, masuala hayo yanajumuisha kuibiana nembo, uasili wa bidhaa, majina ya uwakilishi wa bidhaa *(trade names),* rangi, na vifungashio.
v. Kufanya utafiti wa masuala ya ushindani na utetezi kwa maslahi ya watumiaji.

    i. Kupokea malalamiko na mashauri kutoka kwa Jumuiya za Kiraia za watumiaji na

ii. Kutoa elimu kwa umma juu ya tararibu, haki na wajibu wa watumiaji katika soko.

Mhe. Mwenyekiti, kama ilivyoelezwa hapo awali kwamba Sheria inayokusudiwa kutungwa itaunda pia Baraza la Ushindani *(Fair Competition Tribunal)* ambalo litakuwa na majukumu ya msingi ya kupokea mashauri na kusulihisha masuala ya ushindani wa kibiashara yanayotatiza. Mashauri hayo yatapokelewa kutokana na rufaa zitakazowasilishwa sio tu kutoka Tume ya Ushindani, bali pia kutoka Mamlaka nyengine za Udhibiti kama vile ZURA, ZMA, ZFDA, ZBS, na nyenginezo kwa kuwa zinasimamia masuala ya ushindani na kumlinda mtumiaji. Baraza hilo litaongozwa na Mwenyekiti ambaye atakuwa na sifa za uhakimu na Wajumbe wenye elimu na uzoefu mkubwa katika fani za biashara, uchumi, uongozi wa fedha, sheria na utawala. Baraza hilo la Usuluhishi litatekeleza majukumu yake ya usuluhishi kwa mashauri ya Ushindani yatakapojitokeza.

Mhe. Mwenyekiti, Sheria inayokusudiwa kutungwa itaweka masharti yatakayoruhusu watumiaji kuanzisha Jumuiya zao kwa mujibu wa taratibu za Sheria za uanzishaji wa Jumuiya za kiraiya zinavyoelekeza. Jumuiya hizo zitaanzishwa kwa madhumuni ya kuwasilisha maslahi ya mtumiaji katika Tume ya Ushindani, kupokea na kusambaza taarifa mbalimbali zinazohusiana na maslahi ya mtumiaji, na kushauriana na Sekta husika, Serikali na makundi mengine ya watumiaji kuhusiana na masuala ya maslahi ya mtumiaji.

Mhe. Mwenyekiti, Faida zitakazopatikana kwa uwepo wa Sheria mpya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji ni kama zifuatazo:-

i. Kusimamia ushindani halali wa biashara za bidhaa na huduma baina ya wafanyabiashara na makampuni;

ii. Kuondosha mienendo ya biashara isiofaa kama vile matumizi mabaya ya nguvu za soko, kupandisha bei ili kumuondoa mpinzani, na vitendo vya kuwaengua washindani;
iii. Kudhibiti bidhaa bandia *(Consumer Protection and Anti Counterfeit);*
iv. Kuweka bei elekezi katika soko; na
i. Kupatikana elimu kwa umma juu ya taratibu, haki na wajibu wa watumiaji katika soko.
ii. Kukuza uchumi na uwekezaji katika sekta ya Biashara.
iii. Kustawisha biashara kwa kuweka usawa baina ya wafanyabiashara wadogo, wakati, wakubwa pamoja na watumiaji.

Mhe. Mwenyekiti, **k**utokuwepo kwa Sheria ya Ushindani na Kumlinda Mtumiaji kutapelekea kuwepo kwa athari zifuatazo:-

i. Kukosekana kwa ushindani halali wa kibiashara;
ii. Kukosekana kwa utaratibu unaotoa maamuzi kwa mashauri ya ushindani; na
iii. Kukosekana kwa utaratibu wa kudhibiti bidhaa bandia katika soko.

Mhe. Mwenyekiti, uzoefu wa nchi nyengine unaonesha kwamba masuala ya ushindani yanasimamiwa na vyombo vinavyojitegemea. Kwa upande wa Tanzania Bara inayo sheria ya ushindani ya 2003 ambayo imeunda Tume ya ushindani, Baraza la ushindani, na Jumuiya ya Watumiaji, Kenya imeunda Mamlaka ya Ushindani *(Competition Authority)* na *Mauritius* masuala ya ushindani yanasimamiwa na Kamisheni ya ushindani *(Competition Commission of Mauritius - CCM).*

Mhe. Mwenyekiti, baadhi ya mifano masuala yanayosimamiwa na sheria ya ushindani ambayo yapo katika soko letu yapo nchini

mwetu ni pamoja na Matumizi mabaya katika nguvu za soko katika biashara ya usafirishaji, Ufichaji wa bidhaa kwa lengo la kupandisha bei, wizi wa Nembo au majina ya kibiashara, Utumiaji mbaya wa mikataba ya wafanyabiashara na Wazalishaji kwa lengo la kuhodhi soko, uwepo wa Bidhaa bandia ambazo zinazotokana na udanganyifu wa nembo, jina, ufungashaji na modeli, na udanganyifu katika matangazo kwa mfano Matangazo ya simu, madawa ya kienyeji na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, Sheria hii katika eneo la Kumlinda Mtumiaji itazingatia uwekaji wa bei elekezi kwa bidhaa zinazodhibitiwa kama zilivyoelezwa kwenye Sheria ya Biashara *(Price Structure),* kutambulisha bei za bidhaa na huduma *(Price Display),* dhamana kwa bidhaa *(Product Guarantee),* udhibiti wa bidhaa bandia na kuwacha maeneo mengine ya kumlinda mtumiaji yanayosimamiwa na mamlaka nyengine kama usalama wa Chakula Dawa na Vipodozi (Bodi ya Chakula - ZFDA), ubora wa bidhaa (Taasisi ya Viwango - ZBS) na uhakiki wa mezani na vipimo (Idara ya Biashara).

Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu ulipata nafasi ya kujadiliwa na Kamati na hoja mbali mbali ziliibuliwa katika vikao hivyo zikiwemo sifa za viongozi wataongoza Tume na masuala mengine muhimu ambayo yaliulizwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kwa kumalizia kukushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, na Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuupitisha Mswada huu katika ngazi zote na hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe.Waziri, sasa namwita Mwenyekiti, wa Kamati ya Fedha, Kilimo, ili aweze kuwasilisha hotuba yake. Mhe. Mwenyekiti, karibu sana.

Mhe. Hamida Abdalla Issa (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Spika kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo naomba kutoa hotuba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kusimamia Mwenendo wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji Nam. 2 ya mwaka 1995 na kutunga sheria mpya ya ushindani halali ya biashara na kumlinda mtumiaji, kuweka masharti bora na zaidi pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kwanza kumshukuru Mwenyezi; Mola Mtukufu mwenye kustahiki kushukuriwa na viumbe vyote kwa kutujaalia uhai na afya njema, tukaweza kukutana katika Baraza hili Tukufu kwa lengo la kuendelea kuwatumikia Wananchi wa Zanzibar kwa kutekeleza majukumu yetu mbali mbali kwa niaba yao ambapo leo tupo hapa kuupitia na kuujadili Mswada huu uliopo mbele yetu. Namuomba Mwenyezi Mungu anijaaliye ufasaha katika uwasilishaji wa Hotuba hii na atupe usikivu na uelewa ili hatimaye tuweze kuuchangia kwa umakini kwa maslahi ya Taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kukushukuru wewe binafsi Mhe. Mwenyekiti kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako ili niwasilishe maoni ya Kamati yangu ya Fedha, Biashara na Kilimo, kuhusiana na “Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kusimamia Mwenendo wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji Nam. 2 ya Mwaka 1995 na Kutunga Sheria Mpya ya Ushindani Halali

wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji, Kuweka Masharti Bora Zaidi Pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo".

Mhe. Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nachukua fursa hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein pamoja na Makamu wake wa Pili Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa ujasiri wao katika jukumu zima la kuiuongoza vyema nchi yetu sambamba na uendelezaji na uimarishaji wa sekta ya biashara na sekta nyengine hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa nichukue fursa hii kuupongeza uongozi wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko hususan Mhe. Waziri Balozi Amina Salum Ali kwa uongozi wake mwanana unaodhihirisha kama yeye ni *"Iron Lady"*. Aidha, nawapongeza wasaidizi wake wakiwemo Katibu Mkuu, Wakurugenzi. Naibu Mkurugenzi pamoja na watalaamu wengine wa Wizara kwa mashirikiano na ufafanuzi waliyoutoa kwa kamati katika kipindi chote cha majadiliano ya Mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Wanasheria wa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi pamoja na Wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa uchambuzi na ufafanuzi wa hoja mbali mbali zilizojitokeza wakati wa kuujadili mswada huu kwenye ngazi ya Kamati.

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa sijatenda haki iwapo sitowashukuru Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa kazi waliyoifanya na kuujadili na kuuchambua mswada ulioletwa mbele yao kwa upeo na ustadi wa hali ya juu. Kwa heshima na taadhima, naomba sasa niwatambue kwa kuwataja majina yao Waheshimiwa Wajumbe wafuatao wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo:-

1.	Mhe. Yussuf Hassan Iddi	Mwenyekiti
2.	Mhe. Hamida Abdalla Issa	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Mohammed Mgaza Jecha	Mjumbe
4.	Mhe. Ali Salum Haji	Mjumbe
5.	Mhe. Hamad Abdalla Rashid	Mjumbe
6.	Mhe. Ussi Yahya Haji	Mjumbe
7.	Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Mjumbe

Mhe. Mwenyekiti, katika uchambuzi wa mswada huu, kamati yangu haikusita kufanya kazi bega kwa bega na makatibu wetu ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitusaidia na kuturahisishia kuuchambua ipasavyo mswada huu, naomba nao niwatambue kwa kuwataja majina yao kama ifuatavyo:

1.	Ndg. Asma Ali Kassim	Katibu
2.	Ndg. Said Khamis Ramadhani	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, fasili ya ndogo ya (6) ya Kanuni ya 83 ya Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2016 inaipa uwezo Kamati yetu kuwaalika Wadau mbali mbali kila inapotokea shughuli ya kujadili miswada ya sheria.

Hivyo, Kamati iliitumia ipasavyo fursa hiyo kwa kuwaalika wadau wafuatao ili kutoa maoni yao juu ya mswada uliopo mbele yetu.

1. Association of NGO'S of Zanzibar (ANGOZA);
2. Jumuiya ya Wafanyabiasharawa Soko la Mwanakwerekwe (JUWASOMA);
3. Mtandao wa Jumuiya ya Magari ya Biashara Zanzibar (MJUAMIZA);
4. Kibweni Youth Organization; na
5. Umoja wa Kiislamu, Uchumi na Maendeleo (UKUEM).

Kamati inawashukuru sana Wadau hao na inathamini mchango, maoni na ushauri waliotupatia kutuwezesha kuwa na muwanda mapana ya kuufahamu na kuuchambua Mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, kupitishwa kwa Mswada huu na Baraza lako kuwa sheria, itafuta uwepo wa sheria ya Kusimamia Mwenendo wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji Zanzibar Nam. 2 ya Mwaka 1995 ambayo itashughulikia zaidi masuala la kumlinda mtumiaji na kuacha kutoa wigo mpana kushughulikia masuala ya ushindani. Hivyo, Sheria hii itaunda Tume ya Ushindani Halali wa Biashara ambayo pamoja na mambo mengine itakuwa na jukumu la kupokea maombi ya malalamiko yanayotoka kwa wafanyabiashara na kuyatolea uamuzi.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu pia unaanzisha Baraza la Ushindani Halali (*Fair Competition Tribunal*) litakaloongozwa na Jaji wa Mahkama Kuu kusikiliza na kuamua rufaa zilizokatwa kutoka Tume au Mamlaka nyengine za Udhibiti kama vile ZURA na ZBS.

Mhe. Mwenyekiti, kuwepo kwa sheria hii itatoa afueni kwa Watumiaji wa bidhaa na huduma kuanzisha Jumuiya za Watumiaji kwa mujibu wa sheria ya uanzishwaji wa Jumuiya za Kiraia zitakazokuwa na haki ya kuwasilisha maslahi ya mtumiaji katika Tume ya Ushindani, kupokea na kusambaza taarifa zinazohusu maslahi ya mtumiaji na kushauriana na Sekta husika, Serikali na Makundi mengine ya watumiaji kuhusiana na maslahi ya mtumiaji.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu umepiga marufuku vitendo visivyokubalika katika biashara ambavyo vinahadaa ndani yake vikiwemo kuuza au kusambaza bidhaa au huduma kwa bei makhsusi huku muuzaji akijua kuwa hana uwezo wa kumpatia mteja au mtumiaji kile anachokihitaji kwa bei waliyokubaliana.

Aidha, Mswada huu pia umekataza kusambaza bidhaa au huduma ambazo zina madhara kwa mtumiaji. Sambamba na hayo, sheria hii itakuwa mkombozi na kimbilio kwa wateja wengi wanaokumbwa na udanganyifu unaofanywa na wafanyabiashara wasiojali haki na maslahi ya mteja au mtumiaji.

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi, Kamati yetu inakubaliana na dhana nzima iliyobebwa na mswada huu pamoja na marekebisho madogo madogo iliyoyapendekeza wakati ilipokaa na Wizara kwa nia ya kuuimarisha mswada.

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi Mswada huu ni miongoni mwa miswada muhimu sana kujadiliwa na kupitishwa kwani inamgusa kila mtu katika mazingira tofauti kwasababu sisi wote ni watumiaji wa bidhaa au huduma zinazotolewa na wafanyabiashara ambao kila mmoja hujali zaidi faida na maslahi yake binafsi na kuacha dhima aliyonayo ya kuhakikisha anachokifanya kisimuathiri mteja au mtumiaji wake.

Aidha, Mswada huu umekuja kuweka wajibu kwa wazalishaji au Wakala wao kuzingatia usahihi wa huduma au bidhaa wanazosambaza, sifa za bidhaa kuuzika pamoja na bidhaa hizo ziwe zinalingana na sampuli. Sambamba na hayo, Mswada huu umeweka masharti yanayohusiana na kumlinda mtumiaji kwa kuzuia usambazaji wa bidhaa inayoonekana ina kasoro, haikidhi viwango vinavyotakiwa na sheria, sio salama kwa matumizi ya binadamu, zimepitwa na wakati pamoja na usambazaji au uuzaji wa bidhaa bandia katika soko.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu ilienda ndani zaidi na kugundua marekebisho kadhaa yaliyogawika katika maeneo tofauti yakiwemo makosa ya kiuandishi, makosa katika uteuzi wa maneno, kufuta baadhi ya vifungu vidogo, kuweka sawa tafsiri ya maneno yaliyotumika katika Mswada wa Kiswahili na Kiingereza

na kuviandika upya baadhi ya vifungu ili kuweka dhana halisi iliyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 23 kifungu kidogo cha (1), kamati imependekeza kiandikwe upya ili kiwiane na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na kusomeka kama ifuatavyo:

“Tume itatunza vitabu vya kumbukumbu, na katika kipindi kisichozidi miezi mitatu baada ya kumalizika mwaka wa fedha itatayarisha taarifa zifuatazo na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali”.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu imekifuta kifungu cha 26 kidogo cha (5) na kukiandika upya ili kutoa fursa kwa wajumbe wa Baraza Halali la Ushindani kuweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kimoja tu cha miezi mitatu kwani watu wenye utaalamu wa kuziba nafasi hizo wapo wengi Zanzibar na sio kukiwacha wazi kifungu hicho kunaweza kutumiwa vibaya na kusababisha mjumbe mmoja kuteuliwa zaidi na zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imependeza kifungu cha 33 kifungu kidogo cha (2) kifutwe kwani kinawiyana kimaana na kifungu cha 26 kifungu kidogo cha (6). Kamati imefikia maamuzi hayo baada ya kuona kwamba vinajirudia na havilazimiki kuwepo vyote kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu haikuacha kufikiria kwa undani adhabu zilizoainishwa katika kifungu cha 59 kifungu kidogo cha (2) kinachotoa adhabu kwa mtu aliyeshindwa kuweka bei ya bidhaa anayouza ambae atalazimika kulipa faini ya shilingi Milioni Moja na haitozidi shilingi Milioni Tano. Kwa kuzingatia hali halisi ya kipato cha wananchi wetu, ni busara Baraza

likaweka faini ya shilingi Laki Tano na isiyozidi shilingi. Milioni Tatu.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu imebaini pia makosa madogo madogo ya kisarufi na kupendekeza yafanyiwe marekebisho ili kuweka uwiano baina ya mswada wa Kiingereza na Kiswahili. Kiujumla, marekebisho yote yaliyofanywa na Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo yanayoonekana kwenye waraka wa mapendekezo ya marekebisho ambao Waheshimiwa Wajumbe tayari mmepatiwa.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa nawashukuru Wajumbe wote kwa utulivu na usikivu wenu. Naliomba Baraza liuchangie, liujadili, litoe mapendekezo na hatimae liupitishe mswada huu ili uweze kuwa Sheria na kumuwezesha Waziri kutekeleza yale yaliyoelezwa ndani yake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati yangu ya Fedha, Biashara na Kilimo naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa uwasilishaji wako sasa Waheshimiwa Wajumbe Mswada uko mbele yetu tunaanza kwa kuujadili na kwa sasa naomba nimuite Mhe. Omar Seif Abeid akiwa ni mchangiaji wa mwanzo katika kujadili mswada huu.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana Wataala* mwingi wa rehma kutujali tukakutana leo hapa katika Baraza hili tukufu linaloshughulika mambo mapana ya maslahi nchi yetu pia nachukua fursa hii kukupongeza wewe kunichagua wa kwanza kuchangia katika mswada huu.

Najua umenipa nafasi ya upendeleo lakini pia nachukua fursa hii kuishukuru Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kuletwa mswada huu baada ya kuona kwamba iko haja ya kuleta mswada huu kutoka na kilio cha wafanya biashara ambao mingoni mwao sio waaminifu na ni imani yangu kwamba mswada huu umeweza kukidhi kilio cha wananchi kwa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nachukua nafasi hii kutaka kuuchangia mswada huu kwa yale yote ambayo nimeyaona na ni imani yangu kwamba tutakwenda vizuri hadi mwisho na kabla ya kuchangia napenda tu kusema mimi mswada huu nauonga mkono kwa asilimia mia kwa sababu nimeuona nimeusoma uko vizuri. Lakini kulikuwa na baadhi ya mambo ambayo ningependa yaboreshwe ili kwa ajili ya kuweka sawa, kwa sababu kuna baadhi ya maneno ambayo iko haya ya kuyaongezea.

Mheshimiwa tukienda katika tasfiri kwenye ukurasa wa 236 kwenye kifungu kidogo cha (c) yametajwa baadhi ya mambo pale yanasema juu inasoma Zanzibar itajumuisha matumizi ya lugha nyengine yoyote isiyokuwa ya kiingereza au ya kiswahili katika matangazo hayo na katika maandiko ya bidhaa hizo, bidhaa maana yake ni bidhaa zote. Sasa kwenye kifungu cha (c) kumezandikwa kuna madini, miti au mazao vilivyopo juu chini au vinavyoshikamana na ardhi au vyenginevyo mimi hapo nilikuwa napendekeza kwamba na bahari nayo iingizwe kwasababu bahari nayo inatoa mazao ya biashara ikisha ndio iendelea lile neno vyenginevyo, iweke iingizwe babari.

Lakini pia tukija kwenye neno kundi tafsiri kuhusiana na Shirika maana yake ni Kampuni au kampuni nyengine yoyote ambayo inamiliki Kampuni au matawi yake na Kampuni nyengine ambazo ni matawi ya kampuni zinazomilikiwa. Ningependekeza kidogo hiyo sentensi au iyo tafsiri ya hayo maneno yakaweka vizuri maana naona maneno yamejirejea rejea. Kwa hiyo isomoke

kampuni ni kampuni yoyote ambayo inamiliki kampuni nyengine na matawi yanayomilikiwa na hiyo kampuni nyengine kufupisha vile kujirejea rejea au vipi wataalamu wa kughza watakavyoona wataipanga lakini isewe inajirejea rejea sana.

Tukienda katika neno ukurusa wa 237 kundoa bidhaa wanasema maana yake ni kurejesha bidhaa kwa muuzaji sasa mimi nilikuwa napandekeza au naona kuondoa siyo kurejesha, kuondoa na kurejesha ni vitu viwili tofauti. Kundoa maana yake ni kuondoa na kurejesha maana yake ni kuhamisha tunavyoifahamu kwenye kiswahili zaidi sasa hivi ni vitu viwili tofauti ukisema kuondoa maana ni kurejesha haiko vizuri.

Lakini pia tukienda 238 nilikuwa kuna kitu ambacho kinanipa wasiwasi chini ZBS maana yake ni Taasisi ya Viwango ya Zanzibar lakini hapa tunaona kwamba kunakuwa na bidhaa ambazo zinazalishwa zenye nembo ya TBS lakini kule wenzetu Bara na wao wanaotumia TBS. Sasa ningeomba kwamba katika sheria hii au sijaimaliza sijui kama kiko kipingele kinachosema kwamba bidhaa yetu itakayothibitishwa na TBS itambuliwe na Tanzania Bara hii sijaiona sijui kama ipo au lakini au vipi sijaiona.

Kwa hiyo ningeomba hili jambo hili kwenye mswada huu liwemo ili kuwapa nguvu wazalishaji wetu na Taasisi yetu ya Viwango ambayo inapima ili nayo iweze kufanya kazi kule Bara, lakini pia hiyo 239 kifungu kidogo cha (3) kidogo ya (2) kuna maneno pia nayo yamejirudia kwa madhumuni ya kifungu hiki bila ya kiathiri maana katika hali yengine neno biashara maana yake ni kuuza au kupata shughuli, mimi naona biashara ni kuuza na kununua sio kuuza au kupata shughuli. Shughuli mbali na biashara mbali kwa hiyo napendekeza hapo pafanyiwe marekebisho ya lugha ya hayo maana ya tafsiri.

Lakini pia tukiendelea tena katika 240 kifungu kidogo ya (i) kuna kufanya utafiti na kutowa taarifa kwa umma unaohusiana na utekelezaji wa masharti ya sheria hii na kusambaza kwa jamii, sasa utafiti ni kweli utakuwa unahusiana lakini tukisha toa ile taarifa zinakuwa kuhusiana au zinazohusiana ni mambo ya lugha watalamu wa lugha mimi naomba muziweke sawa na uwezo wa Tume tukienda 241 tunauona uwezo wa tume wanasema tume itakuwa na uwezo, lakini tukiingia chini kifungu cha (i) tunakuta inasema kuingia sehemu yoyote ya kufanya ukaguzi baada ya kuidhinishwa na tume. Sasa mimi nilitaka nifahamu au tuliweke sawa hili jambo ni tume gani ambayo itakuwa na uwezo na ipi ambayo itapewa amri maana hapa panazungumza uwezo wa tume. Lakini kifungu kidogo cha (e) inasema kuingia sehemu yoyote na kufanya ukaguzi baada ya kuithinishwa na tume.

Tukienda katika kifungu cha ukurasa 243 kifungu cha 13(d) kulikuwa pale anasema ukomo wa mjumbe kifungu cha (d) inasema ikiwa ameshindwa kutekeleza majukumu yake kwa sababu za kimwili au kiakili. Mimi napendekeza pale iingizwe neno “ugonjwa wa kimwili au akili”.

Mhe. Mwenyekiti, tukienda katika kifungu kidogo cha 13, ukurasa wa 243, kifungu kidogo cha (7). Inasomeka kwamba mwenyekiti anaweza kuamua baadhi ya vikao vya tume vifanyike kwa simu, kwa televisheni au kwa njia yoyote ile ya mawasiliano ambapo mwenyekiti ataona inafaa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa napendekeza na naona ni vyema midahalo ndio tuifanye kupitia njia ya televisheni, simu, redio au mawasilino mengine. Mawasiliano ya kuitana tunaweza tukafanya. Mikutano mimi napendekeza ifanywe kwenye vikao vyao vyao maalum isiwe kwenye simu, kama mwenyekiti mimi leo nampigia simu tuzungumze kwenye simu, iwe tayari kinaitwa kikao. Kwa hiyo, mimi napendekeza kwamba vikao vifanyike

kwenye sehemu maalum ya ukumbi ambao umepangwa kufanywa mikutano hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa 247(26), kifungu kidogo cha (2) hapa tunataja sehemu ya tatu Baraza la Ushindani Halali, hapa unatajwa uteuzi wa mwenyekiti. Inasema (a) kwamba, "mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais baada ya kushauriana na Jaji Mkuu".

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina tatizo juu ya hili, lakini mimi nilikuwa napendekeza kwamba ilikuwa Mhe. Rais yeye ana njia nyingi za kupata kujua, masharti ya kuwa awe ni Jaji ya Mahakama Kuu hayana tatizo na naunga mkono kwa sababu ni jambo ambalo lipo kisheria, anatakiwa mtu awe mtaalamu wa sheria. Hivyo, tumuachie mwenyewe Mhe. Rais tusimuwekee mipaka kwamba lazima ushaurine na huyu ndio ufanye hivi, aah! Tumuachie Rais mwenyewe ateuwe mtu ambaye anaona anafaa miongoni mwa hao majaji. Yeye mwenyewe atajua njia gani atampata mtu ambaye anafaa kuwa Mwenyekiti wa hilo Baraza.

Kwa hiyo, hili nalisema kwa sababu gani? Pale inawezekana mtu akaja akaingiza mambo yake yeye mwenyewe ambayo ameyahisi akasema mimi fulani na fulani, pengine hata kwa utashi wake akamuacha mtu mwenye uzoefu, lakini Rais mwenyewe kupitia vyombo vyake anao uwezo wa kumtambua kila mtu. Kwa hiyo, atakapoona kwamba huyu ndio anafaaa kuwa mwenyekiti awe yeye, hapa tumuachie Rais amalize shughuli hii ya kumteua mwenyekiti tusimuwekee kikomo au tusimuwekee mipaka kwamba lazima ushauriane na Jaji Mkuu.

Mhe. Mwenyekiti, nazitumia dakika zangu kumi na tano nisije nikaambiwa nimezidisha, zikizidi utaniambia…

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika tatu.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 30(2)(c) mimi nilikuwa napendekeza liongezwe neno "maadili ya umma" ambazo zipo kati kati baina ya neno "maadili na ambazo" ili isomeke "amevunja masharti ya sheria hii au kanuni za maadili ya umma ambazo Baraza hili linatakiwa kuzifuata".

Mhe. Mwenyekiti, pia tunaendelea katika hicho kifungu cha (e) kujipatia fedha kwa njia isiyo halali. Hiyo inasema kupata fedha au maslahi mengine ambayo yanaweza kuathiri kazi za Baraza. Hiyo kupata fedha mimi ningependekeza isomeke vizuri kujipatia fedha kwa njia isiyo halali.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kuna neno katika ukurasa wa 249 ambayo nimeyaona yamejirejea.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tunazungumza sana kuhusiana na maneno ya Kiswahili, kwamba tunataka yawe maneno ya Kiswahili. Mhe. Mwenyekiti, lakini miswada tunaona kuna baadhi ya maneno yanayotumiwa ya Kiingereza ambayo yanaandikwa Kiswahili lakini uhalisia wake ni Kiingereza. Mimi napendekeza kwenye miswada tuleteeni maneno ya Kiswahili, kama hapa utaona kuna neno limeandikwa "kutoa waranti". Sisi ina maana hatuna neno waranti linalotafsirika kwa Kiswahili. Kwa hiyo, mimi napendekeza litumike neno "hati" badala ya neno "waranti" au tutumie neno lolote la Kiswahili litakalotafsirika badala ya neno "waranti", kwa sababu neno waranti ni neno la Kiingereza. Kwa hiyo, ni vizuri na ingependeza zaidi kutumia maneno yetu ya Kiswahili katika miswada yetu ya Kiswahili.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu hicho hicho cha 33 ukishuka chini shahidi mbele ya Baraza atakuwa na kinga na fursa kama ilivyo katika Mahakama Kuu. Mhe. Mwenyekiti, mimi naona hili Baraza ni kweli kwa sababu kama nilivyofahamu kwamba Baraza

hili litakuwa na mamlaka kwenye masuala ya kibiashara. Lakini lazima kidogo tuliwekee na *excuse* angalau na pahali pa watu kukimbilia kwa sababu…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako umemalizika, maliza neno ulilokusudia.

Mhe. Omar Seif Abeid: Haya ahsante sana mheshimiwa baada ya hayo naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia. Ahsante sana mheshimiwa. (*Makofi*)

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi hii kuweza kutoa michango yangu ihusianayo na Mswada huu wa Sheria ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Mhe. Waziri na watendaji wake kwa kuweza kuuleta mswada huu muhimu kwa wakati tulionao katika mustakabala mzima wa maendeleo ya kibiashara hapa Zanzibar. Vile vile nichukue fursa hii Mhe. Mwenyekiti, kuipongeza sana Kamati ya Fedha na Biashara kwa maoni yao na mapendekezo ambayo wameyatoa katika kuufanya mswada huu kuwa mzuri zaidi.

Pia nichukue fursa hii vile vile kumpongeza Mjumbe aliyenitangulia Mhe. Omar Seif Abeid kwa michango yake mingi kabisa juu ya mswada huu. Mhe. Omar Seif Abeid pongezi sana kwako, naona leo umekaribia kunifilisi.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kusema kwamba mswada huu juu ya mwenendo halali wa biashara na kumlinda mtumiaji. Ni mswada ambao ni mzuri, umepangika na kwa sababu tulikuwa na sheria ile ya 1995 ambayo itafutwa kutokana na kupitishwa kwa mswada huu niseme kwamba yale mapungufu mengi ambayo yalitokana

na sheria ile wenzetu wameyaona. Kwa tafsiri hiyo tunatarajia sana kwamba mswada huu sasa utakuwa ni mwarubaini tosha katika suala la uhalali wa ushindani katika biashara.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ina sheria nzuri sana kuliko mataifa mengi, na mswada huu wenzetu wameeleza kwamba wamechukua uzoefu katika nchi mbali mbali zenye sheria za aina hii. Kenya, Tanzania Bara, Mauritius na kadhalika na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba tunapata uzoefu wa mataifa mbali mbali katika kutunga sheria, sasa tunakuwa na sheria nzuri lakini kupitisha sheria ni suala moja, utekelezaji na usimamizi wa sheria ni suala la pili. Hapa ndipo ambapo sisi tuna matatizo kwa sababu Mhe. Mwenyekiti hata hiyo sheria tunayoizungumzia ambayo tunatarajia tuifute ilikuwa na mambo mengi mazuri lakini utekelezaji wake na usimamizi ndio ilikuwa tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia na mpaka leo tunashuhudia hata zile bidhaa ambazo tunasema zimedhibitiwa au tunazo wapunguzia wafanyabiashara ushuru, basi bidhaa zile haziwanufaishi wananchi wa kawaida. Wananchi wa kawaida wanazipata kwa bei ambayo ni kubwa wakati wafanyabiashara wamepunguziwa ule ushuru, au baadhi ya wafanyabiashara wanazificha halafu wanakuja kuuza kwa bei ya juu. Sasa ile azma ya kumsaidia mwananchi wa kawaida juu ya bidhaa zile ambazo tunazipunguzia ushuru basi pia inakuwa haipo isipokuwa ni kuwaongezea faida na utajiri wafanyabiashara ambao sio waaminifu.

Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia kupanda holela kwa bei, tumeshuhudia mpaka hivi sasa bidhaa bandia katika soko letu la Zanzibar. Lakini tumeshuhudia bidhaa ambazo zimepitiwa na wakati, hili linaendelea sasa ndio pale ambapo nimesema kwamba kuwa na sheria ni kitu kimoja, lakini suala la utekelezaji na

usimamizi wa sheria ni kitu cha pili. Mhe. Mwenyekiti, hapa ndipo ambapo sisi tuna matatizo. Sasa sheria hii ni nzuri na mimi naikubali mia kwa mia tuipitishe, lakini niiombe sana Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko baada ya kuipitisha hii sheria suala la utekelezaji na usimamizi ndio la msingi sana. Kitu kikubwa sana ni muhali tunakuwa na muhali katika kufanya maamuzi na hususan kwa wafanyabiashara wakubwa. Kuna wafanyabiashara wanahodhi na wanaukiritimba wa soko, lakini tunashindwa kutokana na muhali. Sasa bila ya kuondosha hiyo kutakuwa na *document* nzuri za sheria lakini haisaidii mwananchi wa kawaida katika kupata unafuu kwenye bidhaa mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, sheria inatarajiwa itungiwe kanuni, lakini Mhe. Mwenyekiti sheria hii katika kiutendaji imegusa taasisi mbali mbali. Ningependa sana wenzetu kuwa makini pale ambapo watatunga kanuni juu ya sheria hii. Sheria hii inahusisha taasisi mbali mbali ambazo zipo na nyengine zipo ndani ya chombo chenyewe cha Wizara ya Habari,Utalii na Michezo lakini nyengine ziko nje, kama umakini haukufanyika basi kanuni zake zinaweza zikaja zikagongana. Kwa hiyo, ningeomba sana kwa sababu na hapa tuna udhaifu vyombo vyetu katika serikali vina udhaifu wa *coordination* japo kazi zake zinakuwa zinafanana, lakini zina udhaifu wa *communication* japo kazi zake zinafana lakini hata udhaifu wa ushirikiano. Sasa unakuja kuta tunatunga kanuni lakini tunagongana sasa katika utendaji kazi wa kanuni.

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa katika waraka wenyewe kwenye sehemu ya kwanza ningependekeza kwamba maneno ambayo yametolewa ufafanuzi basi yawekwe katika mfumo mzuri wa kialfabeti. Vile vile katika eneo hili la kwanza napendekeza vile vile maneno mawili yaweze kutolewa ufafanuzi. Neno la kwanza ni “amri za utekelezaji” ambalo limezungumziwa ikiwa ni kama adhabu kwa yale makosa mbali mbali. Jengine ni “amri za fidia” nalo limezungumziwa ikiwa ni sehemu ya adhabu ya makosa

mbali mbali. Haya maneno ni vyema yakatolewa ufafanuzi ili yaweze kufahamika vyema.

Mhe. Mwenyekiti, nikija ukurasa wa 234 katika neno “ushindani” neno la tatu kutoka juu imesemwa hapo maana yake ushindani palikuwa pana neno “ni” napendekeza liingie ili isomeke vizuri kwamba ushindani maana yake ni ushindani katika soko na kuendelea.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tukija katika neno la “mshindani” neno la nne ambayo inasomeka maana yake ni mtu ambaye aliye katika, nilikuwa napendekeza hapo isomeke “ni mtu aliye katika ushindani”, ambayo iondoke na ibakie “aliye katika ushindani”.

Mhe. Mwenyekiti, tukija ukurasa wa 237 katika tafsiri ya neno “mtu”. Mtu maana yake imesemwa ni mtu binadamu. Kwa hiyo, mtu binadamu isomeke “ni binadamu”, neno mtu liondoke napendekeza hivyo.

Vile vile tukija katika neno “eneo” limesemwa linajumuisha ardhi, jengo lolote, muundo, gari na kadhalika. Hii neno “muundo” haijakaa sawa hapa. Mimi napendekeza kama tumekusudia muundo kama miundombinu lakini vyenginevyo ufafanuzi unahitajika muundo imekusidia nini.

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa katika ukurasa wa 238 katika neno nishati. Neno nishati kwanza sijaliona katika ile *version* ya Kiingereza nimejaribu kutafuta sana sijui kama imetumia *energy* au nini lakini sikuliona katika *version* ya Kiingereza kwa sababu nilikuwa na utata wa hii tafsiri. Anasema maana yake ni umeme, usambazaji wa maji safi na maji taka ambayo si neno zuri kwa Zanzibar hatupendelei kutumia hilo, petroli na mambo mengine. Ningependa ufafanuzi katika tafsiri ya neno “nishati”. Lakini niambiwe katika *version* ya Kiingereza ilitumia neno gani. Kama

itabaki hivyo hivyo napendekeza neno “maji taka” liondoke tuweke “maji machafu”.

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa katika ukurasa wa 242 kifungu cha 6(h) kinasema kuchukua sampuli za bidhaa kwa ajili ya kufanya uchunguzi, lakini kifungu cha (j) kinasema kuzuia bidhaa bandia na zisizofaa ambazo hazikufikia kiwango na kuziharibu kwa kushirikiana na mamlaka nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, hapa ndipo ambapo nina sisitiza juu ya ushirikiano, ninasisitiza juu ya uwiano kwa sababu kazi hizi zinahusisha vyombo mbali mbali. Vile vile kuwe na mipaka kati ya vyombo hivi ambavyo kwa sababu suala la sampuli na uchunguzi lina taasisi nyengine, lakini hapa limeingizwa katika chombo hiki ambacho tunataka kukiunda. Suala la bidhaa bandia vile vile wenzetu wanalishughulika nalo.

Mhe. Mwenyekiti, tunahitaji hapo uwiano mzuri na ushirikiano ili kusije kukawa na migongano katika utekelezaji wa majukumu.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika ukurasa wa 249 kifungu cha 33 ambacho kimeelezea juu ya uwezo wa Baraza, hili Baraza kwanza wajumbe wake ni kidogo na hapa kwenye kifungu kidogo cha (2) kinasema, "Baraza litakamilika wakati wowote ikiwa mwenyekiti na wajumbe wawili watakuwepo". Maana yake hapo Baraza litakuwa na watu watatu, lakini Baraza hilo kama mwenyekiti hayupo maana yake litabaki sijui na watu wangapi.

Kwa hiyo, mimi napendekeza hili Baraza liongezwe idadi ya wajumbe. Kwa sababu hata watakapofanya maamuzi kifungu cha 3 kinachosema, "Maamuzi yoyote yatahesabika kuwa maamuzi ya Baraza ikiwa yatapitishwa na wajumbe walio wengi". Sasa kama tuna wajumbe watatu maana yake wajumbe wengi watakuwa ni wawili. Kwa hiyo, hii itakuwa ni hatari pale tunapopitisha

maamuzi mazito. Hivyo, napendelea sana hiyo idadi ya wajumbe ingetizamwa vyema ili kuona kwamba Baraza litakapofanya maamuzi mazito basi iwe yana mantiki.

Mhe. Mwenyekiti, nije ukurasa wa 257 katika kifungu cha 52(i) ambapo kuna maneno yanasema, "kudanganya au kupotosha kuhusu uasili wa bidhaa'.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa napendekeza kwamba katikati ya neno "kuhusu" na "uasili" pawe na maneno haya, "pahali pa", iwe inasomeka kwamba, "kuhusu pahali pa uasili wa bidhaa". Kutokana na *concept* ya ile *version* ya Kiingereza ambayo inasema, *"concern the place of origin of goods"*. Hiyo ndio itakuwa inajenga ile tafsiri sahihi ya kifungu au kipengele hicho.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie juu ya mantiki ya kazi za chombo hiki. Chombo hiki kitakuwa kinashughulikia bidhaa, lakini vile vile kinashughulikia huduma. Sasa katika huduma kuna huduma wakati mwengine vyombo hivi viko Zanzibar kwa mfano *ZURA* inashughulikia masuala hayo. Lakini je, kuna huduma za simu, kuna huduma za mitandao ambayo sheria yake haipo Zanzibar, sheria yake ni Sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa ningependa Mhe. Waziri atakapokuja atuwekee vizuri tutakuwa na mahusiano gani au nguvu gani kwa huduma za simu na huduma za mitandao ambazo ziko katika sheria ambayo sisi hatuna uwezo nayo. Sasa sijui tutakuja kusimamia vipi hizi huduma na hivi sasa kama tunavyojua huduma za simu zinalalamikiwa sana. Wakati mwengine unapiga simu dakika nzima unasikiliza miziki tu, huduma hiyo hapa lazima italalamikiwa, lakini chombo hiki kitakuwa na nguvu gani.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niwaombe wajumbe wenzangu waweze kuuchangia vyema mswada huu wa sheria muhimu sana, kwa mustakabala mzima wa

taifa letu kuhusiana na mambo ya biashara, lakini na kumlinda mtumiaji. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe kwa kutumia muda wako vizuri, sasa ninamuita Mhe. Suleiman Sarahan Said akifuatiwa na Mhe. Ali Suleiman Ali ajitayarishe.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na mimi kunipa fursa hii ili kutoa maoni yangu machache ili kuweza kuchangia mswada huu ambao utaleta manufaa kwa nchi yetu na wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nimpongeze sana Dr. Ali Mohammed Sheim katika uongozi wake, katika kufanikisha mambo mengi ambayo anayafanyia marekebisho pale pahali anapoona kwamba pana haja na nia njema kwa Zanzibar na wananchi wake. Lakini pia niwape pongezi hawa waliotayarisha huu mswada kwa nia njema ya kuweza kuboresha maboresho ambayo yanaweza yakasaidia biashara na kwa manufaa ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nizungumzie kwanza suala kubwa la elimu kwa jamii juu ya suala zima hili la biashara. Tuna matatizo mengi ambayo yanaweza yakatufika, tatizo kubwa linakuwa ni elimu. Sasa tatizo la elimu mpaka linapofahamika linachukua muda mkubwa sana na badala yake linakuwa limeshaleta madhara au linakuwa limeleta sitofahamu kutokana na watu kutokuelewa mustakabali mzima wa biashara.

Mimi niende kidogo kwenye eneo la kuzungumzia neno 'kisiwa'. Kisiwa kina mwisho na wananchi wake mara nyingi wanakisiwa kwa mantiki ya udogo wake. Kisiwa kinategemea sana Bara na silazima neno ninalozungumza kwamba ni Tanzania Bara, nazungumzia kisiwa chochote kile kinategemea *land*,

kinategemea nchi ambayo iko karibu yake. Lakini kwa maana halisi mimi nikizungumza naizungumzia Tanzania Bara, kwamba Zanzibar tegemeo lake kubwa ni Tanzania Bara kibiashara. Sisi tukizungumzia biashara za ndani ni kwamba sisi ni watu ambao tunategemea biashara kama ni za kilimo zitoke Bara kwa kuingia Zanzibar. Biashara zetu nyengine sisi ambazo tunahisi kama tungekuwa na viwanda pia tungeweza kuuza Bara.

Sasa hoja ya kwanza kwa upande wa hapa inakuja ni vikwazo vile ambavyo kwa pamoja vinakuwa hatulingani kiuwezo. Zanzibar uwezo wake ni mdogo katika mazingira mengi ya kifedha na mambo mengine kutokana na mapato yake, lakini Bara ni kitu kikubwa. Pia tatizo lake sheria mara nyingi zinakuwa zinagongana kwa wafanyabiashara na waathirika wakubwa kwa sababu sisi tunawategemea wao Bara haikosi kitu kwetu sisi, kwa sababu haitutegemei sana, lakini pale zinapotokea changamoto nyingi za kwamba Zanzibar inakuwa ina matatizo ya kitu basi sisi Zanzibar tunapata tabu kutokana na sheria ambazo zinagongana. Nikichukulia masuala madogo madogo tu, sisi tunazungumzia sana maisha mazuri au mepesi kwa kila mmoja anafanya kitu chake katika familia yake iwe na vitu vya ulaini na faida zipatikane kirahisi kuliko ugumu. Lakini sisi tunaofanya biashara katika upande wa Zanzibar na Bara wananchi wetu wanalalamika siku zote kutokana na kwamba wanafanya biashara siku nyingi lakini faida haipatikani. Kwa sababu kila baada ya kipindi cha miezi mitatu kunatokea *issue* ya kuweza kugongana kwa sheria.

Hii inawafanya wafanyabiashara wetu kuwa hawakui, kila siku mpaka jambo likirekebishwa linakuwa na matatizo. Ningeomba sana Baraza letu hili na mambo mengine haya yaliyotayarishwa kwa ajili ya hii, wakafanya kazi ambazo zinakuwa hazileti mgongano ili kuweka wananchi wetu ambao wanafanya biashara za Bara zikaweza kwenda sawiya kuonekana kama hii nchi ni moja.

Mhe. Mwenyekiti, wakati mwengine inategemea kuna bidhaa ambazo zinatoka Tanzania Bara, zinakwenda Rwanda na Burundi zinakuwa rahisi, zinakuwa na ulaini fulani, lakini kitu kikiingia Zanzibar kinakuwa kigumu wakati ni nchi moja. Hii ni migongano midogo midogo ambayo inahitaji kurekebishwa ili kuweka usawa na umoja wa nchi yetu na wananchi wetu kwa pamoja wakapata faida katika biashara zao.

Kitu chengine ninachokizungumza ni faida na hasara. Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar wafanyabiashara wake wengi sio wataalamu, wafanyabiashara wake wengi ni watu wa kujishughulisha bila ya utaaalamu, hawana *feasibility study*, hawana *survey*, hawana chochote. Mtu akishafanya mipango yake ya kuuza gunia zake za karafuu anafanya biashara zake bila ya kuangalia tatizo lenyewe linaweza likafanya kitu gani.

Sasa tatizo linalokuja ni kwamba matatizo yanayowapata ni hali moja ambayo inachangia sana, ni hali ya kodi pamoja na usafiri. Mheshimiwa mpaka leo kitu chochote ambacho kinakwenda Pemba basi unakinunua mara mbili Dar es Salaam; kitu chochote ambacho kinakwenda Pemba unakinunua mara moja na nusu Zanzibar kama sio mara mbili. Tatizo biashara bila miundombinu ya usafiri inakuwa na tatizo na hizi *custom* zinakuwa nyingi. Biashara hiyo hiyo moja inatoka Dar es Salaam, biashara hiyo unaipitisha Zanzibar, biashara hiyo inakwenda Pemba na mote muna *custom duty* humu. Hii inafanya Zanzibar hasa kwa upande wa Kisiwa cha Pemba biashara zake zikawa ghali sana na zinakuwa na maisha magumu sana mpaka watu huwa wanajiuliza. Ukiitizama pesa ambayo inachumwa karafuu ni *trillion* zinakwenda kule Pemba, lakini pesa zake hazionekani ni ashiria moja kwamba pesa zake zinaishia kwenye usafiri pamoja na *duty* ambazo faida yake inakuwa ni ndogo sana katika maisha yale.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nije katika vitu ambavyo tunazungumzia kwamba ni biashara halali na biashara ambayo tunasema inadhibitiwa. Lakini kiuhalisia wake biashara hii inakuwa inaleta mashaka katika nchi yetu, hatukubali kwamba baadhi ya maradhi yetu tunayoyapata katika kisiwa hiki yanatokana na vyakula vya viwandani.

Mhe. Mwenyekiti, ukichukulia katika miaka ya kizamani maradhi mengi yalikuwa hayapo kwa sababu bidhaa za viwanda zilikuwa ni chache sana. Ukichukulia vipimo na viwango tukichukulia vitu kama soda utaona ni soda lakini lugha za kisasa ni sharubati.

Mhe. Mwenyekiti, neno lile lile mtu kama daktari au mwengine anakwambia yeye mwenyewe *individual* kwamba kitu hiki usinywe masukari haya, usinywe soda hizi, zina hatari, zina maradhi gani. Lakini sisi tumeingia moja kwa moja baada ya kutizama afya za wananchi wetu tunaingia kwenye biashara na mapato zaidi bila kuangalia uhalisia wa chakula, matokeo yake tunapata hasara kubwa katika kutibu wananchi wetu hivi sasa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, haya ni mambo ambapo maradhi yamekuwa mengi sasa hivi, hata mtoto wa miaka 20 au 25 wa kiume ukitangaza tu kwamba hapa pana dawa za asili au nyenginezo zinazoweza kusaidia uzazi basi mtari utaweza kufika Malindi matatizo ya vyakula yanatuumiza sana; lazima tukubaliane na hali halisi ya matatizo yetu ni matatizo ya sukari, kensa na mengine. Hatukubaliani na suala la chakula kwa afya, lakini Mheshimiwa mimi nataka niseme bado changamoto iliyopo vyakula vya viwandani vinatumaliza afya zetu. Ningeomba sana Mhe. Mwenyekiti, bado suala la biashara linaungana na suala la afya, biashara nazo katika ukaguzi wake zikaangaliwa kwa kina kuhusu hali halisi kuliko hali inayoendana.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala ambalo tunazungumzia watu ambao wanaweza wakatusaidia katika biashara zetu, utakuta kwamba mtu anasema katika ukurasa wa 242 nambari 8, "Kuanzishwa Sekretarieti ya Tume ambayo itakayoongozwa na Mkurugenzi Mkuu ambaye atateuliwa na Rais".

Mheshimiwa mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ikiwa ni Mzanzibari angalau ana shahada ya kwanza katika fani ya uongozi wa biashara, uchumi, usimamizi wa biashara, sheria, utawala wa umma na fani inayolingana kutoka Chuo Kikuu kinachotambulika, ana uzoefu wa kazi angalau miaka kumi katika fani zilizoainishwa chini ya kifungu hiki.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi suala la umri wa miaka kumi katika masuala haya hatunayo tena na ni suala ambalo tunapigishana kelele sana kati ya wazee ambao hakuna wazee tena ni wagonjwa pamoja na vijana. Sisi tunasomesha vijana wetu Mhe. Mwenyekiti, wanakwenda kusoma kwa niaba ya kuja kutusaidia, atafanya miaka mingapi ya kwake yeye halafu awe na uzoefu wa miaka kumi, huyo mtu atakuwa na umri gani Mheshimiwa? Siku hizi watu wanaofika miaka 40 tayari ni mgonjwa, sisi tusitizame tena uzoefu tutizame elimu ambayo ameipata ili kuweza kufanikisha masuala ambayo ameyapata. Leo huyu kama kenda kusoma shahada ambazo zina elimu halafu asubiriwe miaka kumi watu wameshapiga hatua zaidi ya miaka kumi, sisi tunabakia kule kule tunamtafuta mtu wa miaka 50 nyuma ndio aje atuongoze leo sisi tunakwenda na wakati. Lazima mtu huyu awe amerudi kwenye chuo ana uwezo wa kuhakikisha kuwa elimu aliyoipata inaweza kutusaidia tusiweke kikwazo, tujue kama ana *profession* gani tunamuweka, watu ambao wanakwenda na wakati ndio tunaotaka *speed* hii ya hapa kazi.

Sasa unaposema kwamba kila siku tutafute mzee aje akae pale kwenye benchi huyu kazi yake kusinzia au tatizo kila siku

utampeleka hospitali, kwa sababu ni mgonjwa ule muda umeshapitwa na wakati. Mhe. Mwenyekiti, mimi hili nilikuwa nilichangie nione kwamba kuna haja hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kuna tatizo hapa nimeliona ambalo ndio hayo mambo niliyozungumza ni suala la mienendo ya kibiashara. Utakuta kuna neno kama "*ZURA*" maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati za Zanzibar. Mheshimiwa nazungumzia suala la biashara kama hawa *ZURA* na watu wengine mpaka leo ukiambiwa Zanzibar unaambiwa hatuna sheria ya madini wakati keshokutwa tunataka kuchimba mafuta na bado sasa hivi tukiulizwa tunasema sheria ya madini hatuna. Hili neno la kwamba hatuna tena hakuna kitu ambacho katika nchi hakuna, ningeshauri sana hawa ni biashara hizi lakini ni biashara zinafanyika za kila aina.

Mhe. Mwenyekiti, nchi hata ikiwa biashara yake haina, Kenya hawana karafuu lakini wanauza karafuu, ningeomba sana Mheshimiwa biashara ikatizamwa kila aina ya biashara tukaiweka katika kifungu ambacho biashara inaweza ikatumika.

Kuna masuala mengi, lakini Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie habari ya ulaji. Sisi mpaka sasa hivi tuna mafuta tunaweka hapo Bara tu, mafuta yetu ambayo labda tuseme kama *reserve* au tunasema kwenda kuchukua *tank*, lakini mafuta yale mpaka leo ukienda kuyachukua nchi ambazo zinachukua kama Congo na nchi nyengine zinatoa US$ 3 kwa tani ambayo inakuwa ndio kodi yao. Sisi tunapewa US$ 10 kwa kuja Zanzibar nchi moja, masuala kama haya mlaji ilikuwa yangempunguzia bei kama sisi tungekuwa na biashara ambayo ina uwiano, lakini mpaka leo unakuta mvutano mdogo mdogo wa biashara ya kuwekeana mikwala. Utakuta tuna sukari hapa ina kiwanda ukitaka kuipeleka Bara ina vikwazo na sasa hivi tuna *speed* ya kujenga viwanda tutakwenda kumuuzia nani. Kwa sababu kila ukitaka kupeleka

biashara unaambiwa biashara hii ina viwango ambavyo labda havitoshelezi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna utoaji maalumu wa mambo haya, lakini nizungumzie suala la sheria ambazo kwa upande mmoja zinahusu Zanzibar na upande mmoja zinahusu Bara. Mhe. Mwenyekiti, biashara za Bara na biashara za Zanzibar thamani yake na uwezo wa biashara yake ni mdogo.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa samahani muda wako umetimia.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Naomba kidogo tu namalizia. Utakuta biashara ambayo kama ni ya Muungano utaambiwa kima hiki cha pesa ndio biashara hii ifanyike kwa Tanzania nzima. Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi ukiniambia suala kama la *bureau de change* utaambiwa kwamba utoe shilingi milioni mia tatu ndio ufunguliwe *bureau de change.* Mheshimiwa Chake Chake shilingi milioni mia tatu nikiifungua nambadilishia pesa nani? Lazima tukubaliane kwamba biashara ya Bara na biashara ya Zanzibar ina *limit* ambapo tungewekeana mipaka tukapunguziana biashara hiyo hiyo moja lakini kutokana na biashara zenyewe.

Lakini la mwisho Mheshimiwa ninalozungumza ni utoaji kodi na mikopo ya benki. Mheshimiwa hili suala katika upande wa biashara, anafanyanyisha lakini anaekuja kuchukuwa kodi hakutizami wewe, haitizami biashara anakutizama wewe umenenepa au umekonda anataka kodi. Hatizami *amount* ambayo umeifanyia biashara inakuwa biashara baada ya kwamba iendelee baada ya siku tatu inaifunga kutokana na kodi zinavyokwenda na ikishawekwa kiwango kwamba kodi hii ifike hivi baada ya ng'ombe kukamuliwa maziwa mwisho anakamuliwa damu. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti na naunga mkono hoja. (*Makofi*).

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kuniwezesha kusimama hapa kuchangia Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kusimamia Mwenendo ya Biashara na Kumlinda Mtumiaji ya Zanzibar namba 2 ya mwaka 1995 na kutunga sheria mpya ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji kuweka masharti bora.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri Katibu Mkuu na watendaji wao wote kwa kuona kwamba hivi sasa kuna haja lazima tubadilike katika maendeleo ya maisha ya binaadamu wetu wafanyabiashara na watumiaji.

Lakini pili niipongeze kamati na Mwenyekiti wake Mhe. Yussuf Hassan Idd na Makamu wake na Wajumbe wake wote kwa kutuletea muhtasari wa marekebisho ya hapa na pale. Mhe. Mwenyekiti, biashara ni kitu muhimu katika nchi yetu na biashara ndio uti wa mgongo wa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Kwa bahati nzuri toka asili na enzi Wazanzibari tunategemea biashara hatuna chengine, tunalima, tunafanya nini lakini kilimo chetu sana cha kukitumia sisi wenyewe kuliko kusafirisha. Kwa hivyo, niseme tu kwamba biashara kutoka nje na baadhi ya biashara zinazohusika na kusafirishwa ndio mafanikio na maendeleo katika kupata pato la nchi yetu hususan kwa maendeleo ya watu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba sheria hii inayopendekezwa ina mambo mengi, lakini pia sheria hii ina faida nyingi. Kwa hivyo, mimi niseme tu kwamba mambo ambayo yanapendekezwa humu ni maendeleo kwa maendeleo ya watu wetu na maendeleo ya wafanyabiashara na watumiaji. Wenzangu wengi waliotangulia kuchangia wamezungumzia neno moja zito sana Mheshimiwa kutunga Sheria niseme ya kwanza, kuifata sheria niseme ya pili.

Mhe. Mwenyekkiti, ukishaitunga umeiweka sheria lakini utekelezaji wake ndio una mgogoro baadae. Kwa hiyo, nimuombe sana Mhe. Waziri kama ilivyoanzishwa Sheria ya Kumlinda Mtumiaji huko mwaka 1995 ni vyema sheria hii ikawekewa mkakati kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanafaidika ili waende mwenendo unaiofaa juu ya maslahi yao na usalama wao. Katika dunia yetu ya sasa hivi tumeshuhudia wenzetu Tanzania Bara hivi karibuni kulikuwa na taarifa kwamba kulikuwa na mchele bandia ikawa hali ya hatari katika maeneo ya biashara. Lakini wataalamu wakafanya kila hali, Wazira ya Biashara, Wizara ya Afya wamechunguza neno hilo hawakulipata kama kuna mchele wa *plastic*, kwa hivyo mchele ukiingia Tanzania Bara kama upo naomba Mwenyezi Mungu auondoe usiwepo maana ni hatari, lakini kwa mfanyabiashara hajali. Kwa hivyo, hili liliondoka na halikutokea tena katika nchi yetu Tanzania nzima na hapa petu kabisa halipo.

Kwa hivyo, niseme tu kwamba biashara za bandia zinaelekezwa zipo nyingi maana ya biashara za vitu bandia sio mchele tu au chakula gani lakini hata vitendea kazi kuna vitu vinaingia ambavyo havina ubora, ubora wake unakuwa haufai kutumika katika maeneo mbali mbali kama vitu vya umeme na vitu vyenginevyo ambayo ni hatari kwa watumiaji na pia kwa usalama kwa watu wetu. Kwa hiyo, nimuombe sana Mhe. Waziri hili liangaliwe tuhakikishe kwamba wananchi wetu wanakuwa katika salama katika utumiaji wa bidhaa mbali mbali kutoka nje na za hapa kwetu ndani.

Mhe. Mwenyekkiti, hivi sasa Zanzibar watu wengi wameamka kibiashara na watu wengi wanasafiri nje sehemu mbali mbali ya Zanzibar wanakwenda Tanzania Bara na kwengineko nje wanaleta bidhaa nyingi. Mimi nawapongeza sana wafanyabishara wote wale wanaoitakia kheri nchi yetu, wanaoitakia kheri nchi yetu ni wale waadilifu analeta bidhaa kwa ajili ya namufaa ya

watu wetu wawe salama, lakini wengine wanaleta bidhaa ambazo hazistahiki na zina hatari katika matumizi ya maisha ya binaadamu wanaotumia. Kwa hivyo, hili naiomba sana serikali kupitia wizara inayohusika tuliangalie na tulifatilie kwa hali na mali.

Mhe. Mwenyekiti, unaweza kwenda sehemu ukakuta *Colgate* mfano mpya gamba lake jipya limefungwa vizuri kumbe limepigwa ule muhuri wa bandia ule *expire date* wanayoita inamalizika 2019 mfano kumbe imeshamalizika 2016 ni hatari na wengi yana watokea. Kwa hivyo, ni mfano na sheria hii ambayo sheria hii itawakamata wengi wanaoleta uhalifu kama huo katika nchi yetu, naomba tusiwaonee huruma wafanyabiashara hao.

Lakini pia udanganyifu katika biashara hasa chakula na mimi nasema tu tunaishukuru Serikali yetu ya Muungano kwa ushirikiano mzuri tunaokwenda nao kwa sababu biashara nyingi za mchele na vitu vyengine vinatoka Tanzania Bara. Lakini bahati nzuri mchele wa Mbeya unapendwa sana hapa Zanzibar tena unapendwa vizuri sana. Kwa hivyo, bahati mbaya unapoingizwa mchele ya Mbeya kuna wafanyabiashara wale wasiokuwa waaminifu wanauchanganya na mchele wa mapembe baadhi ya maeneo Mheshimiwa hayo yapo na naomba sana tuyaangalie ili kunusuru hilo lisiendelee.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, bidhaa nyingi biashara zake zinategemea ziwepo kwa wingi ili wananchi wanaufaike. Lakini inaweza kutokea wakati ukaambiwa sukari imeadimika si duka moja utakwenda maduka zaidi ya mia moja kila unapokwenda bidhaa hakuna kumbe ipo lakini imefichwa ili mtu auze bei za juu. Kwa hivyo, nimeupongeza mswada huu kwa wale wote watakaoficha bidhaa watachukuliwa hatua zinazofaa. Namuonba sana Mhe. Waziri hili tusiwaonee huruma watu hao.

Suala jengine Mheshimiwa niseme tu kwamba wananchi wetu narudia tena wanatutegemea kwa hali na mali kwanza kumlinda juu ya usalama wa maisha yake kwa bidhaa halali iliyokuwa nzuri na ya kustahiki, lakini bidhaa iliyokuwa na patashika hapa na pale ni hatari kwa watumiaji hizo tuhakikishe kwamba tunazifanyika kazi tunaziondoa.

Udanyanyifu ni kitu hatari katika biashara, udanganyifu unaweza kuchanganya kitu kama nilivyotangulia kusema mchele huu ukachanganywa na huu ili upate faida. Kwa hivyo, naomba hili lazima Mhe. Waziri atafute watendaji wazuri ambao watafatilia majuku haya ya kila siku hasa tukizingatia kwamba biashara sio mjini vijijini ndio wanapata usumbufu na hali ngumu inakuwa huko kwa sababu mwananchi hajui. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri hili tuendelee nalo kwa faida ya shughuli zetu.

Lakini ufanisi unaweza kupatikana kwa taaluma. Nimuombe sana Mhe. Waziri tunapoandaa lolote la msingi na mandeleo basi taaluma iwe inatoka mara kwa mara ili kila mfanyabiashara na mtumiaji ajue wajibu wake kwa sababu mtumiaji anategemea kitu kimetoka katika duka kiko salama lakini siku nyengine kina kasoro ya hapa na pale lakini yeye hajui. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri hili tuliangalie kuhakikisha kwamba tunawalinda watumiaji wetu kwa usalama wao na usalama wa maisha kwa ujumla.

Jengine Mheshimiwa niseme tu kwamba kuna mambo ambayo ya mazingira mbali mbali, mimi nimeshuhudia hivi sasa hivi nimekwenda katika katika yangu ambayo taarifa nitaitoa baadae ya Kazi Maendeleo ya Wanawake, Watoto, Vijana na Wazee. Wananchi wengi wameitikia mambo ya kilimo na kilimo sahihi kinachoendelezwa sasa hivi kinahitaji viwanda vidogo vidogo, Mheshimiwa namuomba sana afanye ziara makusudi kama Waziri wa Biashara na watendaji wake watembelee sehemu ya Bwejuu,

Dongwe kuna wakulima wemejitolea wanalima kwa nguvu zao zote, ndimu zinaweza kuadimika sehemu mbali mbali lakini Dongwe yaani Bwejuu ukienda unachukuwa magunia kwa magunia unakuja nayo mjini na hivi sasa naweza kukwambia hakuna bei. Kwa hvyo, wenzetu wale kama watapatiwa viwanda vidogo vidogo watasaidia pato ya nchi yetu. Kwa hiyo, nimuombe sana Mhe. Waziri hili liangaliwe na ili tupate faida kwa ajili ya wananchi wetu na serikali kwa jumla.

Halafu jengine Mheshimiwa tumeshuhudia katika kufatilia mambo mbali mbali kuna bidhaa kama nilivyosema katika sheria ile kuna nembo zile za bandia, yaani nembo ya fulani ikapachikwa kwa fulani ile ni hatari katika biashara naweza mimi kama mfanyabiashara nikenda na biashara yangu nzuri naiuza kutokana na utaalamu mzuri lakini inakubalika kutokana na hadhi yake na nembo yake, akaja mjanja fulani akaitumia nembo ile, nembo ile anatumia kwa maslahi yake ni hatari. Kwanza unamvunjia soko lake yeye mwenyewe biashara ile kwa sababu biashara yako wewe inakuwa si nzuri wala haina uhalali ukafanya udanganifu. Kwa hivyo, niseme tu kwamba sheria imesema tu kwamba wale wadanganyifu watumiaji wa nembo za wenzao watachukuliwa hatua na wachukuliwe hatua kweli kweli ndio nikasema Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri wakae waangalie wakiweka kanuni zao sahihi kwa wale wote wadanyanyifu wa mambo kama haya wachukuliwe hatua zinazofaa.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, nimpe pongezi za peke yake Mhe. Waziri na watendaji wake hivi sasa tukitaka tusitaka biashara zimekuwa kweli na biashara zinaongezeka kila utakapokwenda utakuta mabadiliko yanatokea naweza kuthubutu kusema tu kwamba sasa hivi hali ya biashara si mbaya Zanzibar. Mimi namuomba sana Mhe. Waziri lisimamiwe hili. Lakini kubwa zaidi biashara nyingi zinauzwa katika nchi yetu huwa risiti mimi nasema sana pato la nchi risiti hazitolewi. Kwa hivyo, na

hili katika changamoto hilo liwemo biashara halali ni biashara unayouza ukatoa risiti wewe muuzaji na mnunuzi vile vile atake risiti kwa faida pato la nchi yetu, kwa sababu kitovu cha biashara ni ukweli vyenginevyo hatuna faida katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mengi ya kusema lakini kwa hali halisi niseme tu kwamba nampongeza Mhe. Waziri na watendaji wake pamoja na kamati imefanya vizuri. Lakini na mimi nasema tu kwa upande wangu kwamba tunampongeza Mhe. Waziri kwa dhati kabisa kwa juhudi zake mbali mbali za kudumisha biashara zetu hasa kwenye zao la karafuu na mambo mengineyo anafatilia kwa hali na mali kuhakikisha kwamba uchumi wetu unakuwa.

La mwisho niseme tu kwamba naukubali mswada huu kwa asilimia mia moja na naomba wenzangu wauchangie kwa dhati tumsaidie Mhe. Waziri kwa manufaa ya wananchi wetu watumiaji. (*Makofi*)

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote leo kufika hapa tukiwa wazima wa afya katika kikao chetu hichi leo cha kwanza.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii pia kuwashukuru kwa dhati kabisa wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu kwa kuniwezesha mimi leo kuwa karibu nao natambua kwamba wao wananipenda na mimi naendeleza kuhakikisha kwamba na mimi wao nawapenda na nitaendelea kuwa msemaji wao mzuri hadi 2050.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo niseme tu vitu viwili moja nataka nimpongeze Mhe. Waziri kwa mswada mzuri huu ambao umekuja hapa na ninaposema mzuri siangalii zile *content* za mswada huu peke yake. Kwa jambo lolote ambalo katika visiwa

vyetu ya Unguja na Pemba tukiwa tunakusudia kwa makusudi kulinda mlaji au pia kukuza uchumi wetu na kuendeleza biashara basi ni jambo jema kwa visiwa vyetu. Kwa sababu ukiangalia kwa mazingira ya nchi yetu ya Zanzibar basi moja sababu kuu ni kuangalia uchumi basi itakuwa ni biashara.

Kwa hiyo, nampongeza sana Mhe. Waziri kwa kuleta mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kusimamia Mwenendo wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji ya Zanzibar namba 2 ya mwaka 1995 na kutunga sheria mpya ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlida Mtumiaji na kuweka masharti yake bora.

Mhe. Mwenyekiti, nimejaribu kuangalia sheria ndani na *content* zake lakini yapo maeneo huwa napata ghofu ya *publication* ya kazi na utendaji wao. Nitasema kwa mfano tu *historically* ukienda maeneo ya mjini utakuta watu wanapewa leseni kutoka Baraza la Mji au Manispaa, lakini watu hao pia wanakata leseni kutoka Kamisheni ya Utalii. Sasa unakuta wakati mwengine wale wafanyabiashara wanapata hofu au vikwazo wa double *license* yaani kulipa leseni ya biashara ya kila mwaka kwa taasisi mbili tafauti. Sasa mambo kama haya inakuwa hatuwatendei haki wafanyabiashara wetu pamoja na wananchi wetu na mwisho wa siku inakuwa ile *sprit* ya kunyanyua au ya kukuza biashara inakuwa haipo.

Sasa ukiangalia kwenye sheria hii au mswada huu unakuta nilikuwa najaribu kuangalia malengo au madhumuni kwa lugha nyepesi ya mswada huu. Nasema madhumuni ya mswada huu ni kuimarisha ustawi wa watu wa Zanzibar kwa ujumla na kuboresha na kulinda ushindani imara katika soko la kuzuia mwenendo ulio potofu na udanganyifu katika soko la Zanzibar. Lakini ukiangalia katika Soko la Zanzibar wapo wengine kuna *ZFBA*, kuna *ZURA* halafu nachukulia mfano kwa hawa wawili.

Lakini kwenye sehemu ya kwanza au wa pili unazungumzia mswada huu unakusudia kuanzisha Tume ya Ushindani na Baraza la Ushindani halali. Sasa haya ukiyaangalia yote malengo yake pia ni kwenda kumfikia mtumiaji moja kwa moja au mlaji katika mambo ambayo tunaamini wao wananchi au mlaji atakuwa anafaidika katika mfumo mzima wa biashara.

Sasa nitaanza katika kifungu cha 4 kinazungumzia muundo wa bodi ambapo Mhe. Rashid Makame Shamsi alipazungimzia pia. Ukiangalia katika sehemu hii ya 4 kwenye hii tume ambayo itakuwa inajulikana kama Tume ya Ushindani halali wa biashara itatueleza kazi ya majukumu yake ya mipaka na uwezo wa mamlaka waliyopewa kisheria. Sasa wanasema kutakuwa kuna bodi hasa ukiangalia bodi, waziri atakuwa na uwezo wa kuchagua wajumbe kutoka maeneo tafauti. Nafikiria nikiangalia hapa kwa kizungu inasema kwamba, Wajumbe wengine wanne watakaoteuliwa na waziri. Lakini katika Wajumbe hao wanne walivyozungumza sifa zao nikaambiwa waziri ataangalia taaluma uzoefu katika masuala ya viwanda, biashara, uchumi, sheria, Utawala wa Umma na fani zinazolingana kama hizo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, unaweza ukachagua watu ambao wametoka Tanzania Bara au wamaetoka Jamaica au wametoka Australia akiingia leo Zanzibar akaanza biashara lakini pia akawa wamebobea katika hizo sifa ambazo waziri amezitaja. Lakini mfanyabiashara huyo huyo akawa yeye sie mwanachama au huyo mtu atakaeteuliwa hatoki katika tasisi yoyote ambayo inayojulika kama ni *association,* kutoka kwa wale ambao wamekusanyika kwa wanye akili, mawazo na fikra ya pamoja katika kutetea maslahi yao.

Sasa mimi ningeshauri katika kifungu hichi hapa watafutiwe njia kwamba pia Mhe. Waziri atazingatia jumuiya ambazo ziko tayari zimesajiliwa kihalali katika kuteuwa wajumbe ambao

watakaoingia katika bodi hii, na sema hivi kwa sababu gani, unapukuwa katika jumuiya unapata urahisi wa kupata taarifa kwa wale ambao wamekusanyika ili taarifa zao ziweze kuja kwenye wizara moja kwa moja.

Lakini unapochagua mtu yoyote, kutoka maeneo tofauti huwezi kujua kule chini ambapo wao wahusika wanaosimamia biashara wana waza kitu gani, wanachanga moto ya aina gani na wapi wao wanataka waende kibiashara kwa pamoja ili serikili iweze kuwasikia kilio chao au waweze kuunganisha nguvu zao katika kusimia suala zima la biashara. Sasa mimi naomba suala la jumuiya hapo hicho kifungu kiongezwe na hao watakaoteuliwa nitamuachia Mhe. Waziri yeye mwenyewe aamue akiwa anaona watafaa au hawafai lakini ni vizuri uwakilishi katika jumuiya ikiwa ni *Chamber of Commerce* wapo watu kutoka *ZATO* wote hao ni wa *private sector* pamoja na sekta ya utalii pia, *ZAT* na maeneo mengine wako wengine sijui *ZATOGA* wengine sijui wanasimamia wavuvi uko jumuiya zote zipo hizo.

Lakini pia nataka nichangine katika kifungu namba 58, kwenye kifungu namba 58 kinasema hivi:-

" Mtu anaruhusiwa kusambaza au kuuza bidhaa zile tu ambazo zimethibitishwa kuwa na ubora na zinafa kwa matumizi ya binadamu chini ya sheria ziliopo".

Mhe. Mwenyekiti, naomba tuwe wakweli kuna mjumbe mmoja aliyechangia hapa alisema Zanzibar tuna sheria nyingi sana sisi, lakini Mhe. Mwenyekiti, leo tukisema katika suala zima la kulinda mlaji, kama tutaamua tuende Malindi kule Funguni kwenye soko la samaki tukiangalia ule mnada jinsi unavyoletwa pamoja na hapo Mazizni wale samaki wanavyoletwa na kushushwa chini na juu ya suala zima la uhifadhi basi yule samaki unaweza hata usimnunue.

Chini ukiangalia mazingira anapotupwa samaki kabla ya mnada kuanza hapafai, anapoletwa juu kwanye soko jinsi ya mainzi walivyo na uchafu ulivyokaa hapafai, suala zima la sehemu ya kwenda kujusaidia na umbali pengine wa masoko na mazingira yalivyo hayafai. Ubora wa kucha wa yule mtu mvuvi mwenyewe alivyo ukiangalia ndani hazifai, mavazi yake ukiangalia anayovaa hafai, sehemu utakayotoka anapoishi kama ameshindwa kuuza hao samaki kwenda kuhifadhi hawafai.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nakata nifahamishwe kitu kimoja tunapitisha sheria hii huku tukijua sisi asilimia 70 ya Wazanzibari ni wakulima pengine na wavuvi au wafugaji, katika kundi hilo na leo tunakwenda kupitisha sheria hii inayosema mtu anaruhusiwa kasambaza na kuuza bidhaa, hii sheria itakuwa inagongana na sheria na utaratibu nzima ambao uliopo hapa chini sasa ukiangalia katika vifungu vya mbele nafikiria Mhe. Waziri, inampa ruhusa kanuni kuzitunga sasa katika kanuni zake aangalie sana watu ambao watakao toka wasende wakatumia sheria hii vibaya kwenda kuwanyanyasa wananchi wetu hasa walio masikini.

Mimi Jimboni kwangu nina wavuvi wengi najua na Mhe. Mahmoud Thabit Kombo (Waziri wa Afya) ana soko pia nafirika kwa Mazizini, wengine wana masoko kule Chwaka kwa Mhe. Issa Gavu watu wanakwenda kununua samaki, wengine wanakwenda Mkokotoni lakini ukiangalia mazingira kama utafata kwa mujibu wa sheria basi ni mtihani. Kwa hivyo, mimi naomba Mhe. Waziri, kwa kukupa sheria hii itakayopita hapa basi kanuni zako uzisimimie vizuri sana ili kuhakikisha hawabugudhiwi lakini pia usafi wao na maendeleo yao pia yaendelee kuboreshwa.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, unapozungumzia biashara unazungumzia hawa ma-*vendors* ambao wanatembea mitaani wanauza vitu tofauti na bidhaa zao, kama utakwenda kwa njia ya

ukweli hasa ukiangalia hizi biashara zote zinazofanyika Zanzibar kwa vile viwango ambavyo vinavyostahiki kimataifa basi huwezi kuvikuta. Mhe. Mwenyekiti, ukienda Ulaya utakuta maduka ya nguo, kuna sijui kuna *next*, kuna maduka ambayo unajua *quality* ya mashati yamepitishwa ni sahihi.

Mhe. Balozi anafahamu haya kwa sabubu yeye ni mtaalumu na ameishi sana nje anajua majinzi ya *livers* tunapozungumza, ukizungumza mashati ya *ralph and polo, waresley* lakini leo mavazi utakayokuta Zanzibar nguo zitakazokuja hatuwezi kujua chanzo chake kimetokea wapi, maji yanayotumika katika kuyaosha kabla ya *packaging* lakini pia kuhakikisha yale mashati hayatakuwa na ubaya wowote katika ngozi ya binaadamu. Sasa ukiangalia katika mazingira yoyote ya biashara kutokana na umasikini na masharti ambayo yamo humu ndani basi katika sheria zile za kimataifa sheria hii pia tutakua tanagongana na wale ambao tatakuwa tanapitisha vitu pale bandarani ili kuingia hata ndani.

Naomba tena Mhe. Waziri kanuni atakazozitengeneza wakae vizuri sana na watu *ZBS* pamoja na wengine wote kuhakikisha kwamba wafanyabiashara na walaji hawaumii na kuathirika katika mfumo mzima wa kuleta sheria. Kwa sababu tunafata sheria kwa ajili ya mswada huu kuwasaidia wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, leo ukitaka kuleta gari Zanzibar unaitoa bandarini unapita zako pale Malindi polisi gari itakuwa haina namba lakini lazima uichukue kwenda kuipasisha lakini na askari anakukamata, sasa hebu tuulizane mtu ameruhusiwa kuleta gari, gari iko bandarini anapita nayo Malindi pale nje askari anaweka mkona anamkata, askari akishamkamata anamwambia gari weka ndani. Nadhani gari hiyo hiyo pia inatakiwa iende ikapasishwe, ikapasishwe wapi *ZBS. ZBS* iko wapi iko Amani sasa ile gari abebe juu ya kichwa?

Mhe. Mwenyekiti, maana hiyo gari ingekuwa unabeba juu ya kichwa haigusi kwenye barabara ya Mhe. Balozi Ali Karume, barabara zake ni sahihi lakini ile gari lazima itabidi aidha uiendeshe au uipakie katika lori, na njiani ukikutwa utakuja kupigwa faini sasa hizi mgongano na *duplication of license na spirit ya* kuangalia biashara ziangaliwe tena kwa upya jinsi wananchi hapo, haya tunakusudia kwa sababu tunakuja kukutana nao nje tunaposema haya tunayaona wakati mwengine tunaambiwa tuwambie mawaziri kabla ili tuyazungumze humu ndani kwa sababu hii itasaidia inakwenda inasimamiwa kwa haraka.

Lakini hilo linajulikana la magari *duplication of license* inajulikana na bado sasa hivi leseni nyengine pia zitazidi kuanzishwa. Mimi naamini sasa hivi kwa hali tunayokwenda Zanzibar kwa Serikali yetu sasa hivi *license* sio tu sehemu tena ya kuwa *regulator* ya kumtambua nani anafanya biashara. Hivi sasa leseni imekuwa sehemu moja kwa kila wizara kujitengenezea mapato na wizara chache tu sasa hivi zilizobakia nafikiri katika kikao cha bajeti nitakuja kuzungumza kwa undani, nafikiri hivi sasa ni Ofisi ya Rais, haitoi leseni.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe malizia muda wako umemaliza.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ninachukua dakika tatu kumalizia. Mhe. katika hilo pia unapozunguma katika suala zima ambalo pia Mhe. Suleiman Mwakilishi makini wa Chake Chake amezungumza ni suala zima la kodi. Kwa hivyo, naomba sana katika mfumo huu ambao tunapitisha hili wazingatie sana masuala ya kodi ya nchi na jinsi ya katika kumlinda huyo mlaji na kusudio ambalo wizara au serikali imeleta hapa ili wananchi waweze kufaidika.

Mhe. Mwenyekiti, nilitaka niyaseme hayo ambayo naamini Mhe. Waziri atayachukua na ataweza kuyafanyia kazi pamoja na watendaji wake nichukue nafasi hii kukushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, wewe kwa kunipa nafasi lakini pia niwashukuru Waheshimiwa Wawakilishi kwa kunisikiliza naunga mkono haja mia juu ya mia. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa ninamwita Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame na akifuatiwa na Mhe. Panya Ali Abdalla.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru sana kunipatia fursa hii kuchangia machache katika mswada huu wa Mhe. Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko, Balozi Amina Salim Ali.

Mhe. Mweyekiti, kwanza naomba nianze kwenye mswada wenyewe lakini zaidi nitaigusa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, sheria hii Mhe. Mwenyekiti, ina vifungu 75, Kamati ya Uchumi, Fedha, Biashara na mengineyo, nimefanya masahihisho 57 mswada una vifungu 75 masahihisho 57 na masahihisho mengine a,b,c,d kwa hivyo ukienda masahihisho waliyofanya yanaweza kwenda labda mpaka pengine 200, sasa naiomba sana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Mhe. Mwanasheria Mkuu wale *draft man* wake wa miswada kidogo wafanye kazi ya ziada.

Mhe. Rashid Makame Shamsi kaeleza vizuri sana utakuta baadhi ya vipengele au *phase* zinakwenda *direct translation* ya kingereza kwenye Kiswahili lakini Kiswahili English hakikai sawa. Kwa hivyo naomba niipongeze sana kamati kwa kweli kwa kufanya kazi nzuri sana na mengine *typegrapher errors* tu makosa ya *spelling* na nini kwa hivyo anatakiwa awepo mtu wa mwisho kufanya *proof reading* ili waheshimiwa kwenye kamati kazi irahisike kidogo. Lakini sasa kwenye kamati wanakaa siku mbili kwenda kusahihihisha neno a,e,i,o,u, kidogo inaelekea huko

nyuma haikufanywa kazi ya ziada. Kwa hivyo, ni hilo namuomba sana mwanasheria Mkuu atusaidie hawa *draft man* kidogo walete kitu kilichowiva kwenye kamati, ili kamati ishughulikie kwenye *substance* kwenye yale mambo yenye mswada hasa ilo ni ombi maalumu kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu. (*Makofi).*

Sasa naomba nimpongeze sana Mhe. waziri Mhe. Balozi aliyebobea mambo ya biashara kalelewa huko na anazeekea huko. Mhe Mwenyekiti, katika utangulizi wake katueleza kwa vizuri sana masharti ya ushindani halali wa kulinda mtumiaji kama yalivyoainishwa kwenye sheria za *UNTAD* kwenye sheria za *East Africa community*, kwenye sheria namba 2 ya mwaka 2005. Mhe. kaeleza vizuri sana mambo ya kushindana biashara ni ushindani, na yule anayejiweza ndio anaeshindana nampongeza sana Mhe. Waziri.

Sasa tupozungumza *UNTAD* tunapozungumza Jumuiya ya Afrika Mashariki, unapozungumza Tanzania pamoja na Zanzibar, huzungumzi Tanzania bila ya Zanzibar, haijatimia. Sasa Mhe. ikiwa wafanyaji biashara wetu wananyanyaswa, wanatengwa, ule ushindani haupo sasa tumeridhia vipi hiyo sheria ya *UNTAD*, Tanzania tusharidhia, Jumuiya ya Afrika Mashariki tumeridhia, na ni wanachama kama Tanzania. Sasa kwa nini leo wafanyabiashara wetu wa Mhe. Suleiman na wengine umezungumza vizuri sana hapa haya hayapendezi ushafika wakati tena tuyaondoe, lazima tuende kibiashara tuende kiushindani.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti kuna watu wanahoji kwamba Zanzibar inazalisha sukari *senior officer* huyo kwa upande wa pili wa Muungano anahoji kama Zanzibar kuna kiwanda cha sukari inazalishwa sukari Mtanzania huyo? Hivyo hajui kweli kama kuna sukari Zanzibar? Inasikitisha sana Mhe. hiyo yote inawekewa vikwazo sukari inayozalishwa Zanzibar. (*Makofi)*

Pili TBS, *Tanzania Bureau of Standard* kwenye sheria yake sikukikamata vizuri, kwenye sheria yao wanaitaja Zanzibar kama nchi ya kigeni yaani Zanzibar *as a foreign country* bidhaa zinazotoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara upande wa Jamhuri ya Muungano, zinazotoka Zanzibar zinatoka nchi ya kigeni, leo Tanzania ndani ya Muungano miaka 54 kesho kutwa unai-*regard* kibiashara Zanzibar kama nchi ya kigeni?

Mhe. Mwenyekiti, haya kwa kweli yazunguzwe sote wamoja baba mmoja mama mmoja tushindane kibiashara tudumishe muungano wetu hayo ndio tuyayotaka Mhe. Namuomba sana Mhe. Waziri najua wanafanya kazi kubwa sana kwenye kamati yao ya mawaziri, lakini haya kama kamati labda unayaona magumu,mimi nashauri tuwaombe viongozi wetu wawili, tumuombe Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa heshima zote tu kamanda wetu mkuu akae pamoja na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Muhammed Shein tuusaidie uchumi wa Zanzibar, uchumi wa Zanzibar mdogo, na biashara ndio namba moja.(*Makofi*)

Sasa leo kama kuna vikwazo vingi vya kuibana Zanzibar isiweze kushindana kibiashara Mheshimiwa pagumu hapo, kwa hivyo ningemuomba sana Mhe. Rais wetu na naamini ananisikiliza sasa hivi mimi namjua na nampenda anafuatilia Baraza kweli kweli ningemuomba sana na namuomba pia Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wataizame Zanzibar kibiashara.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwinyihaji kaa. Endelea Mheshimiwa.

Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, nilikua najaribu kukazia tu tuende vizuri katika ile dhana nzima tuliosema ushindani halali wa kumlinda mtumiaji, sisi watumiaji wetu hasa hawa wafanyabishara wadogo wadogo na walaji tuwalinde vizuri ndio uchumi wetu unaotegemea hapa,

Mhe.Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo sasa naomba niingie kwenye mswada wenyewe.

Kifungu cha 74 ukurasa wa 265 Mhe. Mwenyekiti, Mhe. pana kifungu cha kanunu pale, kanuni imezungumza vizuri sana kwamba waziri ataandaa kanuni zifuatazo kwa ajili ya utekelezaji bora wa sheria hii, zile kanuni kazitaja ziko *a, to j,* kanuni kumi kwa ujumla. Kanuni kumi kwa kweli ni nzito na kama nilivyosoma kwamba kanuni hizo zitaundwa kwa ajili ya utekelezaji bora wa sheria wenyewe, sasa namuomba Mhe. Waziri ajitahidi sana sheria hii itakuwa haina maana na haitekelezeki na itakuwa yale yale ambayo mara nyingi tunafanya makosa hatutungi kanuni kwa wakati sasa inakwenda kukaa kwenye *shelf* kazi nzuri sana iliyofanya ya sheria hii, kazi kubwa na nzuri sana lakini kama hizi kanuni zilizotajwa hapa a to j hazikuandaliwa kwa kweli itakuwa kazi si barabara.

Sasa mimi naomba niongezee kanuni moja tu naomba kushauri Mhe. Waziri. Katika ile orodha ambayo imetajwa zile bidhaa ambazo tunasema katika kazi za tume naunganisha na kifungu cha 5(1)c moja ya kazi zake ni kusimamia bei za bidhaa zinazodhibitiwa na kupanga bei elekezi kwa bidhaa hizo. Ni imani yangu katika hizi bidhaa hizi bidhaa nizazozibitiwa kwa sasa zaidi ni vyakula hivi vya sukari, mchele na unga wa ngano, tunashkuru lakini kwa jumla sasa nafkiri orodha inaongezeka kwa mahitaji ya watu yalivyo orodha hii inaongezeka kwa hivyo nataka kumuomba Mhe. Waziri aongeze kwenye kanuni hapa aongeze (i) (j) (k) kuweka taratibu ya kupitia orodha ya bidhaa ambazo bei zake zinadhibitiwa. Orodha hii isiwe ndio imekwisha, nayo iingie kwenye kanuni kwamba baada ya muda fulani ipitie orodha. Kama sasa hivi mabati, kila mtu *Alhamdulillah* siku hizi kila nyumba inaezekwa. Mwenye kipato ndio anajiona kidogo hali yangu kwanza bora nianzie bati, lakini vigae sasa *tiles* za kila aina. Lakini angalau bati lile, basi nalo pia liwekwe *gage* hii bei

hii, ije hii kama vile mchele. Pia saruji mheshimiwa sijui kama katika orodha yake saruji imo, lakini saruji nayo kuna *brand* tofauti. Kuna uwa, Mbeya, sijui Tanga wapi. Nayo hii ninafikiri iko haja bei nayo idhibitiwe iingie kwenye orodha hiyo.

Kwa hivyo, utakuta mfano kama vitu hivyo nilivyovitaja vichache tu, viwe *periodical* yaani muda baada ya muda vinapitiwa kuwekwa bei zile za kudhibitiwa. Mhe. Mwenyekiti, hiyo nilisema naunganisha na kifungu hicho cha 5.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mimi sina mengi sana isipokuwa namuomba sana Mhe. Waziri hii sheria kwa kweli ni nzuri na ni muhimu sana. Kuna kipengele kidogo, kuna mahala amesema kwamba sheria hii itasimamiwa na sheria nyengine au za taasisi nyengine. Kwenye page 239 kifungu cha 3(1) naomba kunukuu inasema:

Kifungu cha 3(1):

"Sheria hii itatumika kwa taasisi au Mashiriki ya Kibiashara, vyombo vya serikali na Serikali za Mitaa zinahusika na ushindani na kumlinda mtumiaji".

Mhe. Mwenyekiti, sasa nilikuwa nataka kumshauri tu Mhe. Waziri, kwamba unajua hivi vyombo vya serikali na Serikali za Mitaa nao wanamlinda huyo mlaji au mtumiaji kwa mujibu wa sheria zao nao. Sasa atafute *modality* nzuri ya kukaa na wenziwe hawa ili kuona lile lengo letu la kumlinda yule mtumiaji linafanikiwa, maana tusije tuka-*create* kama walivyoeleza wenzangu, tusije tuka-*create* migongano kwa taasisi zetu za serikali, kidogo lile lengo lililokusudiwa kama halikufanywa vizuri, kwa hivyo naamini lile lengo hatutolipata.

Kwa hivyo, namuomba sana Mheshimiwa kama kifungu cha 3 alichosema, yeye sasa kwa sheria hii ndio itakayosimamia hayo mashirika ya kibiashara, vyombo vya serikali na Serikali za Mitaa. Lakini ni muhimu sana tutafute *modality* nzuri ambayo naamini akijipanga vizuri anaweza akafanikisha lengo hili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mengi sina niliona nikazie tu sheria hii ambayo ni nzuri, imeandikika vizuri na kwa kweli malengo yake tumeyaona. Zanzibar kama nchi ya biashara, nakumbuka kipindi hiki miezi kama hii ya Disemba, Januari na Februari Mhe. Mwenyekiti, ndio wakati ule majahazi na mashua kubwa yanatoka kwa Wasomali Wasuri wanaleta vitu unavyovitaja. Visu vya ukapi, mikanda wewe taja *you name it* ndio vinakuja wakati huu na wakija wale msimu wa madodo siku kama hizi na wao wanakula dodo mpaka wanavimbiwa.

Mhe. Mwenyekiti, naona vipi Zanzibar tulivyotoka na suala la biashara tokea hapo zamani. Kwa hivyo, leo sio jambo jipya tena Mhe. Waziri kurejesha hii misingi ya biashara kui- *support* nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100 ahsante sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nichukuwe fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia tukakutana mahala hapa tukiwa hatujambo. Lakini pia nichukuwe fursa kukushukuru Mhe. Mwenyekiti na mimi kwa kunipa fursa hii niweze kusema machache katika mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kazi kubwa na juhudi kubwa ambazo wanachukua katika kuhakikisha Zanzibar yetu inafikia katika mafanikio makubwa katika biashara.

Mhe. Mwenyekiti, shukrani hizo nizianze kwa kwenda katika madhumuni na sababu ya mswada huu. Mhe. Mwenyekiti, naomba ninukuu kidogo madhumuni ya mswada huu ni kuimarisha ustawi wa watu wa Zanzibar kwa ujumla, kwa kuboresha na kulinda ushindani imara katika soko na kuzuwia mwenendo uliopotofu na danganyifu katika soko kwa Zanzibar nzima hii.

Mhe. Mwenyekiti, madhumuni yametuonesha ni jinsi gani wenzetu ambavyo wanapambana katika kumtafutia Mzanzibari huyu aweze kuwa na yeye ni mfanyabiashara kama walivyo wafanyabiashara nchi nyengine yoyote. Mhe. Mwenyekiti, hongereni sana Mhe. Waziri na watendaji wako.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, pia nichukuwe fursa hii adhimu kuwapongeza sana wajasiriamali wote wa Zanzibar na vikundi vyote ambavyo vinashiriki katika uzalishaji wa bidhaa mbali mbali, ambazo sisi wenyewe tumekuwa ni mashuhuda katika maonesho ambayo yametoka katika nchi yetu, lakini hata walikokwenda katika nchi mbali mbali, wameweza kuzalisha biashara zilizo nzuri na zilizobora.

Mhe. Mwenyekiti, hatuna budi kuwaunga mkono kwa asilimia 100 wajasiriamali wetu tuweze kuwapa moyo, tuweze kuwasaidia katika kila hali ili waweze kuingia katika ushindani huu. Mhe. Mwenyekiti, tunakwenda katika sheria hii sasa ambayo inataka kuweka vizuri masharti ya wafanyabiashara na kuingia katika ushindani ulio halali. Kwa hivyo, lazima tuwajenge wajasiriamali wetu waweze kupata elimu ya kutosha, ili bidhaa zao ziweze kuingia katika ushindani huu wa masoko.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Suleiman aligusia alisema wafanyabiashara wetu wanafanya tu biashara, lakini hawana taaluma iliyosahihi. Mimi naungana naye mkono kwamba ni

kweli inahitajika elimu ya kutosha ili wafanyabiashara wetu na wao waweze kuingia katika ushindani huu.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilisema niseme machache katika mswada huu. Mhe. Mwenyekiti, nianze katika ufafanuzi. Katika ufafanuzi kwenye leseni maana ya leseni, hapa imeelezwa leseni maana yake ni leseni kibali au mamlaka inayoruhusu mwenye leseni kufanya usambazaji ama kupata bidhaa au huduma au kufanya shughuli yoyote nyengine kibiashara.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina maoni kidogo au mapendekezo yangu nasema neno hili la leseni tuliseme leseni maana yake ni kibali au waraka au mamlaka inayomruhusu mfanyabiashara au mwenye kibali kufanya usambazaji, kupata bidhaa, huduma au kufanya shughuli yoyote nyengine kibiashara. Nilitaka niondoshe hii leseni maana yake ni leseni kurudia tena neno hili hili.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu niende katika ukurasa wa 241, nianze ukurasa huu wa 240 ambapo katika kifungu cha 5(s) kinasema:

Kifungu cha 5(s)

"Kushauriana na, hizi ni kazi za tume katika kazi za tume. Mhe. Mwenyekiti, nasema kushauriana na Jumuiya za watumiaji mamlaka, udhibiti asasi za kibiashara, watu wengine wenye maslahi yanayofungamana na masuala ya ufanyaji wa biashara halali na ushindani".

Mhe. Mwenyekiti, mimi tu nilitaka Mhe. Waziri atakapokuja anipe ufafanuzi, kwa sababu sijajua kama tayari hizi Jumuiya tunazo ambazo zitakuwa ndio zinatulinda sisi watumiaji. Imeelezwa hapa sisi watumiaji ambapo tutakuwa ndio sisi walaji wenyewe hapa. Kwa hivyo, nilitaka kujua kama hizi Jumuiya

kama zipo au mna mpango wa kuzianzisha, kwa sababu hawa itakuwa ndio watu wetu wa kupanda katika majukwaa na kuweza kututetea au kutulinda. Sasa nilitaka kujua kama vipo au havipo au kuna utaratibu wowote wa kuzianzisha.

Mhe. Mwenyekiti, pia niende katika kifungu cha 6 ambacho tume itakuwa na uwezo ufuatao. Mhe. Mwenyekiti, tume uwezo wake, nije katika kifungu cha 6(i) kinasema;

Kifungu cha 6(i)

"Kuweka tozo au malipo yaliyokubaliwa kama yanavyoainishwa chini ya sheria au kanuni za sheria hii".

Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze kwa kuyaona haya. Lakini pia ombi langu hapa penye tozo, sisi tuna wajasiriamali ambao wanainukia sasa kibiashara ambapo na wao ndio tunataka waweze kufanikiwa mpaka waweze kuwa wazalishaji wazuri au waanzishaji wazuri wa viwanda. Sasa hii tozo ndio naomba tuje tuwazingatie sana wafanyabiashara wetu ambao ni wadogo bado nguvu zao ni nyepesi ili waweze kuzingatiwa, wasije wakapewa tozo ambayo itawashinda sasa kuweza kuzalisha kabisa hata hiyo biashara.

Pia kifungu cha 7(1) ambacho kinaonesha muundo wa tume. Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 7(2) kinasema:

Kifungu cha 7(2):
"Wajumbe wengine wa tume watakuwa na sifa ya kuteuliwa na waziri ikiwa wanataaluma na uzoefu katika masuala ya viwanda, biashara, uchumi, sheria, utawala wa umma au fani zinazolingana na hizo".

Mhe. Mwenyekiti, hapa Mhe. Waziri haikuoneshwa hao watu atakaowateuwa watakuwa wana taaluma gani. Kwa hivyo, hakikuwekwa kile kiwango cha taaluma yao, kwa hivyo ndio napata wasiwasi na mpaka mchango wangu unakuja tena katika kifungu hiki kwa kukosekana huu ufafanuzi wa taaluma ya hapa, inakuja katika kifungu cha 12(c) ambapo inaonesha ikiwa atajiuzulu. Hapa inaonesha nafasi ya wajumbe hao itakuwa wazi, sasa nafasi hiyo ndio inasema, ikiwa atajizulu au atakuwa kwa namna yoyote amekosa sifa ya kuwa mjumbe wa tume. Sasa hapa inaonesha hizo sifa zenyewe za hawa wajumbe hazikuainishwa. Sasa mimi ningeomba utakapokuja labda uweze kunisaidia ili na mimi niweze kuwa vizuri katika mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda katika kifungu cha 13(1) ambacho kinaeleza kwamba tume itakutana kawaida vikao hivyo vya tume, vitakutana mara moja kila miezi mitatu na inaweza kukutana wakati wowote ikihitaji kwa ajili ya kutekeleza shughuli zake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba hapa pangeongezwa neno tu dogo katikati ya "inaweza kukutana kidharura, iongezwe hii kidharura" kwa sababu baada ya vikao vya kawaida vilivyobaki vinakuwa ni vikao vya dharura. Sasa vikao vya dharura basi vinaweza kukutana wakati wowote. Kwa hivyo, ningeomba hili neno "kukutana kidharura wakati wowote itakapohitajika.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu niende katika kifungu cha 21(1) ambacho hapa kinaonesha fedha za tume zitajumuisha fedha inayoainishwa na Baraza la Wawakilishi, lakini (b) fedha inayotolewa kwa tume kutoka fedha za *ZURA* au *ZMA* na Mamlaka nyengine za udhibiti kwa kazi zinazofanywa na tume.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka kujua labda ni kazi gani ambazo zitaainisha fedha hizi kazi gani ambazo zitaweza kutolewa na

hawa *ZURA* na *ZMA* au na Taasisi hizo nyengine ambazo mnakusudia hapa zichange fedha ili ziweze kuipa hii tume, ndio nilikuwa nataka kujua hizo kazi ambazo zitafanyika ili zitakazotolewa fedha kutoka *ZURA* na *ZMA*. Nilikuwa naomba huo ufafanuzi Mhe. Waziri utakapokuja ili na mimi niwe miongoni mwa waliofahamu vizuri mswada mswada huu, kwa sababu huu mswada niseme umekuja wakati muafaka na naiomba sana serikali ichukuwe juhudi za makusudi, ili kuweza kuona mswada huu sasa unatekelezeka kwa kuwekewa kanuni ili walengwa husika wa mswada huu waweze kufaidika.

Mhe. Mwenyekiti, katika ufafanuzi tena niende liko neno. Mhe. Mwenyekiti, katika ufafanuzi ushindani maana yake ushindani katika soko ndani ya Zanzibar na unahusu mchakato. Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeomba bado tuendelee na Kiswahili chetu fasaha ambacho kinapatikana hapa kwetu Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, neno mchakato kwa maoni yangu nilikuwa naomba liondoke halafu lije neno "matayarisho ya watu wawili au zaidi ya watu wawili" tuondoshe neno "mchakato ili tuweze kutumia neno letu la Kiswahili ambalo linapatikana katika kamusi zetu zote.

Mhe. Mwenyekiti, niseme nachukua fursa hii kushukuru na kuutakia heri mswada huu au sheria hii, ambayo imeletwa mbele yetu iweze kupita katika njia ya ufanisi uweze kupita mswada huu ili wananchi wetu waweze kufaidika.

Mhe. Mwenyekiti, napata shida mjumbe alipochangia Mhe. Mwinyihaji pale amenigusa, na kweli aliposema *TBS* inatutambua sisi kama Zanzibar kama ni nchi ya kigeni Mhe. Mwenyekiti, hili ni sikitiko. Sisi sio nchi ya kigeni, ina maana kwa msemo huo inawezekana nchi za jirani zikawa zina hadhi kuliko sisi hapa. Sisi sio nchi ya kigeni, ni nchi moja tu hapa, tunajua Zanzibar na Tanzania Bara ni nchi ambazo zimeungana, tuna-*share* vitu vingi.

Kwa hivyo, na wafanyabiashara wengi wamekuwa wakilalamika kuhusu masuala kama haya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi najua viongozi wetu wapo wana busara, hekima na wataliona hili. Tumuombe sana mheshimiwa wetu na alivyotuonesha juhudi yake na uchapakazi wake, bado tunaendelea kumuomba sana Mhe. John Pombe Magufuli aliangalie suala hili kwa sababu halijatupa mwelekeo mzuri katika suala zima la kibiashara. Kwa hivyo, namuomba na ninajua imani yake na utekelezaji wake wa majukumu ya kazi zake anavyofanya, ni mtu ambaye ametupa imani moja kubwa sana. Sisi Zanzibar changamoto zetu nyingi hasa zinagusa katika suala zima la mabadiliko ya katiba, mambo yetu mengi yangerekebishika basi tungeweza kupata katiba iliyo mpya ambayo ingeweza kuondosha mapungufu yale ambayo yanaonekana yanajitokeza.

Mhe. Mwenyekiti, tumuombe tu Mhe. Rais wetu aweze kuliangalia suala zima la kuweza kupata katiba mpya ambayo itaweza kuondosha mapungufu mengi katika nchi zetu hizi.

Ahsante sana mheshimiwa, nichukuwe fursa hii kuunga mkono sana mswada huu na ninawaomba wajumbe wenzangu tuunge mkono mswada huu, kwani ni mswada wenye maslahi ya Wazanzibari wote na wote wengine ambao wanafanyabiashara kwa kupitia kisiwa hiki. Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuwa miongoni mwa wachangiaji wa mswada huu wa Ushindani Halali wa Biashara na kumlinda mtumiaji.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze waziri na watendaji wake wote kwa kuona ipo haja ya kuleta mswada huu

ndani ya Baraza hili kwa maana na malengo yao madhubuti ya kuweza kuwalinda watumiaji.

Mhe. Mwenyekiti, nimeupitia mswada huu kwa kiasi kikubwa sana, lakini kwanza nianze tu kwa ujumla kumuuliza Mhe. Waziri, tunapitisha mswada huu wa sheria, lakini la mwanzo tu aje kutupa faida kwa manafaa ya wenzangu tunatumia sera gani katika utekelezaji wa mswada huu, maana lazima tuanze na sera baadae ndio tuje katika maelekezo haya.

La pili, Mhe. Mwenyekiti, naomba moja kwa moja nielekeze kabla sijaingia katika vifungu vya ndani nimeupitia kwa kiasi kikubwa, lakini katika soko la huduma la usafiri halikuangaliwa na hapa pia pana watumiaji kwa kiasi kikubwa sana. Ule ushindani halali hasa katika eneo hili hauna hata ule uhalisia katika nchi yetu, kwa sababu soko hili hasa la huduma la biashara karibu tumewapa watu fulani wengine wakitaka kuwekeza changamoto wanazokutana nazo ni nyingi sana. Sasa inafika pahala chombo hiki kilikuwa hakipo lakini sasa hivi kipo tunashukuru, lakini ndani yake tunaona haikuangalia soko la huduma ya usafiri. Sasa hawa wenzetu maana huko watumiaji ndio wengi zaidi tutakuja kuwalinda vipi katika soko hili nalo lina changamoto kubwa sana. Huu ni mchango wangu kwa ujumla.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, naomba niende sasa kwenye kifungu Nam. 5(1) na vitoto vyake vyote, lakini nataka kuongeza tu kwa kuunganisha kifungu Nam. 8 cha mswada huu. Nilitaka kuumganisha kwa sababu huku tunazungumza uwepo wa tume, lakini kifungu Nam. 8 (1) kinaeleza kuanzishwa kwa sekretarieti ya tume ambayo itaongozwa na Mkurugenzi Mkuu ambae atateuliwa na Rais.

Sasa Kifungu Nam. 5 nilikuwa nasema nataka kuongeza kuanzisha sekretarieti, maana yake Sekretarieti hii itakwenda

kufanya kazi na tume. Sasa nilipo mimi nani ataanzisha, sasa nikasema tuongeze kifungu kidogo kuwa kisome katika kifungu Nam 5 mwisho kabisa baada ya "t" ile tuongeze "u", maana yake moja ya jukumu la tume hii ni kuteuwa ile sekretarieti, wenzetu wata-*propose* kule kwa Mkurugenzi lakini tume iende ikathibitishe, ndio nilikuwa nataka niongeze hilo.

Mhe. Mwenyekiti, pia niende katika kifungu namba 6, "tume itakuwa na uwezo ufuatao:-

Namba 6 (a) kutoa amri na maelekezo kwa mujibu wa masharti ya sheria hii." Maana unapotoa amri mawili yatatendeka, amri ile kutekelezwa au amri ile haikutekelezwa. Lakini katika utaratibu wa sheria hii hatujaona pahala palipoandikwa kuwa tume ina uwezo wa kushtaki au kushtakiwa, maana amri itapokuwa haikutekelezwa maana yake uhalali wa utekelezaji unapatikana Mahkamani kwa mujibu wa sheria zote tunazozitunga. Sasa ndio napata shida kifungu hicho cha (a), maana kutoa amri jee, ikiwa haikutekelezwa tunaelekea wapi? Sasa kama tuna uwezo wa kushtaki au tunaelekea kwenye Baraza kwenda kushtaki maana yake tuongeze kifungu ambacho kitakuwa kina uwezo wa kusema kuwa tume ina uwezo wa kushtaki na kushtakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende sasa kifungu namba 7. Kifungu hiki kinasema kwamba, "Tume itakuwa ina wajumbe 6 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ametajwa Mwenyekiti, Mwenyekiti sawa mimi sina tatizo nae, lakini katika utaratibu wa kawaida Mwenyekiti atakapokuwa hayupo maana yake hii tume haifanyi kazi? Hakuna upatikanaji wa Makamu Mwenyekiti? Hebu tupate maelezo kwa sababu nilikuwa nasema utaratibu huu tunaweza tukaendaje, kwa sababu wenzetu wana uzoefu, lakini watuambie tunaweza kwenda hivi bila ya kuwa na Makamo Mwenyekiti kwa

sababu zipi, utekelezaji wa majukumu upi. Kwa sababu Mwenyekiti atadharurika, lakini tume inatakiwa iende.

Sasa yale mambo ambayo kama Mwenyekiti hayupo akayafanya Makamo Mwenyekiti ndio kaona labda tuone kunako eneo hili la tume tuongeze uwepo wa Makamu Mwenyekiti na utaratibu hata wajumbe tunaweza tukaweka, wanaweza wakamchagua Makamo Mwenyekiti kwa utaratibu ambao tutauainisha kwenye sheria.

Hapo hapo Wajumbe wengine wanne, wenzangu wamepachangia hapa lakini naomba na mimi nipachangie. Sura halali ya mswada huu ni nzuri, nilizungumza mapema Mhe. Mwenyekiti na naendelea kuwapongeza wenzangu wa Wizara Biashara Viwanda na Masoko kwenye jambo hili. Mswada huu mzuri, malengo yake mazuri, lakini wajumbe namna wanavyopatikana maana yake wote kwa pamoja tumewapeleka kwa Mhe. Waziri na mimi sina tatizo la kuwapeleka kwa Mhe. Waziri, lakini kuna maeneo ambayo wajumbe hawa ingekuwa ni vizuri tukawatoa.

Mfano, katika Sheria hii utekelezaji wake yapo maeneo ya kibiashara na sisi serikali yetu inakuja na kusaini mpaka baadhi ya *document* za makubaliano kunako Jumuiya za Kikanda kama *EAC*. Tunakwenda sisi tunashiriki, Ofisi ya Rais Ikulu inashiriki, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inashiriki, lakini ile *component* yake hasa iko katika Ofisi ya Rais Ikulu. Lakini tunaona tunapoandaa hii, tunaposhiriki mikutano ile ya Jumuiya ya Kikanda, kuna mambo mengi tunasaini makubaliano ambayo yatawasaidia wafanyabiashara wetu kurudi katika ule ushindani tunaouhitaji katika masuala ya *tariff* na vitu vyengine, ili kuja kuondoa ule mgongano kama kuna mtu analalamikia bei ya mwenziwe kama karundika bidhaa anaweza akasema, mimi hizi bidhaa zangu zimetokana katika msamaha wa hichi na hichi kilichotokea katika *EAC*.

Sasa hoja yangu ipo kwa wajumbe hawa tukasema tu na tunaainisha sifa waziri awateuwe kwa mujibu wa sifa zao lakini tusiwatoe kwenye maeneo, mimi ndio nikawa napata shida na ndio maana nikainuka nikasema aa! basi, niishauri wizara au niwashauri wenzangu ambao wameupitia mswada huu basi tukubaliane kunako eneo hili wajumbe wanne wabakie vile vile uteuzi atoe Rais lakini tuwaainishie. Mfano mmoja katika hizo Sekta za Umma, maana yake tumtoe Ikulu kwa maana pale pana mtu anaeshiriki mikutano ya *EAC*, lakini wa pili tunaweza kumtoa *TRA* akatusaidia masuala ya *tariff* na vitu vyengine ambavyo vinaingia katika makubaliano ya Jumuiya zile za Kikanda.

Mhe. Mwenyekiti, lakini na eneo jengine *Chamber of Commence* kwa sababu tayari na hawa ni Umoja wa Wafanyabiashara ambao wao wanakaa na vikao vyao kutetea mambo ambayo yanatokea humu. Sasa nikasema katika eneo hili zima maeneo hayo basi tungeyagusa wale wajumbe tukaona kuna maeneo, basi tuwatoe imetajwa *ZURA* ndani ya Mswada huu, watakuwa wana *component* yao ya kuwalinda nao watumiaji, kwa nini tusiainishe? Moja kwa moja tuone kama mtu kakosa kwenye tume lakini tutapounda Baraza kule mbele tunamuingiza, lakini maeneo yote mawili tuweze kuwashirikisha. Ulikuwa msaada wangu huo lakini sina tatizo, niseme tu napendekeza kiujumla wake.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nende kunako kifungu namba 26(4) ambacho kwa ujumla chini mwisho kule ukikipitia vizuri kinataja ushiriki wa sekta ya umma na sekta binafsi katika ule uteuzi atakaoufanya Mhe. Waziri. Hapo napo sina tatizo napo, lakini hoja yangu inalingana na kule. Sekta ya Umma tunajua hii serikali nzima kwa taasisi zake zote na sekta binafsi tunajua ndio hizo *Chamber of Commence* na vitu vyengine. Lakini nilikuwa naomba sana hapa pabakie hivyo hivyo, lakini Mhe. Waziri nimuombe tu, katika eneo la kutunga sheria naomba maeneo haya

muyaainishe ili yasije yakaleta mgongano zaidi. Hiyo sekta ya umma maana yake tutawatoa wapi na wapi. Kwa sababu serikali kubwa maeneo mengi isijekuwa siku moja watu hawa wote amewatoa Mabaraza ya Miji tu, lakini huku kwengine, lakini sasa ni vizuri tukaweka kanuni, basi tukawaainisha watu kulingana na yale maeneo wanayotoka, tukaainisha yale maeneo ndio nilikuwa nakusudia hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine kifungu Namba 28, "Mrajis wa Baraza". Waziri atateuwa Mwanasheria kuwa Mrajis wa Baraza. Nakubaliana nayo, lakini Mwanasheria huyu atakuwa mpya ndio kaomba kazi katika matengenezo ya *Shortlist*, lakini atateua kwengine katika Wanasheria Waandamizi. Sasa tulikuwa tunataka tuiweke vizuri au labda tukiiwacha hivi waziri atuahidi kwenye sheria ataifafanua vipi, maana yake tupate tu ule mwelekeo mwema wa utekelezaji wa sheria hii mimi sina tatizo na aina hiyo.

Pia katika eneo hilo hilo namuomba Mhe. Waziri tuongeze kifungu kimoja hapo kisomeke kifungu (4) kuwa, Mrajis atakuwa ndiye Katibu wa Baraza. Kwa sababu huku kuna maeneo kuwa Mrajis huyu ndio atakuwa Mtendaji wa Baraza, lakini mara nyingi hawa ndio wanakuwa Makatibu. Sasa bora tukamuainisha kabisa ili kuondoa yale maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba tena niende kunako kifungu namba 30(2), "Muhuri wa Baraza kwenye waraka wowote utathibitishwa kwa kutiwa saini na Mwenyekiti au Katibu". Katika eneo hili tumeona hapo tumempeleka Mwenyekiti au Katibu, katika utaratibu wa kawaida hawa wote kweli ni viongozi, mmoja kateuliwa na Rais, mmoja kateuliwa waziri. Katika utekelezaji wa jambo hili ambalo tunatumia matumizi ya muhuri tungeainisha pamoja tu, tukajua tu hii *liability* iko kwa nani, kuliko kuweka huko au huku, tunaweza tukawapata watu ambao wakashindana kunako eneo hili tu kila mmoja akatengeza wake. Sasa si busara

sana, mimi nasema eneo moja tulihamishe na mapendekezo yangu maana yake tuhamishe Mrajis wa Baraza basi ibakie Mwenyekiti wa hilo Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu wenzangu wameuchangia sana na mimi nisengependa nikasema sana naona bora niwaachie na wenzangu, lakini kwa ujumla niwashukuru sana wenzetu wa wizara wameleta kitu kizuri, ambacho kitawasaidia wananchi wetu. Nashukuru sana Mwenyekiti kwa kunipa nafasi. Ahsante.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniona. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kusimama mchana huu na kuweza kuchangia mswada mzuri na wenye manufaa kwa nchi yetu. Mimi niipongeze tu wizara, waziri mwenyewe pamoja na timu yake kwa kuleta jambo jema katika Baraza letu.

Mhe. Mwenyekiti, katika uchangiaji wangu nitajikita kwenye Kitengo cha *ZBF*. Tumeingia katika ushindani na uletaji wa bidhaa nchini kwetu na hakuna *limit* ya bidhaa za kuingiza, lakini ipo haja na dhamira ya kitengo hiki kuimarishwa. Hivi karibuni tumeshuhudia kuna baadhi ya bidhaa zenye kuingia ambazo hazina ubora na kwa hakika zipo bidhaa za kumlinda mlaji kwa afya yake yaani chakula, lakini pia kuna bidhaa ambazo zimeingia hazina viwango katika upande wa vifaa vya ujenzi.

Kwa hiyo, kitengo hichi naishauri wizara kiimarishwe na kiwe kina utaratibu wa kuchunguza bidhaa zinapoingia Bandarini na hata zikiwemo katika soko. Yote hayo yanakuja kwa kupatiwa vifaa, yaani *laboratory* ya uhakika. Kuna bidhaa zimeingia ambazo zinahatarisha hata maisha ya watu na zimo sokoni na ni hatari hasa, maana yake ziko bidhaa ambazo zinafika hadi kuondoa maisha ya mtu kwa njia ya macho na zimo sokoni.

Kwa hivyo, namshauri Mhe. Waziri kwa namna moja au nyengine ili biashara iende sambamba na utumiaji wa halali na wa uhakika, kitengo cha *ZBF* kiimarishwe kipate zana za uhakika, kusudi tuweze kuchunguza na kuthamini na kutoa ripoti yake. Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba inawezekana bidhaa zikaingia katika soko, lakini kwa vile hazikuchunguzwa bandarini zikaingia katika soko na watu wakatumia, sijui utaratibu gani wanaoutumia wa kufanya *Stop order* ya bidhaa zile zisiendelee kutumiwa kwa maslahi ya mwananchi na kumlinda mtumiaji.

Mimi niseme tu kama siku sita nyuma kuna ajali imetokezea ya bidhaa ambayo haina ubora, kabla alivyoinunua bidhaa ile haina ubora na akanambia bidhaa hii haina ubora, matokeo yake siku aliyotumia ilitokea ajali, ajali ambayo wameshuhudia tukaenda hospitali na tukaripoti kwamba hii bidhaa haina ubora lakini iko sokoni. Kwa hivyo, Mheshimiwa pamoja na timu yake kuna bidhaa za ujenzi zimeingia hazina ubora.

Mhe. Mwenyekiti, kesi ya pili, inawezekana bidhaa ikiwa imetengenezwa lakini si kwa nchi hii pengine Comoro na ikawa *standard* yake sio ya hapa, bidhaa ile kwa makusudi ya ku-*monopoly market and profit* ikaingia hapa na ilipoingia hapa ikawa *supply* na ikatumika na ikawa haina uwezo au haina kiwango cha kutumika, kwa hivyo, ukirejea nyuma unakuta *lab***.** Kwa hivyo mimi ningeshauri Mhe. Waziri na timu yake *lab* ni muhimu isiwe ya magari tu aa, hata bidhaa za chakula pamoja na bidhaa za ujenzi. Kwa hivyo, mchango wangu mimi unakuja kwamba wizara hii kwa namna moja au nyengine iweze kuweka *lab* ya uhakika kusudi tuingie katika ushindani wa kisasa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache mswada ni mzuri na una manufaa kwa nchi yetu kutulinda sisi, nchi yetu na umekuja wakati muwafaka. Mimi binafsi nauunga mkono asilimia mia moja, tena wizara inafanya juhudi kubwa, inakwenda na wakati

na kwa upande wa pili naipongeza sana kwa jinsi ilivyoshughulikia uvunaji wa karafuu katika msimu unaomalizika. Ripoti yao ni nzuri na inafurahisha na ukiangali kama karafuu zimevunwa vizuri na zimeuzwa na serikali haina deni hata senti moja kwa wauzaji, hongereni sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache naunga mkono asilimia mia moja mswada huu. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru na hapo ndio mwisho wa mjadala wetu, sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko aweze kuja kujibu hoja za wajumbe.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe, naomba kuchuku nafasi hii kwanza kabisa kuwashukuru na kukushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kutupa nafasi tena ya kuja kujibu hoja za Waheshimiwa Wajumbe, ambazo wametaka ufafanuzi, wengine wamechangia kuongeza uzuri wa huu mswada na wengine wametaka marekebisho wametoa mapendekeza.
Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba mswada huu umetuchukua muda mrefu wizara yetu kuushughulikia, naweza kusema kama takribani zaidi ya miaka mitatu tumetumia wataalam mbali mbali kutusaidia kutupa mawazo na kuweza kuwa ni mswada ambao kwa kweli utawezesha utekelezaji wa nia yetu ya kuifanya Zanzibar kuwa kituo cha biashara utakuwa unakamilika.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, kama walivyosema Wajumbe wengi mambo mengi yamezingatiwa katika mswada huu na ndiyo maana michango ya waheshimiwa ilikuwa na ufafanuzi mdogo mdogo na mapendekezo ambayo kwa kweli yanaongeza ubora wa huu mswada.

Kwanza kabisa niseme wachangiaji waliochangia ukijumlisha na kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo, wote kwa jumla ni wachangiaji kumi, akiwemo Mhe. Shehe Hamad Matar amechangia kwa maandishi.

Mhe. Mwenyekiti, naanza kwanza kuchukua nafasi hii kuwashukuru, Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo lakini na wajumbe wote wa kamati hii ambao tumekaa nao kwa kina kabisa kwenye semina na siku ya kamati tukapitia vifungu kimoja baada ya kimoja.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu hii kwa kweli wamefanya kazi nzuri kwa sababu waliona kwamba kufanya peke yao haoitoshelezi wakawaongeza pia wataalam maalum wakiwemo watu wa Asasi Angoza, NGO', Wafanyabiashara wa soko la Mwanakwerekwe ambao hao ndio wanaojua masuala ya biashara, watu wa mitandao mbali mbali, vijana na watu wa Uchumi. Kwa kweli hii inaonesha wazi kwamba kamati yetu inakwenda na wakati kwa sababu inaangalia inapata maoni sahihi ya wataalam.

Kwa hiyo, nakubali naomba niseme kwamba yote ambayo kamati wameyapendekeza hapa ni mapendekezo ambayo yamependekezwa na marekebisho yaliyofanywa yote sisi wizara tumeyakubali, na yote yamo katika waraka ambao wameleta wa mapendezo.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba tu niseme kwamba sisi wizara tuna wingi wa shukurani kwa kamati yetu hii, tunaendelea nayo vizuri na ningeomba wazidi kusimamia wizara zetu kwa sababu haya ndiyo mambo yanayotakiwa yafanywe kwa ajili ya mustakabali mwema wa Taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba niendelee kujibu hoja za Waheshimiwa Wajumbe mmoja baada ya mmoja, lakini niwataje tu waliochangia kwanza ni Mhe. Omar Seif Abeid, Mhe. Rashid Makame Shamsi, Mhe. Suleiman Sarahan, Mhe. Ali Suleiman Ali, Mhe. Simai Mohammed Said, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe.Miraji Khamis Mussa, Mhe. Ahmed Yahya na Mhe. Shehe Hamad Matar Mwenyekiti wetu ameleta kwa maandishi.

Mhe. Mwenyekiti, kama tulivyosema katika madhumuni, wajibu mkubwa wa sheria hii ni kuangalia kwamba wazalishaji na wenye kutoa huduma, Ma-*argent* wao na wote ambao wamo katika sekta hii ya biashara lazima watekeleze wajibu waliokuwa nao, wanazalisha kwa uhakika na wanafikisha bidhaa kwa kuzingatia usahihi katika usambazaji, kutoa huduma na kadhalika na masharti yote yanayotakiwa yafanywe yanafatwa bila kumdhuru mtumiaji lakini pia kwa manufaa ya taifa letu na wao wenyewe binafsi.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hayo ndiyo maudhui makubwa kama yalivyokuwemo katika mswada wetu ya maana ya mswada huu, huko nyuma tulipokuwa na soko huria ilikuwa kama vile soko holela lakini serikali yoyote haiwezi kuachia soko likawa holela ambalo mwisho wake linawaumiza wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wa Mhe. wa Omar Seif Abeid mengi ambayo ameyazungumza yamo katika mapendekezo ya kamati yetu, kwa mfano pendekezo la bahari tafsiri ya kuongeza bahari katika makundi na vile vile tafsiri ya kuondoa na kurejesha tafsiri aliyotoa yeye, labda niseme tafsiri ya kuondoa maana yake kuna bidhaa ndani ya soko kuziondoa na kuzirejesha ni sawasawa kwa hiyo unaziondoa unazirudisha kunakohusika yaani unaziondoa katika soko na kuwa biashara zile hazimo.

Jengine Mhe. Mwenyekit,i alisema kuhusu utambuzi wa bidhaa ambazo zinafanywa na ZBS kwamba uwe *automatic* unatambuliwa na TBS, Mhe. Mwenyekiti, haya yanafatwa na sheria yetu iliyomo sheria iliyopo ya ZBS vile vile na sheria ya TBS. Tayari makubaliano hayo wanayo kwa hiyo kilichobakia hapa ni utekelezaji, haiwi *automatic* lakini kuna makubaliano ambayo wamekubaliana.

Mhe. Mwenyekiti, mengine aliyozungumza Mhe. Omar Seif, ni kuhusu uwezo wa tume kuingia popote na nifafanue kusema kwamba mtaalamu ambae anafanya katika tume anaruhusa ya kuingia mahali popote kufanya uchunguzi, lakini ruhusa hiyo lazima itolewe na tume, huo ndio utaratibu ambao umepangwa na kwa mujibu wa sheria zote lazima mtu anaefanya uchunguzi lazima apewe ruhusa na chombo kinachohusika.

Lakini jingine kuhusu ukomo wa mjumbe akishindwa kufanya majukumu yake ni kweli ukomo wa mjumbe ama anakuwa mgonjwa ama anashindwa na maadili ya chombo yanambana na kuwa akikosea maadili anabidi nae vile vile akome ule ukomo wake wa uwakilishi nao unakuwa unaathirika.

Vile vile mikutano ya Tume ifanywe kwa Televisheni, sasa hivi kuna utaratibu wa *tele conference* Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo siyo tu kwamba tuwabane mkutano wa tume uweko makao makuu lakini hata kwa *tele conference* inaruhusiwa kwa sababu *tele conference* ni miongoni mwa chombo cha kufanyia mikutano tunakwenda katika usasa.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ambalo limezungumzwa na wajumbe wengi sitopenda kulirudia tena kwa sababu ya muda suala la mwenyekiti, uteuzi wa mwenyekiti kwamba, Mhe.Rais ashauriane na jaji, tusisahau kwamba huyu mwenyekiti ni jaji wa mahakama kuu, kwa hivyo huwezi kumpora jaji wa mahakama kuu bila ya

kushauriana na mwenyewe mkuu wa chombo hiki ambae ni Jaji Mkuu, kawaida hivyo ndivyo anavyofanya Mhe. Rais kwa kazi maalum zenye utaratibu maalum.

Jengine Mhe. aliongeza maadili ya umma hayo kama nilivyosema marekebisho hayo tayari yameshapendekezwa humu, yote aliyosema suala la *warrant* tumelikubali ni kwamba baada ya kusema *warrant* na kusema kutoa taarifa ya wito.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika mchango wa Mhe. Rashid Makame Shamsi amesisitiza zaidi kuhusu kusimamia lakini pia suala la kuweka kanuni ambalo wajumbe wengine wamezungumza na vile vile utaratibu wa kuwa watu waondoe muhali, na wajumbe wengine wamezungumza, kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti mimi na kubaliana nae moja kwa moja, mia juu ya mia kama sheria kama hazisimamiwi haziwi sheria baadae zinabakia sheria kwenye mabuku. Lakini pia kanuni ni muhimu sana kwa hiyo naomba nitoe taarifa kwamba tayari tumeshaanza *process* za kufanya kanuni na nimeshatoa agizo kwamba kabla ya kumaliza kanuni zetu kupitisha kwa Mwanasheria Mkuu tunatakiwa tukae vyombo vinavyohusika vikiwemo ZBS, TBS na vingine vyote ambavyo vanahusika na sheria hii ili tuwe na kanuni ambayo hatuingiliani au kupingana katika utekelezaji wa sheria hii.

Lakini vile vile katika masuala ya amri za utekelezaji na masuala ya adhabu, fidia zitatolewa yote hayo Mhe. Mwenyekiti, tutashughulika baada ya sheria hii kupitishwa na wakati tunatayarisha kanuni zetu.

Mengine Mhe. Mwenyekiti, katika tafsiri ya ushindani na mshindani kama nilivyosema tafsiri zote hizi zimewekwa sawa wakati wa kamati zetu na zimo katika mapendekezo ya marekebisho ya sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rashid Makame Shamsi alizungumzia pia kuhusu mipaka baina ya maidara kama nilivyosema kama tutakaa tuangalie mipaka ni kweli, kwanini tukashindwa kufundisha nyuma kwa sababu sheria ile ya nyuma ilichukuwa mambo mengi ya sheria ambayo iliyokuwepo, kwa hiyo tutakaa na kuweza kuona mipaka ya kila chombo mipaka yake ni ipi.

Jengine alilozungumzia Mhe. Rashid ni kuhusu kuongeza Wajumbe wa Baraza niseme tu kwa kweli tunafungwa na taratibu na sheria zetu zilizoko nchini hatuwezi tena kuongeza wajumbe wakawa zaidi ya wajumbe watano yaani Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wake hawa wanne hilo hatuwezi kulifanya.

Mhe. Mwenyekiti, jengine alizungumzia katika suala zima kudanganya katika pahala pa uasili wa eneo hili nakubaliana nae kwamba tuongeze hii uasili wa eneo katika mapendekezo haya katika mswada huu. Jengine alilozungumzia Mhe. Rashid, naomba nimuhakikishie tu kwamba kuna vyombo ambavyo havimo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, vikiwemo vyombo vilivyopo chini ya usimamizi wa Serikali ya Muungano wa Tanzania ambayo ni kwa mfano *TCRA* ambacho kinahudumia masuala ya huduma za simu na mawasiliano, naomba nimuhakikishie tu yeye Mhe. Rashid lakini na wajumbe wote wa Baraza kwamba Tume yetu hii kwa kupitia mswada huu watakuwa na mawasiliano na kuona makubaliano maalum na vyombo ambavyo viko Muungano lakini pia Tume hii ya Biashara *Fear Trading* nayo itatakiwa kuwa na mikataba maalum vile vile na chombo kama hiki kilichopo serikali ya Muungano kule Tanzania Bara.

Mhe. Mwenyekiti, nijibu suala la Mhe. Suleiman Sarahan alisema kuna haja ya kutoa elimu, na mimi nakubaliana nae mia juu ya mia kwa kweli mambo haya ni magumu hata mtaona kwamba huu mswada wenyewe umetuchukua muda kutoa semina

kuwafahamisha wajumbe si jambo jepesi kwa sababu ni la kitaalamu lakini pia ni mambo ambayo wanatakiwa Wafanyabiashara wawe na uzoefu nayo na wengi hawana uzoefu nayo mambo hayo yaliyozungumzwa. Yanajulikana na yanaonekana lakini uzoefu nayo hayana, kwa hiyo tutajaribu kutoa elimu hii kwa ajili ya kuwasidia wafanyabiashara waielewe hii taarifa, waelewe mswada wetu huu ili mambo yote yaende vizuri.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, ambalo limezungumzwa na Wajumbe wengi ni kuhusu mahusiano yetu sisi na Tanzania Bara, na ningeomba niwajibu wote wale akiwemo Mhe. Mwinyihaji, Mhe. Panya na wengine kuhusu matatizo yaliyoko katika biashara ya Zanzibar na biashara ya Tanzania Bara. Ni kweli Mhe. Mwenyekiti, hisia hizo zipo na malalamiko hayo yapo na kwa upande wetu kama serikali tunajaribu kulifanyia kazi suala hili, tumeshapeleka katika kamati, utaratibu ulioko ni kamati ya Muungano inayosimamia na mwenyewe Makamu wa Rais wa Tanzania ndie anaesimamia kamati hii, tumeshazungumza masuala haya, tumetakiwa tukae na wenzetu wa Serikali ya Muungano Wizara ya Biashara na Viwanda, wataalamu wameshakutana lakini bado watakutana tena, sisi tunasema kwamba biashara ndiyo maisha ya wananchi wa Zanzibar, kwa sababu Zanzibar ni nchi ya biashara.

Kwa hivyo kwa biashara ya Zanzibar na kwa udogo wa Znzibar lakini bado kuna haja vile vile wafanyabiashara wa Zanzibar na wao wapewe nafasi ya kushindana na wenzao wa Serikali ya upande wa bara bila ya kuwekewa vikwazo, bila ya kuwekewa masharti ambayo ni ya kiurasimu bila ya kuwekewa utaratibu ambao unawarudisha nyuma, kila jambo liko wazi na tumelizungumza lakini ni imani yangu kwamba Serikali ya Muungano siyo serikali ndiyo ambayo inaweka vikwazo kwa wafanyabiashara wetu. Inawezakana sana kuna watendaji ambao

hawaelewi utaratibu, hawaelewi historia ya muungano wetu, hawaelewi umuhimu kwamba Zanzibar kuna wananchi wanaofikia milioni moja na nusu ambao nao maisha yao wanategemea biashara, wanataka na wao vilevile wapewe nafasi ya kuweza kuingia soko la Bara.

Naomba niwahakikishieni ndugu waheshimiwa kwamba suala hili litamalizwa kipindi hiki kwa sababu mbio tunazidi kuzungumza na wenzetu na wao naamini wasikivu wataona haja ya kuwa na uhuru na kuwa urahisi wa wenzao wa upande mwingine wa muungano waweze kufanya biashara kama wanavyofanya biashara wenzetu wa bara kuleta katika soko la zanzibar.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, kuhusu vipimo na viwango, tutoe elimu ni kweli tutazidi kuongeza kutoa elimu, tunatoa elimu hiyo lakini tutazidi kuongeza katika masuala ambayo yanahusu sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu uteuzi wa tume na viongozi wa tume, Mhe. Mjumbe, alizungumzia suala la umri. Lakini naomba nimuhakikishie tu kwamba kuna sehemu mbili hapa kwa upande wa watendaji wataalamu. Mtaalamu ni mtaalamu anatakiwa hata kama akiwa kijana madamu ni mtaalamu apewe nafasi afanye kazi, lakini katika uongozi wa mashirika kama haya kwa mujibu wa sheria yetu ya nchi ambayo imeweka viwango na utaratibu mzuri kwa sheria ya utumishi hiyo inataka kwamba kuwe na kiwango maalum na miaka maalum ya uzoefu kwa nafasi hizi zilizokuwa za juu kwa mtendaji mkuu.

Kwa hivyo, hapo nadhani Mhe. Mwenyekiti, hatuna namna sisi ya kusema kwamba mtu asiwekewe viwango, na ulimwengu mzima Mhe. Mwenyekiti, unawekewa viwango kama kuna nafasi

ya juu kabisa ya uongozi lazima uweke aidha miaka mitano au miaka kumi, kwa hiyo, ni kwa mujibu wa sheria za nchi zilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile Mhe. Suleiman Sarahan aligusia kuhusu maeneo ya biashara, katika maneno ya biashara sheria zipo kama nilivyosema sheria ziko nyingi tu Mhe. Mwenyekiti, katika biashara kuna sheria nyingi ambazo zina *guide* mambo ya biashara, kwa hiyo ningeomba tu watu wafate zile sheria na watumie maneno ambayo yamo na yanakubalika katika sheria za biashara zilizoko nchini. Sheria zipo si kama hazipo lakini utekelezaji wake labda watu hawatekelezi, basi tusimamie sheria zile zitekelezwe inavyotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu sheria za viwango kama nilivyosema tunafanya kazi vizuri sisi *ZBS* na *TBS* Bara wana mkataba wa kushirikiana. Vile vile kuna wajumbe wa bodi wa Zanzibar wanatoka shirika hili la *TBS*. Kwa hivyo, tunakwenda vizuri ila kunahitaji mara kwa mara waendelee kuzungumza na waweze kubadilishana mawazo kurekebisha pale ambapo pana kasoro.

Jengine aligusia yeye kuhusu suala zima la kodi. Kwa hivyo, utaratibu wa kodi Mhe. Mwenyekiti, msingi mkubwa wa kodi ni ile *sales* uliyofanya. Siyo kweli kwamba inatolewa tu *arbitrary* yaani inawekwa tu, lakini unaangalia vile vile viwango vilivyowekwa kwa mujibu na taratibu za kodi zilivyo, kwa sababu huwezi kulipiwa kodi *flash hold* na *turn over* ile ambayo ya biashara uliyokuwa umefanya. Hiyo siyo kweli na naomba nimuhakikishie Mhe. Suleiman Sarahan kwamba suala hili linakwenda kwa mujibu wa utaratibu ambao umewekwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nijibu suala la Mhe. Ali Suleiman masuala yake kwanza naomba nikubaliane mengi aliyoyasema ni ya msingi na ya manufaa kwa taifa letu, kweli ni kwamba sheria hii inasisitiza usalama wa vitu tunavyotumia kwa wananchi wetu,

lakini pia inasisitiza kwamba wafanyabiashara nao wapewe nafasi wafanye biashara bila kuonewa, siyo akawa mfanyabiashara akamkandamiza mfanyabiashara mdogo na akamfanya biashara mdogo asipate nafasi ya kufanya biashara kwa sababu mfanyabiashara mkubwa ametumia hila, ametumia ghilba, ametumia ukubwa wake akaweza kumpinga mwenzie mdogo asifanye biashara.

Kwa hivyo, mambo mengi aliyokuwa ameyazungumza Mhe. Ali Suleiman yote haya ni ya msingi na yametia nguvu mswada wetu. Nakubaliana nae kwamba suala la kilimo sasa hivi huu ndio mkakati mkubwa wa serikali kuona kwamba viwanda vyetu tunashajihisha sekta ya kilimo na sekta ya utalii. Niko tayari kutembelea hawa wenzetu walioko Bwejuu Dongwe kwenda kuangalia mradi wao wa ndimu. Kwa sababu ndimu ni moja ya Kiwanda ambacho tunataka kukisimamisha, kwa sababu ndimu unaweza kufanya juisi unauza juisi ya ndimu kwa ajili ya kupikia. vile vile kuna utaratibu wa kutengeneza ndimu ya unga ili kuuza na kupata pesa. Kwa hivyo, Kiwanda cha Ndimu na wale wanaozalisha ndimu naomba niwape moyo sana kuwaambia kwamba tunaangalia uwezekano kumtafuta mtaalam wa kuwasaidia kuweza kutengeneza ndimu ya maji na kutengeneza *vinegar* na kutengeneza vile vile ndimu ya unga ambayo watapata manufaa na wataweza kupata maisha mazuri kutokana na kilimo hiki cha ndimu. Yote hayo Mhe.Mwenyekiti, kama nilivyosema nimeyaeleza katika mswada huu pale awali, namuunga mkono na naomba tushirikiane zaidi na Mhe. Ali Suleiman.

Mhe. Simai Mohammed Said alizungumzia masuala ya leseni za biashara, ni kweli leseni za biashara zipo katika taasisi tofauti na ndiyo maana tukaunda Baraza la Leseni. Baraza la Leseni moja ya majukumu yake ni kuangalia utaratibu mzima wa leseni na jinsi kiwango gani tutaweza kuweka sawa kuondosha usumbufu, kuweka iwe rahisi lakini vile vile kuainisha ni mahali gani mtu

anaweza kupata leseni. Ni kweli leseni moja wakati mwingine inatolewa taasisi kama tano, sita mpaka saba, hiyo nayo inakwamisha utendaji mzuri wa biashara na ndiyo maana Zanzibar tukawa katika nafasi ya chini huko katika utaratibu mzima wa kufanya biashara kwa ufanisi. Kwa hivyo, ili kuweza kwenda vizuri serikali ilipitisha uamuzi kwamba moja ya jambo tunalotaka tulifanye ni kuongeza kasi ya wafanyabiashara na kuwaondoshea Wafanyabiashara usumbufu.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba mjumbe alipendekeza wajumbe katika tume hii watokane na taasisi. Hili pia wamelizungumza wajumbe wengine kwa hiyo sitolirudia tena. Hilo haliwezekani Mhe. Mwenyekiti kwa nini? Kwa sababu Tume hii ni ya wafanyabiashara wanaoshitakiwa pale ni wafanyabiashara sasa hatuwezi kuwatia watu ambao wanawakilisha hizi taasisi kwa sababu itakuwa pale wanalinda maslahi ya watu, tunataka watu ambao wako *neutral* hawako upande wowote.

Kwa sababu kama suala la biashara kwa mfano tunao wafanyabiashara Mhe. Mwenyekiti, ambao tayari wanafanya biashara zile kuna pesa tumeshazipokea nyingi tu sitaki kuzisema hapa, lakini wafanyabiashara wale wengine viongozi wengine ni wajumbe, wengine tunao humu wajumbe ukiwatia kwenye kamati zile wataanza kutetea maslahi yao na hatutaki kufanya hivyo. Maana ya Sheria hizo tunataka kile mtu awe na usawa katika biashara, usawa katika kufanya mambo yao kwa hivyo tukiwatia watu kwa mujibu wa jumuiya zao itakuwa lengo lile Mhe. Mwenyekiti, tunaliharibu. Kwa hivyo hiyo haiwezekani tumelijadili sana na tumeona tufanye hivyo kwa sababu tunataka watu wafanye biashara bila ya mtu mwengine kutumia nafasi yake akaweza kushawishi maamuzi.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, alilozungumza Mhe. Simai Mohammed Said ilikuwa kuhusu ubora wa vyakula kwamba sheria hii tunayoitengeneza inaweza ikawaadhibu watu ambao hawana makosa. Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar tunakwenda na wakati na Zanzibar tunayoitayarisha sasa hivi chini ya uongozi wa Dk. Ali Mohammed Shein ni Zanzibar ya kisasa Mwenyekiti. Mimi ningeomba sana wananchi wa Zanzibar wakaelewa na ndugu zangu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakaelewa hatuwezi kuendelea na Zanzibar hii, ndio maana sasa hivi tunakwenda kwenye *Zanzibar City*, Zanzibar nyengine kabisa inayotengenezwa. *(Makofi).*

Mhe. Rais, Dk. Ali Mohammed Shein ni Rais wa historia unajua unaposoma historia unaambiwa kwa miaka ya makuti 1960 kiongozi wakati ule sipendi kumtaja sana alianzisha mambo ya umeme, majumba ndio maana tunaona sasa hivi Zanzibar ndio ilikuwa ya mwanzo kwa Televisheni ya Mwanzo, mambo mengi ilikuwa ya mwanzo. Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar tunayotaka tuijenge sasa hivi ni Zanzibar hiyo Zanzibar ya kisasa, kwa hivyo kama sasa hivi samaki tunanunua vichochoroni marikiti wanatupwa chini au pwani kule wanatupwa chini haiwezekani Mheshimiwa. Zanzibar hii tuisahau tujenge Zanzibar ya kisasa ambayo mazingira yake yaendane kwa usasa.

Kwa hivyo hii Sheria tuntakiwa mambo mengine tuyarekebishe kwa mujibu wa sheria hii, kuna wafanyabiashara sasa hivi wanauza samaki Mombasa wanatumia vipimo, lakini ukimwambia auze samaki unguja kwa vipimo hawataki. Kwa hivyo hatuwezi kwenda na Zanzibar hii twendeni na Zanzibar ya kisasa, kwa nini nasema hivyo Mheshimiwa hivi leo watu wa mahoteli hawanunui vyakula vyetu kwa nini havilingani na hayo kwa sababu samaki wa chini hanunui mwenye hoteli. Machinjio ya Ng'ombe sasa hivi ambayo hayaendani na kisasa hawanunui wenzetu wananunua nyama Kenya, Bara na kadhalika, kwa hivyo

twendeni na wakati mimi kama Waziri wa Biashara na Viwanda nasema hivi lazima sheria zirekebishwe tujipange vizuri tuweze kwenda na wakati….

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa wajumbe kwa kuwa muda wetu wa kumaliza Waziri kujibu hoja utakuwa hautoshi namuomba Mwanasheria aweze kutengua Kanuni ya muda ili tuweze kuendelea kujibu hoja na baadae jioni tuweze kuipitisha.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko ameshaanza kufanya majumuisho ya hoja yake na kwa kuwa muda hautoshi wa yeye kumaliza, lakini pia kwa Baraza kukaa kama Baraza la kutunga sheria naomba kutenga kando kanuni ya muda ili kumpa muda Mhe. Waziri amalize kufanya majumuisho yake na baadae Baraza likae kama kamati ya kutunga sheria ili tupitishe Mswada huu na kumaliza. Mhe. Mwenyekiti naomba kutoa hoja.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwanasheria Mkuu rafiki yangu kwa bahati mbaya sana hakuitaja kanuni hiyo ya kuondoa muda na kataja tu kanuni ya kuweka kando muda, kwa hivyo kanuni hiyo itakuwa batili na tuendelee kama tulivyo.

Mhe. Mwenasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kanuni ya muda ni kanuni maarufu kanuni ya 25. *(Makofi na Vicheko)*

Mhe. Mwenyekiti: Sasa niwahoji Wajumbe wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Mwanasheria wanyanyue mkono, wanaokokataa waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, nimalizie katika mchango wa Mheshimiwa Simai Mohammed Simai kuhusu sheria zinagongana za kimaaifa, Mhe. Mwenyekiti, sheria hazigongani kabisa za kimataifa kwa sababu hili suala lilifanyiwa kazi na tumeona na tumepitia kila sheria na inakwenda vizuri na itaweza kutuwezesha pahali pazuri.

Leseni kama chombo cha kujipatia mapato Mhe. Mwenyekiti, leseni ni kweli tuliona huko nyuma kama kuna wengine wanaona kama sio kitu cha kupatia mapato, lakini leseni ni chombo vile vile cha kuweza kufuatilia zile shughuli zinazofanywa na vile vyombo, lakini pia kuna *user fee* ambayo kwa ajili ya kuweza kujenga zile *instution* ambazo tunatakiwa tuzijenge. Kwa hivyo kwa upande mmoja leseni ni chombo lakini ni *tools* ya kuweza kuendeleza yale maeneo.

Mhe. Mwenyekiti, nije nimjibu Mhe. Mwinyihaji Makame yeye alizungumzia zaidi masuala ya Mswada na masuala ya Tanzania nimekwisha kuyajibu, lakini niseme tu hili moja chombo ambacho kinachosema kweli sheria yake ambayo haiendani na Zanzibar ni *TFBA* sio *TBS* naomba nikurekebishe sio *TBS, TFBA* ndio ambayo sheria yake haitambui Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kweli inasema kwamba Zanzibar ni nchi ya kigeni. Lakini badi katika mazungumzo tuliyofanya kikao cha mwisho chini ya Mwenyekiti wa Makamo wa Rais wa Tanzania hili suali lilizungumzwa kwa kina na vizuri sasa hivi nimepata taarifa kwamba *ZFBA* na *TFBA* wameshasaini mkataba wa kufanya kazi kwa pamoja, ingawa sisi kama Wizara ya Biashara na Viwanda hatujaona huo mkataba wao, lakini tutakapokwenda kikao chengine itakuwa

tunazungumza haya ili kuona kwa kiasi gani hayo makubaliano yao nayaweza kurahisisha biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara.

Ni kweli hili suala lilikuwa linasumbua lakini *inshaallah* Mwenyezi Mungu anaweza akalifikisha mahali pazuri.

Mhe. Mwenyekit,i vifungu vyengine kama cha 74 alichokizungumza ni kweli sheria hii za kufanya kanuni nimeshajibu, lakini pia sheria hii inatakiwa utulivu, inatakiwa umakini kabisa wa hali ya juu kwa hivyo hayo yote Mhe. Mwenyekiti, tutayazingatia. Lakini pia suala la kuongeza bidhaa katika *Control Goods* nalo tutalifanyia kazi tumeshaona baadhi ya bidhaa za ndani kwa sababu zinasimamiwa na vyombo vyengine kwa hivyo vina- *qualify* kuingia katika *Control Goods* hiyo ina maana kwamba tubadilishe sheria kidogo.

Lakini jengine kuhusu suala la taasisi na Mashirika kama nilivyosema pale mwanzo tutashirikiana tutakuwa na kikao chetu pamoja ili kuona tunafanya vizuri bila ya kuwa na sisi tukaanza kushindana wenyewe kwa wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nijibu Masuala ya Mhe. Panya Ali Abdalla mengi yao nimeshamjibu lakini jibu hili la wajasiriamali ni kweli wajasiriamali ndio wengi hapa Zanzibar wafanya biashara wa Zanzibar wengi wao ni wajasiriamali, lakini na wengi wao hawana elimu ya kutosha kuhusu biasha na wengi wao hawana vifaa lakini wengi wao wanapambana na ushindani wa hali ya juu Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo sheria hii itawawezesha na wao vile vile kuwekewa mazingira ya kuweza kufanya biashara zao vizuri na kuweza kuwaongeza katika ubora na katika bidhaa zao na katika vile vile kufikia mahali pazuri.

Kwa hviyo Sheria hii kama nilivyosema Wizara itachukua jitihada kubwa kabisa kuona wajasiriamali nao, hofu tuliyokuwa nayo sisi moja tu kwamba wajasiriamali kwa sababu watafanya bidhaa zao hizi wanaweza hawa watu wakubwa wakaja wakachukua bidhaa zao wakazitengeneza vizuri zaidi wao wakakosa faida, hilo nalo tumeliona lakini tutawawekea kinga kubwa sana ya kuweza na wao hata kama watashirikiana na wafanya biashara wakubwa kwa sababu inaruhisiwa hiyo kisheria ili na wao vile vile wapate faida kubwa.

Lakini vile vile kuhusu lile la kushauriana na jumuiya tutashauriana kama ilivyo katika vifungu hivi mapendekezo yake mengi mazuri na mimi pia nayakubali na nayaunga mkono.

Kuhusu uwezo wa Tume na kuweka tozo na malipo hasa kwa wajasiriamali nimelizingatia nimeshasema lakini pia kuhusu muundo sifa kwa watakaoteuliwa, Mhe. Mwenyekiti, humu tumeelezea sifa za watakaoteuliwa. Watakaoteuliwa kama wajumbe tumesema wawe na elimu fulani fulani hiyo ni sifa tosha ya kuwawezesha wao vile vile wateuliwe kwa wale ambao tumewasema. Isipokuwa hatuwezi kuwatia watu wa Jumuiya kama tulivyosema pale mwanzo, sifa ya kuondoka ikiwemo mgonjwa na maadili hapo akikosa maadili anatakiwa hiyo ina maana kwamba anasimamishwa, anakosa anafikia ukomo wa kuwa mjumbe.

Kuhusu kukutana kwa mara moja kwa dharura nimelikubali ni marekebisho mazuri, suala la *ZURA*, *ZMA* hizi zitafanyakazi vipi kama nilivyosema, moja kazi watakaofanyiwa *ZURA* na *ZMA* kwa sababu kuna hizi kesi zitakazokuja malalamiko yatakayokuja na mambo mengine wao *ZURA* na *ZMA* na wengine hawa wakitaka kufanyiwa, itabidi nao wachangie kwa kweli hawalipi sio malipo, lakini wanachangia ili hii taasisi iweze kufanya kazi kwa ufanisi

na ndio inavyofanya Bara na nchi nyengine Marekani wanafanya kazi kama hizo.

Kuhusu ushindani nalo hili marekebisho nimeyakubali na hilo la *TBS* nimeshalitolea ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kumjibu hoja zake Mhe. Panya Ali Abdalla nijibu hoja ya Mhe. Miraji Khamis Mussa alitaka kujua sera gani, kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, tunatumia Sera ya Biashara, tuna Sera ya Viwanda mwaka 1989 na Sera nyengine ambazo tunazifanyia mapitio. Kwa hivyo sera ipo inotulazimisha sisi kufanya marekebisho kwa sababu sheria hii sio mpya, sheria ipo tunafanya marekebisho katika sheria ambayo tayari ipo.

Jengine alilozungumzia Mhe. Miraji ni kuhusu soko la huduma na usafiri, soko la huduma na usafiri Mhe. Mwenyekiti, linasimamiwa zaidi na *ZMA* pamoja na *TCRA* na vile vile vyombo vyengine vinavyosimamia masuala ya fedha, lakini sheria hii kwa sababu ina uwezo huo hawa wote niliosema *ZMA* na wengine watakuja kuripoti kunako Tume hii, kwa hivyo kwa ilivyo ina maana kwamba Sheria hii pia inasimamia huduma na usafiri kama ilivyokuwa imejieleza katika Mswada wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, mifano aliyotoa wanalindwa kwa sababu kama *ZMA* wanavyokuwa wanaweka bei za usafiri ni *ZMA* ambao wanaya-*prove* hii bei ya usafiri wa vyombo vya baharini. Vile vile kwa vyombo vyengine wanatakiwa wao vile vile chombo hichi kinachohusu usafiri vile vile washughulikie kama wanavyotakiwa, kwa mfano bei za daladala na kadhalika wanatakiwa wao wafanye. Lakini kama kuna mzozo kama wananchi wanaona hawa wanajumuiya Jumuiya zipo Mhe. Mwenyekiti zimeshaanzishwa lakini hazina nguvu, kwa hivyo tunachotaka kufanya hivi sasa kuziwezesha hizi jumuiya ziweze kufanya kazi zao vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, ikwa upande wa Tume, Tume inao uwezo wa kuanzisha *secretariat* kwa sababu humu kwenye kifungu cha 5(1) na cha 8 vimeeleza mle utaratibu wa kuanzisha *secretariat*. Kwa hivyo sheria hii tayari imewapa *power* Tume kuanzisha *secretariat*. Lakini vile vile kwamba Tume haina uwezo wa kushitaki, Tume inao uwezo ukisoma kifungu cha 4(2)(a) kinaelezea utaratibu wa kuweza kushtaki na kushitakiwa.

Kwa upande wa upatikanaji wa Makamo Mwenyekiti wenyewe marekebisho yamefanywa wenyewe watu wa Tume watakuwa miongoni mwao watachagua Makamo Mwenyekiti ili waweze kuendeleza mikutano yao, la Jumuiya nimekwisha kulisema.

Mhe. Mwenyekiti, sekta ya umma na sekta ya binafsi inatambuliwa Sekta ya umma inajulikana na sekta binafsi inajulikana, sekta ya umma ni Serikali na sekta ya binafsi nayo vile vile ni watu ambao hawamo ndani ya Serikali lakini nakubaliana nae tutaiainisha hii kwenye Kanuni.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kwa upande wa Mrajis wa Baraza atatoka wapi nani atakayemteua huyu Mrajis, Mrajis ni Mwanasheria Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo mwanasheria ni mwanasheria aidha anaweza kuchaguliwa ndani ya Serikali wanasheria wapo wamo ndani ya Serikali, kwa hivyo utaratibu kwamba ni mwanasheria kwa hivyo kuna nafasi nyingi na kuna wanasheria wengi mradi akikamilisha viwango vinavyotakiwa ni mwanasheria na historia yake ya kazi zake basi atakuwa anaweza kuchaguliwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa mhuri kati ya Mrajis na Mwenyekiti haya katika Kanuni tutafafanua na tutaiweka wazi. Kwa upande wa mrajis kuambiwa ni Katibu wa Baraza nalo vile

vile Mhe. Mwenyekiti kama halimo kwenye Sheria tutalifafanua liwekwe wazi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kujibu hoja za Mhe. Miraji Khamis Mussa nijibu michango ya Mhe. Ahmada Yahya, michango yake ilizungumzia zaidi kitengo cha *ZBS* kiimarishwe. Hivi sasa hivi tumo mbioni kuimarisha kitengo hichi, Mhe. Mwenyekiti *ZBS* tayari maabara yao ya mambo ya *electronic* tayari na sasa hivi wanatayarisha maabara mengine pesa zinapatikana katika bajeti wanapewa wanakwenda vizuri Mhe. Mwenyekiti. Bado lakini ipo haja ya kuendeleza zaidi na hiyo kazi bajeti inayokuja tutawaombea vile vile wamalize jengo lao lakini pia waweze kuingia katika maabara nyengine na zaidi wanavyosema wenyewe ni maabara ya mambo ya vyakula ndio nadhani iko haja ya kuyashughulikia.

Kuhusu bidhaa za magari na ujenzi hayo pia tumeona changamoto zipo na *ZBS* nao wako imara kuangalia changamoto hizi, lakini bado kuna haja kuongeza utaalam wa aina hiyo kwa ajili ya maeneo haya kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, nimechukua mchango nimepokea vizuri sana mchango wa Mheshimiwa Ahmada Yahya.

Mhe. Mwenyekiti, wa mwisho ulikuwa ni mchango wako mwenyewe Mwenyekiti Mhe. Shehe Hamad Matar, ulitaka kujua tu kwamba kuhusu masuala ya ukiritimba wa soko kifungu namba sita nafikiri, ulisema kwamba je, watu walipokuwa wanauza bidhaa zao kwa lugha ambayo haifahamiki kwa mfano anatia kwenye bidhaa lugha ya kichina nje kwenye gamba kwa sababu tumesema bidhaa lazima kuwa na *Display* zielezwe kwa lugha inayofahamika hapa Zanzibar. Kama ikiwa ya kiingereza au ya kiswahili ambayo ndio inayofahamika hapa Zanzibar. Je, kama lugha ya kichina au ya kifarsi au ya kifaransa ambayo hatutumii. Mhe. Mwenyekiti, huku ni kwenda kinyume na utaratibu kwa sheria hii lazima lugha ambayo wananchi wanafahamu, kama

huna lugha hiyo basi unatakiwa uitafsiri ili wananchi waweze kununua kitu ambacho wanakifahamu, kwenda kinyume na hicho ni sawa sawa na kuvunja sheria.

Jengine Mheshimiwa ilikuwa kwa upande wa matangazo kwa bidhaa za umeme na gesi kwamba je ile mitungi wanapimaje kama kilo sita kumi na tano wanapimaje. Mhe. Mwenyekiti, nikuhakikishie kitengo chetu cha vipimo wanatakiwa wapime mpaka masuala haya yote na kazi hiyo wanaifanya kwa hivyo hakuna tatizo kubwa katika kupima vipimo katika mafuta na masuala ya gesi. Lakini kama kuna haja ya kuongeza nguvu katika Idara yetu ya vipimo basi nadhani tutaongeza nguvu ili tuweze kuona kwamba hakuna athari na tatizo zinazotokea kwa kuwa mitungi ya gesi ambayo haijafikia ule uzito wa kiwango ambacho kimekubalika, lakini suala hilo wanatakiwa wafanye na wanapita kila mara katika wiki mara mbili au zaidi kupitia maeneo ambayo yanahusika na mambo mbali mbali.

Jengine lililoulizwa na wewe mwenyewe ni kuhusu bei ya bidhaa hasa zaidi kwamba itolewe elimu katika suala zima la bei ya bidhaa ni kweli bei za bidhaa wanatakiwa wafanyabiashara wanavyokuwa wanauza bidhaa zao katika masuala ya *promotion* wanatakiwa nao vile vile watoe elimu kuwafahamisha wananchi juu ya utaratibu mzima na bei zao, na kama wafanya sale vile vile wawafahamihe wananchi mpaka vijijini. Kuna kampuni fulani fulani sasa *hivi* wanafanya kazi hii kwa ufanisi zaidi.

Lingine ilikuwa ni *guarantee* Mhe. Mwenyekiti, unavyosema kwa mfano unanunua bidhaa au vifaa vya *electronic* kwa mfano simu na kadhalika unatakiwa mle kwa sababu wao wanapata *guarantee* na wewe unayeuza unatakiwa pia umpe *guarantee* huyu mtu mdogo mdogo ambaye unampa, wengine wao wanakuwa ni ma-*agent* kwa hivyo tunawaomba hawa ma-*agent* wazungumze na wale ambao ni *supplier* wao wawaruhusu suala zima la kuweza

kuweka *guarantee*, kama *guarantee* haijamalizika kama unatokea ubovu basi yule mnunuzi bidhaa yake kwa mfano kama simu au chombo chake anatakiwa arejeshewe au alipwe ili na yeye kuweza kupata huduma kwa mujibu wa ahadi ambayo ametoa yule mtengenezaji chombo kile au kitu kile.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kujibu masuala yote, hoja zote, michango yote ambayo yaulizwa na Waheshimiwa Wajumbe naomba Mheshimiwa kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa niwaulize wale wote wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri, wasiokubaliana, waliokubaliana wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama kamati ya kutunga sheria ili kuupitia Mswada huu kifungu kwa kifungu. Mhe. Mwenyekiti naomba kutoa hoja.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji ya Zanzibar, 2017

SEHEMU YA KWANZA

Utangulizi

Kifungu 1 Jina Fupi na Kuanza Kutumika pamoja na Marekebisho yake

Kifungu 2 Ufafanuzi pamoja na Marekebisho yake
Kifungu 3 Matumizi ya Sheria hii pamoja na Marekebisho yake
Kifungu 4 Uanzishwaji wa Tume pamoja na Marekebisho yake
Kifungu 5 Kazi za Tume pamoja na Marekebisho yake
Kifungu 6 Uwezo wa Tume pamoja na Marekebisho yake
Kifungu 7 Wajumbe wa Tume pamoja na Merekebisho yake
Kifungu 8 Sekreterieti ya Tume Pamoja na Marekebisho yake

SEHEMU YA PILI

Kazi za Sekretariet

Kifungu 9 Kazi za Sekretarieti.
Kifungu 10 Muda wa Utumishi wa Wajumbe.
Kifungu 11 Maposho.
Kifungu 12 Ukomo wa Ujumbe pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 13 Vikao vya Tume pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 14 Kukasmisha Madaraka pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 15 Kuanzisha Lalamiko pamoja Marekebisho yake.
Kifungu 16 Jumuia za Watumiaji.
Kifungu 17 Uanzishwaji wa Vitengo vya Tume pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 18 Wafanyakazi wa Tume pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 19 Usiri pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 20 Mgongano wa Maslahi pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 21 Fedha za Tume pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 22 Matumizi ya Fedha za Tume.
Kifungu 23 Hesabu na Ukaguzi wa Fedha pamoja na Marekebisho yake.

Kifungu 24 Ripoti ya Mwaka pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 25 Bajeti pamoja na Marekebisho yake.

SEHEMU YA TATU

Baraza la Ushindani Halali

Kifungu 26 Baraza la Ushindani Halali pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 27 Mjumbe Mualikwa pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 28 Mrajis wa Baraza pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 29 Kanuni za Maadili pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 30 Muhuri wa Baraza pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 31 Kuondolewa Ofisini Mjumbe pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 32 Kazi za Baraza pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 33 Uwezo wa Baraza pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 34 Maamuzi na Amri za Baraza.
Kifungu 35 Mishahara na Maposho.
Kifungu 36 Pingamizi kwa Baraza pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 37 Kanuni za Baraza pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 38 Fedha za Baraza pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 39 Matumizi ya Fedha za Baraza.
Kifungu 40 Hesabu na Ukaguzi wa Fedha pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 41 Ripoti ya Mwaka pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 42 Bajeti pamoja na Marekebisho yake.

SEHEMU YA NNE

Mienendo ya Biashara Inayokatazwa

Kifungu 43 Mienendo ya Biashara Isiyo ya Ushindani pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 44 Mikataba ya Biashara Isiyo ya Ushindani pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 45 Kukatazwa kwa Baadhi ya Makubaliano Bila ya Kujali Athari Zake Katika Ushindani pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 46 Kuzuia na Kukataza Kusambaza Bidhaa pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 47 Makubaliano ya Biashara pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 48 Matumizi Mabaya ya Nguvu za Soko pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 49 Miungano na Ununuzi wa Mashirika pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 50 Taarifa Uchunguzi, Kuzuia Miungano ya Makampuni na Ukiritimba Katika Soko pamoja na Marekebisho yake.

SEHEMU YA TANO

Masharti Yanayohusiana na Mienendo ya Upotoshaji na Udanganyifu

Kifungu 51 Mienendo ya Upotoshaji na Udanganyifu.
Kifungu 52 Udanganyifu au Upotoshaji pamoja na Marekebisho yake.

SEHEMU YA SITA

Vitendo Visivyokubalika Katika Biashara

Kifungu 53 Matangazo Yenye Hadaa pamoja na Marekebisho yake.

Kifungu 54 Kukubali Malipo Bila ya Kukusudia au Kutoweza Kutekeleza Usambazaji wa Bidhaa au Huduma pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 55 Biashara Isiyokubalika.
Kifungu 56 Viwango Salama pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 57 Bugudha na Vitisho.

SEHEMU YA SABA

Masharti Yanayohusiana na Kumlinda Mtumiaji

Kifungu 58 Uuzaji wa Bidhaa
Kifungu 59 Kuoneshwa kwa Bei pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 60 Dhamana kwa Bidhaa.
Kifungu 61 Muundo wa Bei pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 62 Wajibu wa Wazalishaji au Wakala wa Bidhaa Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 63 Kuzuia Bidhaa Kusambazwa.
Kifungu 64 Marufuku kwa Bidhaa zisizo salama pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 65 Marufuku kwa Bidhaa Bandia pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 66 Kukamata Bidhaa zisizosalama na Bidhaa Bandia.
Kifungu 67 Kuharibu Bidhaa zisizosalama na Bandia pamoja na Marekebisho yake.

SEHEMU YA NANE

Masharti ya Jumla

Kifungu 68 Maelekezo ya Waziri.
Kifungu 69 Utekelezaji wa Amri na Makubaliano ya Utekelezaji pamoja na Marekebisho yake.

Kifungu 70	Kukinzana na Sheria Nyengine pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 71	Rufaa.
Kifungu 72	Makosa ya Ujumla na Adhabu pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 73	Adhabu ya Papo kwa Papo.
Kifungu 74	Kanuni pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 75	Kufuta na Kubakiza pamoja na Marekebisho yake.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga sheria imeupitia Mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wanaoafiki hoja ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji ya Zanzibar, 2017

(Kusomwa kwa mara ya tatu)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kusimamia Mwenendo wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji ya Zanzibar Nam. 2 ya Mwaka 1995 na kutunga Sheria mpya ya Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji, kuweka masharti bora zaidi na mambo mengine yanayohusiana na hayo kusomwa kwa mara ya tatu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mfunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Niwahoji wale wanaoafiki hoja ya Mhe. Waziri, Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)
(Mswada wa Sheria wa Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Katibu na ahsante Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru kwa utulivu wenu na kuweza kujadili Mswada wetu uliokuwa mbele yetu na kuweza kuupitisha bila ya pingamizi yoyote.

Kabla sijaahirisha Kikao hichi naomba nikazie Kanuni yetu ya Baraza ambayo kuwa inaanza kupingwa pingwa. Kanuni ya 61 naomba ninukuu.

61(b) “Mjumbe aliyekuwepo kwenye Baraza Wakati wa Mjadala atatulia na kukaa kwa heshima mahali pake hatatanga tanga kwenye ukumbi wa mkutano”

Naomba Waheshimiwa Wajumbe kukazia Kanuni hiyo. Pia vile vile Kifungu cha 61

61(1)(b)(i) “Mjumbe aliyekuwepo wakati wa mjadala hatozungumza kwa sauti ya juu.”

Waheshimiwa Wajumbe baada ya hapo nawashukuru sana na natangaza kwamba naakhirisha kikao hichi hadi kesho saa 3:00 za asubuhi kwa vile shughuli za Baraza kwa leo zimemalizika.

(Saa 7:19 mchana Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 08/02/2018 saa 3:00 za asubuhi)